

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA NNE**

**Kikao cha Kumi na Tatu - Tarehe 19 Desemba, 2013**

*(Mkutano Ullanza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA  
MAKAZI:-**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu Zilizokaguliwa za Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kwa Mwaka ulioishia Tarehe 30 Juni, 2012 (*The Annual Report and Audited Accounts of the National Housing Corporation (NHC) for The Year ended 30<sup>th</sup> June, 2012*).

## **WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:-**

Taarifa ya Mwaka ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii (*SSRA*) kwa Mwaka 2011/2012 (*The Annual Report of Social Security Regulatory Authority (SSRA) for the Year 2011/2012*).

### **MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge leo ni siku ya Alhamisi, tunakuwa na Maswali kwa Waziri Mkuu. Kawaida yetu kama Kiongozi wa Upinzani yupo basi ndiye anayeanza. Naona sijamwona. Kwa hiyo, nitaanza na Mheshimiwa Murtaza Mangungu. Mheshimiwa Murtaza Mangungu.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kipindi cha miaka ya 1970 kuja 1980 Serikali ilifanya jitihada kubwa sana kupanua elimu ya juu nchini.

Lakini kutokana na matatizo ambayo hayajaelezeka kipindi kirefu hatujawekeza vya kutosha hivyo kuna upungufu mkubwa sana wa Wahadhiri katika Vyuo Vikuu hasa ukizingatia Sheria yetu ya ajira inatoa ukomo wa kustaafu siyo zaidi ya miaka 65 na maprofesa wote ambao ni *full Professor* wamezidi umri wa miaka 65. Je, Taifa letu tunalipeleka wapi katika Sekta hii ya Elimu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru tu Mheshimiwa Murtaza Mangungu kwa swali lake zuri na labda nianze kwa kusema kwamba *of course* ni la Sera hili na si kwamba ni jambo linagusa sekta moja ya elimu kwa maana ya walimu hapana.

Mfumo ulivyo sasa muhimili wa Mahakama ndiyo ambao umewekewa utaratibu wa kwenda mpaka miaka 65 na kwa ajili ya Majaji wa Mahakama ya rufaa. Lakini Majaji wengine nadhani tuko sawa sawa kama katika utumishi wa kawaida wa miaka 60.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[WAZIRI MKUU]

Kwa hiyo, walimu wengi na wenyewe wako kwenye kundi hilo la miaka 60. Isipokuwa kwa upande wa Vyuo vya Elimu ya Juu kilichopo kwa sasa ni kwamba anaruhusiwa kwa mkataba kuongezewa muda hadi miaka mitano, kwa miaka miwili, miwili, mmoja. Baada ya pale inakuwa ndiyo amefikia ukomo wake. Kwa hiyo, ni kama amefikia miaka 65 kama ilivyo kwa Majaji wa Rufaa. Sasa rai yake ni kwamba pengine katika mazingira tuliyonayo.

Je, isingalikuwa busara pengine kupanua wigo tuongeze muda wa kustaaifu ili tuweze pengine kuziba na kuwa na maprofesa wengi?

Mimi nadhani ni rai nzuri. Inaweza ikaangaliwa, lakini iangaliwe kisera na lazima tutazame mfumo mzima unavyounganishwa na maeneo mengine yote ambayo yanagusa utumishi wa Umma.

Lakini kwa upande mwingine alieleza vile vile kwamba inaonekana kwa sababu katika utaratibu wetu huu wa kukataa maprofesa inawezekana hatukuwekeza sana. *Of course* jitihada zimekuwepo muda wote na pengine kwa sasa naweza nikasema jitihada ni nzuri zaidi kwa sababu ukichukua Chuo cha Nelson Mandela pale ukachukua na Vyuo Vikuu vyenyewe sasa hivi walimu wengi tunaweza kuwapata ambao wanaweza kuijendeleza kwa njia ambayo ni pana zaidi kuliko iilvyokuwa siku za mwanzoni.

Lakini bado pengine nitajaribukuzungumza na Waziri wa Utumishi pamoja na Waziri wa Elimu labda wakae waangalie hiyo rai na *effect* yake kwenye utumishi mpana wa Umma itakuwa ni nini. (*Makof*)

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Nashukuru sana kwa majibu ya matumaini yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ningependa kuuliza swalii moja la nyongeza. Wenzetu hawa ambao waliingga kwenye taaluma ya ufundishaji walikataa kazi zile za maslahi makubwa.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MURTAZA A. MANGUNGU]

Lakini jambo la kusikitisha kabisa kwamba hawakuweza kulipwa pensheni. Mheshimiwa Rais, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, alitoa agizo kwa Serikali yake kwamba wastaa fu hawa Wahandiri wa Vyuo Vikuu walipwe pensheni.

Je, leo Serikali inatamka nini?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, inawezekana nisiwe na jibu sasa kwa sababu ni kitu *very specific* kinalenga kinataka tutoe jibu la uhakika. Lakini ninaloweza kukubaliana tu ni kwamba Vyuo hivi nya Elimu ya Juu vina mfumo wake au *scheme* yake ya pensheni ambayo ndiyo wamekuwa wakiitumia kwa muda mrefu na kuna wakati hapo siku za nyuma nilipata nafasi ya kukutana nao kwenye mkutano mrefu mzuri.

Lakini kulikuwa na mambo mawili. Moja ilikuwa ni kweli kwamba kulikuwa na maeneo ambayo yalikuwa na hitilafu katika malipo yao ambayo tulijaribu kukaa na kujaribu kuyatatua ili waweze kulipwa zile staili zao. Muda mrefu kidogo na maadam umeliuliza leo kwa sababu sijawahi kulipata hapo katikati labda unipe muda tu nita-*cross check* na wenzetu wa Elimu pale, tuone kama lile jambo lilikwisha na kama bado basi nitapata maelezo kwa nini ili tuweze kulimaliza.

Lakini kimsingi tulishalifanyia kazi na tukakubaliana na ni maeneo mengi ambayo walikuwa wameyaleta yaliweza kutatuliwa bila tatizo kubwa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kama tulivyosema maswali kwa Waziri Mkuu ni ya Sera. Mkiuliza Sekta kwa kweli *it is just* siyo sawa sawa. Maana yake unamliza Waziri Mkuu wakati kuna wa *Sector Minister*. Tafadhalri nawaombeni na muwe *brief*, tunaweza ku-*cover* watu wengi. Mheshimiwa *Engineer James Francis Mbatia*.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Nashukuru Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa waziri Mkuu, kasi ya kukua kwa majiji mengi duniani ni changamoto ambayo inatukumba hata kwetu sisi hapa Tanzania. Kwa mfano Jiji la Dar es Salaam kwanza ndio chanzo kikuu cha mapato kwa zaidi ya asilimia 80 fedha ya ndani tunaipata katika Jiji la Dar es Salaam.

Kwa sasa msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam pamoja na majiji mengine yanayokuwa ni janga la kitaifa na linaingiza hasara kubwa sana katika Taifa letu. Kwa sasa Jiji la Dar es Salaam linaweza likatumika kwa usafiri wote yaani usafiri wa maji, reli, barabara, anga hata kwa *tele-conferece* katika kufanya majukumu mbalimbali.

Je, Serikali kwa sasa hivi ina mkakati gani, kwa sasa licha ya mkakati ulioko wa mabasi yaendayo kwa kasi, ili kuondoa janga hili ambalo linatakiwa lipatiwe ufumbuzi wa kupambana na majanga? (*Makofii*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa James Francis Mbatia kwamba msongamano uliopo Dar es Salaam kwa kweli ni adha kubwa. Kwanza kwa jamii yenyewe. Lakini kubwa zaidi hasa ni athari zake kwa uchumi kwa ujumla. Kwa sababu *money hour loss* inakuwa ni kubwa mno, kiwango cha masaa ambayo yanapotea pale ni mengi.

Kwa hiyo, ni kweli ni *concern genuine* kwa kila Mtanzania na hasa sisi wakazi wa Dar es Salaam. *Of course* kwa upande wa Serikali tulikuja na lile wazo la mabasi yaendayo kasi, *of course* miradi imeanza kutengenezwa kujengwa. Lakini bado swali halitabadilika kwa sababu hiyo tu, hata kidogo. Kwa sababu lazima tukubali hilo kwamba idadi ya wakazi imeongezeka mno. Kwa hiyo magari vile vile yameongezeka katika Jiji letu la Dar es Salaam.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI MKUU]

Sasa pengine tunachoweza labda na kumwahidi Mheshimiwa James Mbatia hapa unachohitaji kwanza ni kujaribu kuona katika muda huu mfupi katika hali tunayoliona pale, kwa sababu hata utengenezaji wa barabara nao umeongeza vile vile msongamano kwa kiasi kikubwa sana. Kwa hiyo, haja pengine ni Wizara ya Uchukuzi, wizara ya Fedha, TAMISEMI, Jiji lenyewe, Mambo ya Ndani ya Nchi, hawa wote pengine wakae mapema iwezekanavyo wajaribu kuona katika kipindi hiki cha muda mfupi ni hatua zippi zingeweza kuchukuliwa ili tuweze kuona namna ya kupunguza msongamano ambao sasa unaathiri sana shughuli za Serikali.

Lakini wakati huo huo ni lazima tuendelee kama Serikali kuona jitihada hizi za kujaribu kujenga barabara sijui wanaziita za wapi za juu. *Fly Overs*, lazima zipewe msukumo mkubwa sana. Kwa sababu nchi nyngi zimepambana na tatizo hili. Lakini suluhu imekuwa ni katika kujaribu kupata hizo barabara zina uwezo wa kuweza kubeba magari, kuteremshwa kwenye maeneo mbalimbali.

Sasa pale tunao mradi mmoja ule wa Ubungo lakini hauwezi ku-*provide*, hautatoa jibu kwa msongamano wa Jiji lote la Dar es Salaam. Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa James Mbatia kuwa changamoto hii ni ya Serikali lakini ni yetu wote. Kwa hiyo, nadhani katika hatua hii ya mwanzo ngoja nikubali *challenge* hiyo tuone *immediately* nini tungeweza tukafanya pale.

Lakini nadhani kwa muda mrefu itabidi Bunge nalo liendelee vile vile kushauri na kujaribu kuzungunza na Serikali tuendelee kulitafakari kwa pamoja ukuaaji kwa kasi kwa miji na namna tunavyoweza kukabiliana na huu msongamano katika siku zinazokuja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa *Engineer* James Francis Mbatia, swalii la nyongeza kwa kifupi sana.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Nashukuru Mheshimiwa Spika. Kwa kuwa ni vizuri kuwa na tahadhari, yaani kujikinga na majanga kabla ya janga lenyewe halijatokea na ucheleweshwaji wa kufanya maamuzi haya ulichukua miaka mungi kidogo tangu mwaka 1996 tuliwahi kulijadili Bungeni. Mheshimiwa Waziri Mkuu unaonaje kwamba Wizara hizi ulizozitaja ni sahihi kabisa zikakaa *immediately* na mimi *declare interest* mimi ni mtaalam wa majanga niko tayari kutoa ushauri wangu katika Wizara hizi? (*Makof!*)

**WAZIRI MKUU:** Mimi nafikiri hilo mimi sina ugomvi nalo hata kidogo. Najua ndiyo eneo lako la fani. Kwa hiyo, kama utakuwa na mawazo ya kusaidia tutaona namna ya kujaribu kutengeneza timu ndogo, tuone *initially* nini kifanyike, *utadrive* mawazo yako vile vile tuyachanganye tuone maana ni tatizo letu wote. Kwa hiyo, mimi nita-*appreciate* sana kama utakuwa sehemu ya ufumbuzi wa hilli tatizo. (*Makof!*)

**DKT. ANTONY G. MBASSA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Waziri Mkuu katika nchi yetu hii ya Tanzania kumekuwepo na operesheni mbalimbali ambazo zimekuwa zikianzishwa na Serikali kwa nia ya kuweka mazingira yetu katika hali ya usalama na uzuri zaidi. Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwamba operesheni hizi zimekuwa zikifanya kazi vibaya, badala ya kufanya kazi ile ambayo imekusudiwa imekuwa ikifanya kazi ambayo haikukusudiwa. Ni-*declare interest* kwamba natokea Mkoa wa Kagera ambako ni pembezoni, kumekuwepo na wahamiaji haramu, kumekuwepo na wafugaji haramu na operesheni mbalimbali zimekuwa zikifanya.

Kwa mfano, mwaka jana imefanyika operesheni okoa mazingira ya Kagera, ambayo nia ilikuwa ni kusaka hawa wafugaji haramu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Watendaji waliokuwa wakishughulika katika operesheni hii badala ya kusaka wafugaji haramu matokeo yake wakaingilia kuwakuta wale wafugaji halali ndani ya vijiji ambao walichomewa nyumba zao, ambao mifugo yao ilichukuliwa na wengine hata mazao yao kuharibiwa.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[DKT. ANTONY G. MBASSA]

Lakini mbaya zaidi Mheshimiwa Waziri Mkuu, watu hawa wamefikia mahali wakaanza kuwafukuza wanavijiji ambao wameishi pale miaka nenda rudi kwamba wanaishi maeneo ya Hifadhi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu suala hili limeleta siyo tu hali ya wananchi hawa kuichukia Serikali, lakini vile vile kutokuwa na uhakika wa maisha yao ya baadaye. Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kijiji, Kata ya Kaninha, Kijiji cha Kaninha kumekuwepo na suala hilo ambalo sasa wamewekewa mabango kwamba wanapashwa wahame. Wakati wananchi hao wamekuwepo miaka miaka nenda rudi. Vijiji hivi Mheshimiwa Waziri Mkuu vimesajiliwa .....

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, hiyo hotuba sasa.  
(*Kicheko*)

**DKT. ANTONY G. MBASSA:** Swali Mheshimiwa Waziri Mkuu, vijiji hivi vimesajiliwa na vina Hati ambayo ilitolewa tarehe 1 Septemba, 2012 vijiji vyote viwili. Lakini leo hii Wakala wa Misitu wameweka mabango kwamba wananchi wahame. Nini kauli yako Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu suala hili? (*Makof!*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kuhusu Mheshimiwa Dkt. Antony Mbassa ameweuka mambo mengi sana kwenye swali lake. Lakini pengine kwa hili la mwisho ambalo labda ndiyo ame-focus kwamba ana kijiji pale ambacho kina Hati lakini na chenyewe sasa kwa mujibu wa taratibu zilizojitokeza inaonekana wako ndani ya hifadhi. Hilo nalo linawezekana kwa sababu masuala ya mipaka ni magumu kidogo na kwa sababu wakati vijiji vinapoibuka na wanapokuja kuomba kwamba wanataka kuwa kijiji wakati mwingine swali la kama wako ndani ya hifadhi au hapana huwa halibuki. Baadaye ndiyo linakuja kuibuka mnapoanza kujaribu kwanza kutatua hilo tatizo sasa ndiyo mnaingia sasa kwenye taratibu za kusema waleteni wataalam tuone mpaka umepita wapi. Hatimaye unakuta kijiji kile kipo ndani ya eneo la Hifadhi.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI MKUU]

Kwa hiyo, suluhu ya kweli pale moja ni hiyo, kwamba waachie eneo lile libaki ni kwa matumizi ya hifadhi. Lakini lazima vile vile mseme mnawapeleka wapi? Lakini namna nydingine kutegemea na aina na tatizo lilivyo. Njia nydingine ingekuwa ni ushauri kwamba Serikali kwa nini msifikirie ule mpaka *you know* kuurekebisha ili ku-*accommodate* kile kijiji kiendelee kukaa pale. Lakini nayo itategemea eneo hilo likoje. Kijiji kiko katika mazingira gani kwa sababu mara nydingi Serikali imekuwa *reluctant* ku-*open up* milango kwa ajili ya mambo kama hayo kwa sababu inawezekana maeneo ni mengi mtakuta maeneo mengi sasa yameingia katika mgogoro mkubwa zaidi.

Kwa hiyo, mimi nafikiri nikubaliane na wewe tu kwa maana kwamba basi maadam umelileta kwangu kwa njia ya swali. Hebu ngoja na mimi nipate maelezo, nipate *exactly* kilichotokea ni nini halafu tuone kama kuna njia ya kuweza kusaidia pale. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Antony Mbassa, swali lilikuwa *specific* mno. (*Makofii*)

**DKT. ANTONY G. MBASSA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu wananchi hawa sasa wamewekewa mabango na Wakala wa Misitu kwamba kufika mwezi Januari, 2014 wahame na suala hili kadiri ya maelezo yako linahitaji timu ya wataalam na wewe mwenyewe uweze kuliona likoje. Sasa Mheshimiwa Warizi Mkuu, nikuombe wakati suala hili linasubiriwa kupata ufumbuzi niombe kauli yako kwamba wananchi wale sasa wahakikishiwe usalama wao wakati unandaa timu ya wataalam kwenda kulifanyia kazi Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Ni sawa mimi nafikiri hilo sina ugomvi nalo kwa sababu liko ndani ya uwezo wa Ofisi yetu. Nitakachofanya tutaagiza tu pale kwamba kwa sasa, tatizo utakalolipata hapa kila unaposema ngojeni sasa mpaka tufanye hili, kazi zile ambazo ulikuwa unataka zisifanyike lazima zitafanyika. Kwa hiyo, unauendeaza mgogoro zaidi, unazidi kuwa mkubwa.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI MKUU]

Mheshimiwa Spika, ingekuwa ni kwamba tunakuja tunaleta wataalam kwa wakati huyo *activity* zizifanyike ambazo zinaweza zikaleta mgogoro kuwa mkubwa, kwa kukubalika ingekuwa suluhu ya kweli. Lakini naomba uniachie tu tutacheki na Mkuu wa Mkoa, tutaona namna ya kujaribu kulipatia ufumbuzi kama itaonekana ni jambo ambalo liko katika eneo ambalo si lazima tukaendelea kugombana katika jambo hilo.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi nilikuwa naomba nimwulize swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa kuwa kauli yako ya Kilimo Kwanza, imeitikiwa na watu wengi sana hasa vijijiini na wanapenda kilimo.

Lakini tatizo kubwa ambalo limejitokeza ni zana za kilimo. Hasa Matreka ambayo yalikuwa yanauzwa na SUMA JKT yalikuja kwa wingi wakapunguza bei wakapunguza masharti wananchi wakaitikia kwa wingi na wengi wakachukua fomu wamejiandikisha lakini Trekta zile zimekwisha na hadi sasa hatuelewi ni lini. Trekta zitakuja, maana kilimo ndiyo hicho kinakuja wananchi wanasubiri kwa hamu. Lakini tatizo ni hili nilikuwa naomba uwaeleze Watanzania ili waweze kujua Trekta hizo zitafika lini?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kama Nchi lazima tujitahidi tutoke kwenye jembe la mkono twende kwa kweli kwenye zana bora za kilimo kama tunataka kuongeza uzalishaji hapa Nchini na ndiyo maana juhudzi zile wakati ule zilituwezesha tukapata Matreka kupitia Mkopo laini kutoka India. Tulipata Matreka karibu 1,860. Ni kweli kwamba baada ya kuondoa gharama zile za Bandarini Matreka yalishuka bei na yalimalizika baada ya muda mfupi sana.

Kwa hiyo Serikali bado inaendelea na jitihada hizo za kupata matrekta mengine. Tunaendelea kuzungumza na Serikali ya India kuomba kama tunaweza kupata mkopo mwingine. Ule wa kwanza ulikuwa wa Dolla (*USD*) milioni arobaini (*USD. 40,000,000*).

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[WAZIRI MKUU]

Tunaomba sasa tupate kama *Dollar* milioni tisini (*USD. 90,000,000*) lakini bado mazungumzo hayajakamilika kwa sababu wenzetu walisema kidogo wana matatizo ya kifedha. Lakini nilipokuwa ziara ya China majuzi nilikutana na Makampuni mengi sana na nilijaribu na yenyewe kuyaomba kama inawezekana yaje hapa.

Kwa bahati nzuri nadhani kama Makampuni matatu (3) tumeisha yaunganisha na SUMA JKT na katika zoezi hilo nilichosisitiza ni kwamba badala ya kuendelea kununua Matrepta haya yakiwa yanaletwa yakiwa yamefungwa yaani yako tayari. Basi bora tulete Matreka lakini *not down part* kwa maana kwamba vifaa vile unavyoweza kuvunganisha hapa Nchini. Kwa hiyo tuwe na kiwanda chetu cha kuunganisha Matreka hapa Nchini ili tupunguze gharama zaldi na tuweze kuwa na Matrepta mengi zaldi.

Nilichowaomba tu ni kwamba katika mazungumzo yao kwanza wakubali tuwe na Matreka elfu tatu (3,000) ya kuanzia yaletwe kama yalivyo wakati huo huyo twende sasa kwenye hatua ya pili ya kuanzisha kiwanda cha kuunganisha Matrepta hapa Nchini, ambayo tunaamini na wenyewe watatusaidia kuweza sasa kuwa na utaratibu mzuri zaidi.

Juzi nimecheki na watu wa JKT inaonekana Kampuni moja imeridhia sijaua ni ipi lakini inaonekama Kampuni moja iko tayari tukifaulu hilo nafikiri litapunguza sana kero ya matakwa makubwa sana ya Matrepta.

Mheshimiwa Spika, katika hatua hii ya sasa SUMA JKT walikuwa wameagiza Matrepta karibu 270 au 275 yameishaingia tayari Nchini lakini kwa kiwango cha mahitaji bado ni kidogo sana. Wenzetu wa Zanzibar wameniomba Matrepta 20 kwa bahati nzuri tumesema wapewe Matrepta yote 20. Nadhani wameshakubaliana huko namna ya kwenda kuyatumia.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI MKUU]

Kwa hiyo kwakweli ongezeko la watu kuhitaji ni kubwa na lazima tutafute suluhi la kudumu la kuwa na kiwanda chetu hapa kwa kuanzia kiwe cha kuunganisha lakini polepole tujenge uwezo hata wakuweza kutengeneza kwa sababu inawezekana kabisa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Martha Mlata, swalı la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na nashukuru kwa maelezo mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nilikuwa naomba atusaidie kwamba zile fomu zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya kujaza ili waweze kupata mkopo wa zile Trekta bado zimekuwa zikiwachanganya sana Wananchi kule vijiji.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba atusaidie utaratibu upi ufuatwe ama Wakurugenzi ama Maafisa Kilimo, waweze kuwasaidia wananchi kujaza zile fomu, wengine wanabakia nazo mie niligawa fomu 40 lakini wengi walishindwa kujaza ilibidi wanisubiri mimi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba utaratibu huo ili kuwasaidia wananchi. Ahsante sana. (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ushauri tutauzingatia, tutatoa maelekezo kwa Wizara inayohusika.

**SPIKA:** Jamani hata fomu. Ahsante sana, tunaendelea na Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa fulsa ya kuuliza swalı kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, suala la Ulinzi na Usalama kwenye Nchi ni jukumu namba moja kwa Serikali. Masuala ya ulinzi wa wananchi na Mali zao ni jukumu la Serikali, masuala ya utoaji na upatikanaji wa haki kwa Watanzania ni jukumu la Serikali yetu ya Tanzania.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JOSHUA S. NASSARI]

Sasa kwa sisi ambao tumekuwa wahudhuriaji wazuri wa Magereza, kuwaona Wafungwa na Mahabusu, kuna malalamiko mengi ya watu ambao wamesingiziwa na kubambikiwa kesi na ambayo malalamiko hayo yamekuwa yakifishwa kwenye ofisi za Waheshimiwa Wabunge na ukiangalia mazingira mengi unakuta kweli watu wanapewa kesi za kusingiziwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu, swali langu ningependa kujua tu kwamba hivi ni nia au ni mkakati au nidhamira ya Serikali kutumia vyombo vya dola kuwabambikia au kuwasingizia wananchi kesi?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, si nia ya Serikali kuwabambikia watu kesi, haiwezi kuwa hiyo ndiyo nia ya Serikali hapana, lakini itategemea kesi na kesi.

Kwa hiyo, kama una kitu *specific* ambacho unataka kuomba tu Serikali ikitazame basi linaweza kuangaliwa kwa maana hiyo ya kesi maalum ambayo unadhanu mtu katika kesi hiyo amesingiziwa, kwa sababu ni mchakato lazima uwe na maelezo fulani kwenye jambo fulani.

Lakini haiwezi kuwa kwa ujumla wake tu kwamba wote waliomo mle ni kesi za kubambikizwa hapana. Sidhani kama itakuwa sahihi sana kwa hiyo kama kuna kitu maalum basi tutaomba tu nione ni lipi halafu nione namna ya kuweza kusaidiana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Godbless Lema or Mheshimiwa Joshua Nassari.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Lema ni kaka yangu hujakosea sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu nashukuru kwa majibu mazuri na umesema pengine *specific cases*. Mimi ningependa nitolee mfano kesi moja ya *specific*. *Kwamba kuna kijana mmoja .....*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nassari!

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Ninatoa mfano wa *case specific* Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nassari halafu ikawaje?

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Ninatoa mfano wa *case specific*, ili Mheshimiwa Waziri Mkuu aelewe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joshua Nassari, siyo hadithi ndefu!

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Ndiyo Mheshimiwa Spika. Kuna kijana mmoja sasa alishikwa Nzega, akawekwa ndani Nzega, akachukuliwa akapewa kesi ya kulipua kwa mabomu Kanisa la Olacity, Arusha na kwenye mukutano wa Chadema Soweto, huko huko Arusha. Akawekwa ndani (mahabusu/gerezani) Kahama, akatolewa ndani Kahama, akapelekwa Shinyanga, akatoka Shinyanga akawekwa ndani Mwanza kwa siku nyingi sana, akatoka Mwanza akapelekwa Arusha na baadaye wakati anahojiwa .....

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mnyamaze, mimi ndiye ninayeongoza kikao. (*Makofî*)

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunilinda.

**SPIKA:** Mheshimkiwa Nassari na wewe uwe *brief*.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, nitakuwa *brief*, ahsante sana.

Yule kijana akaambiwa kwamba aseme na akubali kosa. Kwa mteso makubwa akavunjwa mguu akaminywa sehemu za siri, kwenye msitu kule Makuyuni akiwa safarini baada ya kiwanda cha Minjingu akiwa amechukuliwa na polisi kupelekwa Arusha. Akaambiwa aseme kwamba aliyemtuma kulipua yale mabomu Kanisani na kwenye Mkutano wa Chadema ni Mheshimiwa Goodbless Lema, na ametumwa yeye akiwa na Mkenya mmoja anaitwa Kamau na amewekwa ndani kuanzia mwezi Agosti, 2013 mpaka juzi siku ya Jumatatu, tarehe 16 Desemba, 2013 kwa miezi minne (4).

Sasa baadaye wakati anahojiwa Arusha akasema kwamba wakati Kanisa linalipuliwa nilikuwa niko Gerezani kwa kesi nydingine na hapo ndipo wakaamua kumwachia. Ningependa kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu atuambie, hivi kweli huu ni mkakati wa Serikali kujaribu kuwanyamazisha viongozi wa Upinzani hususan viongozi wa Chadema kwa kuwapa kesi? Kwa sababu yule kijana yupo na yuko tayari kuzungumza jinsi mteso alivyoyapata na jinsi ambavyo alikuwa anasukwa ili awape kesi viongozi wa Chadema.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joshua Nassari, sasa siyo swalii kwa Waziri Mkuu, hiyo ni hotuba sasa.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, swalii ningependa kujua kwamba ni mkakati wa Serikali kunyamazisha viongozi wa upinzani hususan Chadema kwa stabili hiyo ya kuwapa kesi? Kijana mwenyewe yuko pale juu na yuko tayari kuzungumza.

**SPIKA:** Mkiendelea namna hiyo hamtaruhusiwa kusema.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, unajua kwanza siyo rahisi kwa Waziri Mkuu kujibu hili swali kwa namna ulivyoileza, haiwezekani. Yaani wewe una taarifa zote amepelekwa wapi, akawekwa wapi, akatoka pale akafanya nini, halafu unasema Waziri Mkuu una sema nini hilo. *Mimi is not so easy oky!* Kimoja tu ambacho nataka niseme, suala lile la kulipua Bomu la Kanisa la Olacity, Arusha na baadaye kwenye uwanja ule wa Soweto.

*Take it from me halikuwa jambo dogo hata kidogo na presha kubwa imekuwa kwamba watu wanataka wajue nani alilipua na kwanini alilipua. Sasa juhudzi za Serikali zinaendelea katika kujaribu kuona nani alilipua na kwanini alifanya hivyo.*

Sasa wewe maelezo ullaonipa haya kwasababu mimi siyajui. Sana sana ninachoweza kukuambia tu kwamba yaha ndiyo mambo unatakiwa uyaandikie kwa kina, nipe nitaipa Wizara inayohusika watazame ukweli wa hayo unayoyasema halafu kama kuna maeneo ambayo pengine tumekosea, wako tayari watu kusema kwa nini umefanya hivi kwa nini umefanya hili. Hilo linawezekana kabisa lakini kutegemea kwamba nitaweza kujibu sio rahisi sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Godbless Lema na wewe uwe brief usiwe kama alivyofanya mdogo wako. (*Makofii*)

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni dhahiri kabisa kwamba lile Bomu la Olacity na Bomu la Soweto, lilifanywa .....

**SPIKA:** Mheshimiwa Godbless Lema, naomba ukae. Kwa mujibu wa Kanuni zetu, huendelezi swali lililokwisha tangulia. Hatuendelezi hivyo, sasa kama wewe una swali lingine sema, tafadhali.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika, kwa leo hii ni *concern* yangu, kwa sababu mlitaka kuniua na mnataka kunitengenezea kesi. Kwa hiyo sitokuwa na swali lingine kama hili sitoweza tena kuliboresha zaidi. Kwa sababu yule ambaye aliambiwa anitaje mimi kwamba nimempa mabomu yuko amekaa pale sasa kwa kweli yuko *emotional* na ninaumia sana kwamba nimetaka kuuwawa, halafu ninapewa na kesi ya *murder case*. Kwa hiyo sina swali lingine.

**SPIKA:** Kwa hiyo wewe mshirikiane na Mheshimiwa Nassari mkaijenge hiyo hoja mnayoisema na kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu, mpelekeeni. Tunaendelea na anaefuata ni Mheshimiwa Godfrey Zambi.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi nimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu swali na swali langu ni fupi sana. Moja ya kero kubwa sana katika Nchi na hususani alipotembelea Mkoa wa Mbeya Mheshimiwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Abdalhaman Kinana, ilikuwa ni kwa walimu wengi kuendelea kuidai Serikali mpaka sasa na kwa Mkoa wa Mbeya peke yake kuna madeni karibu bilioni sita (6) kwa walimu. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kuwalipa walimu wote Nchini na haiendelei kudaiwa tena?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikubali tu, nikiri kwamba ni kweli yapo malimbikizo kwa upande wa walimu lakini si walimu tu hata watumishi wengine. Lakini tunayo vile vile madai ambayo yanatokana na huduma mabali mbali ambazo zimetolewa na vyombo mbali mbali Serikalini.

Lakini kubwa ninaloweza kusema kwamba muda wote tumeendelea kujitahidi kulipa hayo madeni. Tatizo lake tu kwamba ni lazima tupitie kwenye mchakato wa kujiridisha kwenye madai yenye kama hatua muhimu sana. Baada ya pale ndipo tunapeleka Hazina na utaratibu wa kawaida wa malipo unaendelea.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI MKUU]

Kwa hiyo tumekuwa tukijitahidi tumelipa sana na nadhani kiasi ambacho tumbaki nacho kwa taarifa niliyopata juzi, karibu sehemu kubwa wameshafanya uthibitishaji wa uhalali wa yale madeni. Kwa hiyo nataka nikubaliane na Mheshimiwa Godfrey Zambi na kazi yangu mimi nikuendelea kulisukuma kwasababu ni kitu na mimi kinanikera. Kwa hiyo, naamini muda si mrefu tutakuwa tumemaliza hili tatizo.

Lakini la pili tuliofanya kwa mifumo hii ya Elektroniki ambayo imeanza kutumika tumejitatihidi sana sasa tumefikia hatua nzuri, ambayo itatuwezesha kwa kiasi kikubwa kutokuwa na malimbikizo tena hii nayo itakuwa suluhu ya kweli katika zoezi zima ambalo limekuwa likisababisha malimbikizo ya muda mrefu. Kwa hiyo, tukifika hatua hiyo nafikiri jambo hili litakuwa limekwenda vizuri.

**MHE. GODFREY ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, walimu wanapata matatizo haya mengi kutohana pia na ukweli kwamba kuna vyombo vingi ambavyo vinashughulikia masuala yao. Kuna Wizara kama Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji, Ofisi ya Rais, Sekretariat ya Utumishi wa Umma, sjui Wizara ya Fedha.

Nini mkakati wa Serikali au kwanini Serikali isitamke kuwa na chombo kimoja ambacho kitashughulikia sekta ya Elimu katika Nchi ili kuondoa matatizo hayo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, moja ya jambo ambalo lazima tukubali kwanza kwamba walimu ni asilimia zaidi ya hamsini (50) ya Utumishi wa Umma kwa sasa.

Kwa hiyo, ni kundi kubwa na unapokuwa na kundi kubwa la Utumishi kama hili, ni dhahiri kabisa kwamba matatizo mengine kama haya yanaweza yakajitokeza. Lakini kubwa ni kwamba tusikubali yaendelee ikawa ndiyo kila siku utaratibu wa namna ya kushughulikia tatizo hili. Ndiyo maana nimesema analolisema Mheshimiwa Godfrey Zambi na sisi tumelitazama. Pengine ni kwa sababu ya wingi wao.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI MKUU]

Lakini tukasema hapana, hiyo peke yake haiwezi kuwa ndio sababu. Lazima kuna sababu nydingine ambazo lazima na zenyewe zitazamwe kwa pamoja. Kwa hiyo mimi ninachowea kumwahidi Mheshimiwa Godfrey Zambi, ni ile tu kwamba jambo hili tumekuwa tukilifanyia kazi kwa muda mrefu sana kama Serikali na nimwambie tu kwamba tulipofika kwa kweli mie naamini tukishamalizana na hili tatizo katika hatua hii ambayo tumefikia kwa sehemu kubwa kabisa hili jambo litakuwa limekwisha. Tumetazama sana wazo hilo la kuwa na chombo maalum kwa upande wa walimu lakini nacho kina changamoto yake.

Kwa hiyo tumesema hili si jambo la kuharakisha. Kwanza tuone kwa nini wengine hawapati tatizo kama hili na walimu ndio iwe tatizo kubwa. Tukitatua hilo mimi naamini litatufikisha pazuri halafu baadye ndio tuje tuone uwezekano wa chombo na nini maana yake, illi tuweze kuainisha na mifumo mingine ya Utumishi. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu ya maswali uliyouliiza. Waheshimiwa Wabunge safari hii mmejitokeza kweli kweli, lakini ndio hivyo haiwezekani. Kwa hiyo, wale wengine bahati mbaya ni mpaka siku nydingine. Katibu tuendelee. (*Makofii*)

### **MASWALI YA KAWAIDA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa Maswali ya Kawaida pia tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu na atakayeuliza swali la kwanza ni Mheshimiwa Dkt. Henry Shekifu.

Na. 149

### **Tatizo Sugu la Maji Mji wa Lushoto**

**MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na ongekezo la watu pamoja na uchakavu wa miundombinu ya kusambaza maji

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU]

kwenda Mji wa Lushoto, kumesababisha tatizo la maji katika Mji huo kuzidi kuwa kubwa.

- (a) Je, Serikali imejipanga vipi kutatua tatizo hili sugu la maji katika Mji wa Lushoto?
- (b) Mwaka 2012/2013 Halmashauri iliomba fedha za dharura shilingi milioni 450 ili kupunguza uzito wa tatizo la maji kwa kuongeza maji kwenye matenki ya Kwembago kutoka kwenye chanzo cha maji cha Kibohelo.

Je, Serikali inatoa kauli gani sasa kutohana na ahadi yake kwamba ingetoa kiasi hicho cha fedha?

### **NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Henry Daffa Shekifu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, (a) hali ya upatatikanani wa maji safi na salama katika Mji wa Lushoto ni asilimia 60 hivyo bado ipo changamoto katika huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hiyo katika Bajeti ya mwaka 2013/2014 Serikali imetenga shilingi milioni 450 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji.

Kazi zitakazofanyika ni pamoja na kuweka mtandao wa bomba katika chanzo cha maji Kibohelo, hadi Magamba na kutoka Magamba mpaka Maguzoni kujaza Tanki ujazo wa lita 225,000 kutoka Maguzoni mtandao huu utapeleka maji Mjini Lushoto. Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto inaendelea na jitihada za kufuatilia fedha hizo kutoka Hazina ili ziweze kupatikana kwa ajili ya kazi zilizopangwa.

Aidha, katika mwaka ujao wa fedha wa 2014/2015, Serikali imepanga kuweka katika Bajeti shilingi milioni 561 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji mjini Lushoto.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAMISEMI]

(b) Mheshimiwa Spika, shilingi 450,000,000 zilizoombwa katika mwaka 2012/2013 zililenga kupunguza uzito wa tatizo la maji kwa kuongeza maji kwenye matenki ya Kwembago kutoka kwenye Chanzo cha Maji cha Kibohelo.

Aidha, tathmini iliyofanyika kwa kushirikisha wataalam wa Wizara ya Maji imebaini kuwa gharama halisi za kutekeleza mradi huo ni shilingi milioni 260.2. Halmashauri iliandika barua ya tarehe 2 Desemba, 2013 kwa ajili ya kukumbushia upatikanaji wa fedha hizo, kutoka Wizara ya Maji na tayari Wizara imetoea shilingi milioni 150.0 tarehe 16 Desemba, 2013. Ufutiliaji unaendelea ili fedha zilizobaki ziweze kupatikana kwa ajili ya kazi hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Henry Shekifu swali la nyongeza.

**MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri na pia nichukue nafasi hii kumshukuru sana Waziri wa Maji na Naibu wake pamoja na Watendaji wa Wizara ya Maji. Baada ya kuwatemebelea walitoa hizo milioni mia moja na hamsini (150,000,000/=). Lakini kama walivyosema katika jibu lao la msingi mahitahi ya mwanzo ya kupunguza tatizo ilikuwa 450,000,000 mtaalam wao alipokwenda alisema 260,000,000/= wametoa 150,000,000=/. Je, huoni kwamba hata lile lengo la kupunguza tatizo halitafikiwa?

Mheshimiwa Spika, swali namba mbili la kisera ambalo ningeomba Waziri wa Maji ajibu. Sera ya kupeleka maji katika miji midogo inatamka kwamba kwa sasa Miradi ya maji ya miji midogo itashughulikiwa na Mamlaka za Maji kupitia Benki ya Dunia. Uzoefu unaonyesha wazi kwamba benki ya dunia kwa kweli wanachelewesha sana katika utekelezaji wa miradi hii kama tulivyoona katika vijiji kumi. Kwa sasa hakuna uwazi wa maelezo yoyote unapotaka kujua miradi ya maji ya miji midogo. Serikali inatamka nini na ni kwa nini tuendelee na Benki ya Dunia katika utaratibu huu ambaa unaafisha utekelezaji?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Henry Shekifu, Mbunge wa Lushoto. Fedha ambazo zimepelekwa Lushoto ni hatua ya kwanza ili kazi iliyopangwa itekelezwe, baada ya mkandarasi atakayewekwa kukamilisha kazi kwa hatua hiyo kwa shilingi 150 milioni fedha zilizobaki zitatolewa kwa ajili ya kukamilisha kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha fedha za ziada shilingi 461 milioni zimepangwa katika kupelekwa Lushoto ili kuhakikisha kwamba tatizo hilo linaondoka. Kuhusu upelekaji maji katika miji midogo, ni kweli kwamba miji mingi midogo ya Wilaya na miji midogo kama Makambako, Lushoto, Mombo na kadhalika, ina matatizo makubwa sana ya maji sasa hivi.

Tumefanya juhudu kuondoa matatizo ya maji katika miji mikubwa, miji mikuu ya mikoa na kupeleka nguvu kubwa vijijini. Ni kweli kwamba tatizo la miji midogo bado litabaki lakini kuanzia Bajeti ya mwaka huu (2013/2014) na mwaka unaokuja (2014/2015) tutaanza kuweka nguvu katika miji mikuu ya wilaya na miji midogo ili kuhakikisha kwamba kwa ujumla tatizo la maji hapa nchini linapungua kwa kiasi kikubwa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Anasema Benki ya Dunia achana nayo sasa utajibuje? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Benki ya Dunia ilipewa jukumu na *partners* wetu hawa wa Maendeleo katika kusimamia utekelezaji wa miradi kama mlivyoona mwaka jana 2012/2013 tuliamua kuondoa *no objection* kutoka *World Bank* katika miradi ya vijijini na hivyo hivyo katika miradi hii ya maji ya miji midogo.

Kwa hiyo, tutaendelea kufanya hivyo hivyo pale ambapo tunaona kwamba inaharakisha utekelezaji wa miradi. Ukweli ni kwamba *Donors* hawa pamoja na Serikali wanachangia kwenye *Water Sector Development*

[WAZIRI WA MAJI]

*Programme.* Benki ya Dunia siyo inayotoa fedha yenyewe, *donors* wengi wanashiriki katika jambo hili na wako ambao wanataka Benki ya Dunia lendelee kutoa *no objection* na wako wale ambao kwa kweli hawapendi mlolongo huu uendeleee. Kundoa mlolongo huo katika vijiji umepunguza sana ucheleweshaji wa kazi na tutaendelea kuhakikisha kwamba kazi hazichelewi kutokana na mlolongo huu wa *World Bank*.

Na. 150

### **Uuzaji wa Dawa za Uzazi wa Mpango**

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT** aliuliza:-

Baadhi ya maduka ya dawa huuza dawa za Uzazi wa Mpango na baadhi ya akina mama hununua dawa hizo na kuzitumia pasipo maelekezo ya Daktari:-

(a) Je, ni sahihi kuuza dawa hizo bila udhibiti wa cheti cha Daktari?

(b) Je, ni nini madhara yanayoweza kuwapata watumiaji wa dawa hizo bila kufanyiwa uchunguzi wa afya zao?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII**  
aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Andrew Clement, lenye sehemu a na b kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa sasa kuna mikondo miwili ya upatikanaji wa dawa za uzazi wa mpango. Mkondo wa kwanza ni kuititia Vituo vya Huduma za Afya vya Serikali vyenye wataalam waliopata mafunzo maalum kwa ajili ya utoaji wa huduma za uzazi wa mpango bila malipo.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII]

Mkondo wa pili wa upatikanaji wa dawa ni kuitia maduka ya dawa yaliyoidhinishwa na vituo vya watu binafsi vya kutolea huduma hizo. Uuzaji wa dawa za Uzazi wa Mpango katika maduka ya dawa yaliyoidhinishwa hauhitaji uthibitisho wa cheti cha daktari isipokuwa ni sharti muuzaji awe na elimu na ujuzi wa matumizi ya dawa hizo kwa lengo la kutoa maelekezo sahihi kwa mtumiaji.

Maelezo kwa mtumiaji ni pamoja na jinsi dawa inavyofanya kazi, ufanisi, faida za dawa na maudhi madogo madogo ambayo anaweza kupata mtumiaji. Hata hivyo si dawa zote zinaruhusiwa kuuzwa katika maduka ya dawa. Dawa zilizoruhusiwa kuuzwa katika maduka ya dawa ni kondom na vidonge tu ambazo hazihitaji uchunguzi wa afya. Dawa nyingine zote hutolewa katika Vituo vya Afya baada ya mteja kufanyiwa uchunguzi na kupata ushauri kufuatana na dawa atakayolchagua.

(b) Mheshimiwa Spika, dawa za uzazi wa mpango kama dawa nyingine zozote zinahitaji uchunguzi wa afya na ushauri kabla ya kuzitumia. Endapo mtumiaji hatafanyiwa uchunguzi wa afya na ushauri kabla ya kuzitumia, dawa hizi zinaweza kuathiri ufanisi wa dawa.

Aidha, iwapo mteja ana matatizo ya kiafya kama shinikizo la damu kuna uwezekano wa kuongezeka kwa hali hiyo.

Hata hivyo wateja wote na watumiaji wa njia za Uzazi wa Mpango wanashauriwa kuonana na wataalam wa afya iwapo watapata au kuona mabadiliko yasiyo ya kawaida baada ya kutumia njia ya Uzazi wa Mpango.

Serikali kuitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, inatoa wito kwa jamii kuwa kabla ya kutumia dawa za Uzazi wa Mpango ni muhimu kuonana na wataalam wa Huduma za Afya kwa ajili ya uchunguzi na ushauri. (*Makof!*)

**MHE. AMINA ADREW CLEMENT:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Tanzania ilipoamua kuleta mpango huu wa uzazi wa mpango ulikuwa una malengo.

Je, hivi sasa tayari tumeshafikia malengo hayo ya matumizi ya madawa hayo?

Swali la pili. Je, hivi sasa tuko katika asilimia ngapi ya matumizi ya madawa hayo? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, lengo la matumizi au kiwango cha Watanzania ambao wanalengwa wawe wanatumia uzazi wa mpango ni asilimia 60 kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo ya Milenia.

Lengo namba tano (5) ifikapo mwaka 2015 na hivi sasa kiwango cha matumizi ya uzazi wa mpango kwa mujibu wa tafiti za hali ya afya na idadi za watu yaani *demographic and survey* ya mwaka 2010 ni kiwango cha asilimia 27 hivi sasa ndio wanatumia. Kwa hiyo, tuna upungufu ya kiwango cha watu ambao bado wanatakiwa kutumia uzazi wa mpango. Tunaendelea kuelimisha watu zaidi ili angalau hiyo asilimia 60 ifikapo mwaka 2015 iweze kufikiwa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa nani yule, kwanza niite na wanaume Mheshimiwa Malocha.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Rukwa ni tegemeo kwa wananchi wa wilaya zote katika mkoa huo na mkoa wa Katavi lakini kwa sasa inakabiliwa na ukosefu wa daktari bingwa baada ya daktari aliyekuwepo kustaaifu.

Je, ni lini Serikali itapeleka daktari bingwa haraka ili kunusuru maisha ya wananchi wa mkoa wa Rukwa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:**

Mheshimiwa Spika, changamoto ya uwepo wa madaktari bingwa katika hospitali za mikoa tunazifahamu na taratibu zipo za kuwezesha wataalam wetu kuweza kupata mafunzo kukamilisha fani zao za kuwa madaktari bingwa na baadaye Serikali kuwapatia nafasi za kwenda kufanya kazi.

Bado kwenye utaratibu huo pamoja na kuzipandisha hadhi hospitali hizi lengo lake kubwa ni kuwawezesha angalau wataalam wetu wawe wameliza kozi ya udaktari bingwa na wale ambao wamemaliza labda wanapangwa kwenye vituo, kutokana na idadi yao kutotosheleza, lazima kwa kipindi fulani tutaendelea kuwa na upungufu kwenye baadhi ya hospitali.

Lakini tutaangalia kwenye hospitali hiyo ya mkoa wa Rukwa ili tuweze kuona madaktari waliopo na ambao wanaweza wakapata nafasi za ajira kwenye kipindi kinachofuata na wale ambao watakuwa wamemaliza taaluma yao ya ubingwa tuweze kuwapanga katika maeneo mengineyo ikiwepo mkoa huo wa Rukwa. (*Makof*)

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imejitahidi sana kuhamasisha suala la uzazi wa mpango na hivi sasa vilevile kina baba wamekuwa wakihamishwa kujunga na uzazi wa mpango.

Je, ni kwa kiwango gani akina baba wamekuwa na mwitikio wa kujunga na mpango huo wa uzazi wa mpango?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:**

Mheshimiwa Spika, kiwango cha matumizi ya uzazi wa mpango miongoni mwa anababa bado ni kidogo sana. Ni kiwango kidogo sana cha wanaume ambao wanajitokeza. Kwa mfano katika kufanya na kutumia njia ya *vasectomy* ni kwa kiwango kidogo sana. Lakini tuje katika matumizi ya *condom*, kiwango ni kikubwa sana miongoni mwa wanaume wanaotumia *condom*. (*Makof*)

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kwa kuongezea majibu ya Naibu Waziri ya Mheshimiwa Kasembe, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni sahihi kabisa kwamba bado tuna changamoto kubwa ya kushawishi akinababa kujunga katika mbinu za uzazi wa mpango. Hivi sasa katika nchi yetu kama alivyosema Naibu Waziri ni asilimia 27 ya wanawake ambao wanahitaji uzazi wa mpango ambao wanatumia uzazi wa mpango. Bado kuna mahitaji ambayo hayajakidhiwa ya asilimia 25 na tatizo kubwa ni upungufu wa vifaa vya uzazi wa mpango.

Takwimu hizo tunazozizungumzia ni kwa upande akinamama, lakini kwa upande wa wanaume bado kiwango ni kidogo mno, kiasi cha kwamba tunahitaji kuendelea kutoa elimu kuwaelekeza wanaume kwamba uzazi wa mpango siyo lazima ufanywe na kinamama peke yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wito wetu ni kwamba wanaume wahamasike wajitokeze katika kuhakikisha kwamba na wenyewe wanashiriki kikamilifu katika uzazi wa mpango ili tupunguze. Sasa hivi Tanzania *fatality rate* ya mwanamke yaani wastani wa idadi ya watoto kwa kila mwanamke mmoja wa Tanzania ni watoto watano nukta nne ambayo ni kiwango kikubwa sana ni lazima tushuke hapo, lakini kwa mara nyingine tena suala hili lisiwe la wanawake peke yao ni letu sote. (*Makofii*)

**SPIKA:** Haya Waheshimiwa Wabunge, tuishie hapo hapo. Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse, atauliza swali lake.

**Vitendo vya Kikatili Vinavyofanywa na Askari wa Wanyamapori**

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE** aliuliza:-

Askari wa Wanyamapori katika hifadhi zetu wamekuwa wakifanya vitendo vya kikatili dhidi ya wananchi kama vile kuwabaka akina mama, kupiga na kuua au kusababisha ulemavu kwa wananchi, ng'ombe kupigwa risasi na kadhalika(a)      Je, Serikali inajua hayo?

(b)      Kama ndiyo, je, imechukua hatua gani ili kukomesha kabisa matukio hayo ya kinyama dhidi ya wananchi wetu na mifugo yetu?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Israel Yohana Natse, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu a na b kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imepokea tuhuma kuhusu askari wa wanyamapori ambazo zimebainishwa kwenye swali la Mheshimiwa Mchungaji Israel Yohana Natse, Mbunge wa Karatu.

Mheshimiwa Spika, watumishi wote na hapa nikimaanisha askari wetu wote wa wanyamapori wanaofanya katika mapori yetu waliotuhumiwa au watakaotuhumiwa kuhusika katika vitendo vilivyoainishwa na Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse katika swali lake wataendelea kufikishwa kwenye vyombo vya sheria ili kuruhusu sheria kuchukua mkondo wake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse, swali la nyongeza Haaa! Kama mnalijua wote.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kutoa majibu mepesi kwa maswali mazito. Naomba kuuliza maswali mawili. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii amekiri kupokea tuhuma. Je, ni askari wangapi au watumishi wangapi ambao wamekwisha kufikishwa kwenye vyombo vyoma?

Swali dogo la pili. Kupokea tuhuma ni jambo moja, lakini hata sasa maeneo mengi, hata kwa mtoto wa Mkulima kule Katavi, Tabora, Serengeti bado vitendo hivyo vya kikatili vinaendelea kutendeka. Naomba kufahamu Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wanataka kuwaambia nini wafugaji wote nchini juu ya vitendo vya kikatili dhidi ya mifugo ya wananchi vinavyoendelea hata sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nimhakikishie tu kwamba Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse kwamba jibu letu la msingi la Wizara la kuwakamata watuhumiwa wote ambao watatumia vyeo vyao kama askari kwa kunyanya wa wananchi. Kama hizo tuhuma zimethibitishwa ahadi ya Serikali ya kuwakamata na kuendelea kuwakamata na kuwapeleka kwenye vyombo vya sheria siyo jibu jepesi ni jibu ambalo linalinda na kuzingatia maslahi ya msingi ya haki ya kila mwananchi na wajibu wa Serikali wa kuilinda haki hiyo.

Ningependa pia niseme kwamba tunaweza na tutajiandaa kumpatia takwimu ambazo Serikali inazo za watu ambao katika vipindi mbalimbali tumeendelea kuwakamata baada ya tuhuma zao kuthibitishwa na kuwapeleka katika vyombo vya sheria ikiwa ni pamoja na kuwafungulia mashtaka yanayohusika.

Kipengele cha pili cha swali lake ningependa tu kujibu kwa ujumla kwamba vitendo ambavyo Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse anavisema hapa vya kunyanya wa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII]

wananchi, kubaka, kupiga na uonevu ni vitendo ambavyo Serikali haiwezi kuvivumilia kabisa. Kwa vyovyote vile napenda kutoa onyo kwa watumishi wote nchini ikiwa ni pamoja na askari wa wanyamapori wajihadhari na wahakikishe kwamba wanafanya kazi zao kwa mujibu wa sheria zilizopo.

**MHE. MOZA ABEID SAIDY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, nami napenda kumwuliza swalii la nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, pamoja na majibu yake mazuri, ningependa kujuia kwa kuwa wakati huu ni wakati wa masika na kwa kuwa askari wako wanatumia nguvu na kuwachomea wananchi nyumba na kuwahamisha katika maeneo kwa kutumia shuruti.

Je, Serikali inatoa wito gani kwa wananchi wote kuhusiana na wakati huu wa kilimo, wewe kama Mheshimiwa Waziri na Serikali yako kwanini isiwape muda wananchi wale wakaendelea kukaa katika eneo lile wakaweza kulima na askari wako ukawapa maelekezo yaliyokuwa mazuri ili wasitumie shuruti?

**SPIKA:** Swalii hilo yaani limezunguka kwa kweli, naomba ujibu kwa kifupi pia.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba maelezo haya yataendana sambamba na majibu aliyojatoa Mheshimiwa Waziri Mkuu katika moja ya swalii la leo kwamba Wizara na hili Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ameanza kulifanyia kazi. Mheshimiwa Waziri Khamis Kagasheki. Wizara inayapitia maeneo yote ambayo yamekuwa na migogoro ya jinsi hii ikiwa ni pamoja na kuhakikisha suala zima la uhakiki wa mipaka ili ijulikane wapi mipaka sahihi ipo na wapi wananchi wanapaswa kuhama.

Lakini kwa vyovyote vile kama wananchi wanalahazimika kuhama basi utaratibu muafaka unaozingatia haki zao, unaozingatia haki za mali zao, unaozingatia haki ya kupewa taarifa mapema ikiwa ni pamoja na kushirikishwa kwa uhakika kwa uongozi wa mkoa na wilaya tutahakikisha

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII]  
kwamba zinafanyika na tutahakikisha kwamba maeneo haya ambayo yanaweza yakazungumzika kwa maana ya wananchi kupewa muda fulani unaohusika kuwawezesha wahame yatakekelezwa. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Silvestry Koka.

**MHE. KHALFAN HILALY AESHI:** Mheshimiwa Spika, naitwa Mheshimiwa Khalfan Aeshi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khalfan Hilaly Aeshi, sikukuona.

**MHE. KHALFAN HILALY AESHI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Nina swali la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri, Mkoa wa Rukwa na Mkoa wa Katavi una *Game Reserve* inayoitwa Rukwa Rukati na *Rwafi Game Reserve* na kutokana na kauli mbiu yetu ya kulinda wanyama pori wetu, wale askari hawana hata gari moja la kulinda au kutembelea kulinda mipaka ile. Mheshimiwa Waziri ni lini sasa unaweza kupeleka usafiri huo na magari hayo?

**SPIKA:** Hili swali mna – *divert*, yule alisema ni unanyanyasaji na vitu vya namna hiyo, tena magari yakanyanyase zaidi. (*Makofii*)

**MHE. KHALFAN HILALY AESHI:** Mheshimiwa Spika, ili kuzuia ujangili.

**SPIKA:** Nimeshakwambia hilo siyo swali lenyewe lakini Waziri jibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali fupi la Mheshimiwa Khalfan Aeshi, kama hivi ifuatavyo.

Kwa ujumla wake kwamba Serikali inakiri kwamba tuna upungufu mkubwa nchi nzima, katika mapori yetu yote na katika Hifadhi zetu zote na vitendea kazi kwa maana ya

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII]

magari na vitendea kazi vingine muhimu. Lakini vilevile tuna upungufu mkubwa sana wa rasilimali watu na Serikali imechukua hatua za awali kama alivyotangaza mapema mwaka huu Mheshimiwa Waziri wa kuajiri askari wengi zaidi.

Lakini kinachoambatana na hicho ni kuwawezesha kibajeti na kama mnavyofahamu tunaendelea na hatua mbalimbali za operesheni mbalimbali ambazo zinahitaji siyo tu fedha lakini zinahitaji vitendea kazi kama magari na kwa kadiri ya uwezo wa Serikali tutaendelea kugawa magari na vifaa mbalimbali katika mapori yetu kwa uwiano nchi nzima. (Makofii)

Na. 152

### **Mambo Yanayoathiri Sekta ya Utalii Nchini**

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED** aliuliza:-

Sekta ya Utalii ni kichocheo kikubwa au muhimili muhimu wa maendeleo ya kiuchumi katika nchi yetu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupambana na athari zake ikiwemo mmomonyoko wa maadili?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Utalii umekuwa na matokeo chanya kiuchumi katika nchi yetu, kijamii na hata kisasa. Pamoja na faida za kiuchumi zinazotokana na mapato ya wageni wengi wanaotembelea nchi yetu Utalii pia umekuwa kichocheo kikubwa cha ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi kama vile usafirishaji, viwanda, biashara, kilimo, miundombinu na sanaa za mikono.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA MALIASILII NA UTALII]

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, suala zima la utandawazi na maendeleo ya teknolojia limechangia kwa kiasi kikubwa sana kuleta changamoto za kijamii zilizopo ikiwemo ile ya momonyoko wa maadilli.

Mheshimiwa Spika, Wizara ikitekeleza maaazimio mbalimbali yakiwepo yale Maazimio ya Shirika la Utalii Duniani yanayohusu Kanuni za Maadili ya Utalii Duniani (*The Global Code of Ethics for Tourism*).

Kanuni hizi ambazo ni muhimu kuzingatiwa katika maendeleo ya utalii, zinatambuliwa kisheria katika Sheria yetu ya Utalii Na. 29 ya mwaka 2008 na zimeweka bayana pamoja na mambo mengine kuwa wadau wa utalii na wageni wanao wajibu wa kuheshimu Maadili, Mila na Desturi katika jamii wanazokutana nazo.

Vile vile Kanuni zinapringa unyanyasaji dhidi ya jamii yoyote na hasa watoto na yejote atakayekiuka anapaswa kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imetafsiri Kanuni hizi katika lugha ya Kiswahili na kusambaza kwa wadau wa utalii. Aidha Wizara itaendelea kuhamasisha wadau wa utalii ili waendelee kutoa elimu kwa wageni wote wanaoingia nchi hii ili waheshimu Mila na Desturi za wananchi wa taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kwa upande mwingine, kupitia Miradi ya Utalii wa Utamaduni, wananchi wakiwemo vijana wameweza kufanya shughuli halali zinazowaingizia kipato ili kuondokana na umaskini wa kipato. Wananchi wanahamasishwa kote nchini waendelee kushugulika na kazi mbali mbali kama vile kazi za kuongoza Watalii, kazi za kutoa huduma mbali mbali za kitalii na zenye viwango vinavohitajika ili kujipatia kipato halali kwa shughuli za utalii. (*Makofii*)

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini bado ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, uzoefu unaonyesha kuwa nchi nydingi duniani zilizofanikiwa katika nyanja ya Utalii kwa kiasi kikubwa. Mazingira yake yamechafuka kwa kiasi kikubwa kupitia takataka nydingi za kemikali za sumu kama vile sabuni za unga (*Detergent*), chupa za *Plastic*, Vigae na mambo mengine. Kwa kuwa Tanzania tunavutia sasa utalii kwa kiasi kikubwa.

Je, tumechukua tahadhari gani ili na sisi tusije tukakumbwa na uchafuzi huo wa mazingira kama uliowakumba wenzetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili. Kwa kuwa katika jibu lako umesema kuwa mmong'onyoko wa maadili unachangiwa kwa kiasi kikubwa na Utandawazi na Maendeleo ya Teknolojia. Kuna nchi nydingi duniani ambazo zina Utandawazi na Maendeleo makubwa ya Teknolojia kama vile Dubai. Unapofungua mitandao kuangalia kama vile filamu za ngono na mambo mengine yanayohusiana na ngono unakuwa hupati.

Je, Serikali iko tayari, kuptia *TCRA* na sisi tukazuia mitandao yote ya ngono, ili mmonyoko huu wa maadili usiendelee katika nchi yetu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mhehsimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, kama hivi ifuatavyo:-

(i) Tunapenda kukiri na kuungana na Mheshimiwa Rukia Ahmed, kwamba uchafuzi wa aina yoyote wa mazingira ikiwa ni pamoja na matumizi ya mifuko iliyopigwa marufuku ya *plastic* ni jambo ambalo

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII]  
hatutalivumilia. Tunasisitiza na tumeendea kusisitiza kwamba wadau wote wa Utalii, nchini na hasa hata wale ambao wanapanda na wanapandisha Wageni katika Mlima Kilimanajaro na sehemu nyingine ambako Watalii wanakwenda, wahakikishe kwamba wanazingatia suala zima la usafi, ikiwa ni pamoja na wageni kuondoka na mifuko yao yote ambayo wameitumia na kuhakikisha kwamba Mlima Kilimajaro au sehemu nyingine nchini kama fukwe zinakuwa zimebekwa katika hali ya usafi.

(ii) Ni kweli kama anavyosema suala zima la utandawazi linawezekana kabisa kuzuiwa. Sasa hivi tuna teknolojia ambayo inaweza kwa mfano kuzuia matumizi ya aina fulani ya mtandao usiingie katika mtandao mkubwa. Hii ikiwa ni pamoja na Vituo vyetu vya Televisiuni na Serikali kwa ujumla wake inalichukua hilo na kulitazama ili tuhakikishe kwamba linatekelezeka, usalama wa maadili ya wanafamilia wetu wanakua katika hali ambayo tunategemea. (*Makof*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda tulionao ni mfupi sana na maswali bado ni mengi.

Na. 153

### **Ajira Katika Migodi ya Buzwagi na Bulyanhulu**

**MHE. AZZA HILLAL HAMAD (K.n.y. JAMES DAUDI LEMBELI** aliuliza:-

Wilaya ya Kahama imebarikiwa kuwa na maeneo mengi yenye madini ya dhahabu na mpaka sasa kuna migodi miwili mikubwa ya Buzwagi katika Jimbo la Kahama na Bulyanhulu katika Jimbo la Msalala na kila mara Serikali imekuwa ikihubiri umuhimu wa migodi hii kiuchumi na ustawi wa jamii inayoizunguka:-

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. AZZA H. HAMAD (K.n.y. JAMES LEMBELI)]

Je, Serikali inaweza kueleza Umma kwamba tangu Migodi ya Buzwagi na Bulyanhulu ianze, imetoa ajira ngapi za kudumu kwa Watanzania na wangapi kati ya hao wametoka katika vijiji vinavyozunguka migodi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimwia James Daudi Lembeli, kama hivi ifuatavyo:-

Mheshimwia Spika, Sera ya Madini ya mwaka 2009 inasisitiza kuwianisha sheria zinazohusika na ajira ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na uendelezaji wa Wataalam wa kutosha katika fani za ufundi zinazohitajika migodini.

Serikali imezitaka Kampuni za Madini ziajiri wataalam wa ndani na pia kuzitaka ziweke *program* zitakazohakikisha Watanzania wanachukua nafasi za kitaalamu zinazoshikiliwa na wageni.

Mheshimiwa Spika, jambo hili limefanyika na linatekeleza kwa umakini na hivi sasa katika Mgodi wa Buzwagi *General Manager* katika Mgodi huo kwa mara ya kwanza unaongozwa na Mtanzania Ndugu Rweyemamu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kampuni za Madini zimekuwa zikihamasimshwa kuzingatia Sera ya Madini ya mwaka 2009 na Sheria ya Madini ya mwaka 2010 ili kuhakikisha kuwa zinatoa ajira kwa Watanzania hususan wananchi walio jirani na maeneo wanayofanya kazi kwa kuwapa fursa za ajira au kuwawezesha kujajiri wenyewe kutokana na uwekezaji husika.

Uhamasishaji huu unalenga kuwajengea mazingira wananchi ili waweze kuona kuwa migodi au miradi husika ni sehemu yao. (*Makofii*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. S. J. MASELE)]

Mheshimiwa Spika, migodi ya Buzwagi na Bulyanhulu ni mionganini mwa migodi mikubwa inayotoa ajira za kudumu na za muda mfupi kwa Watanzania wa fani mbalimbali na wananchi wanaozunguka migodi hiyo. Mgodi wa Bulyanhulu ulianza uzalishaji wa dhahabu mwezi Julai, 2001 na kufikia mwaka 2012 ulikuwa na jumla ya wafanyakazi 2,716. Watanzania wakiwa 2,535 na wageni wakiwa ni 181. Kati ya Watanzania hao 2,535 wafanyakazi wanaotoka maeneo yanayozunguka mgodi, kwa maana ya Wilaya ya Kahama ni 269 sawa na asilimia kumi (10%) ya wafanyakazi wote.

Aidha, Mgodi wa Buzwagi ambaa ulianza uzalishaji mwaka 2009, ulikuwa na wafanyakazi 1,168 na kufikia mwaka 2012, Wafanyakazi 1,064 walikuwa ni Watanzania na wageni 104 na Kati ya Watanzania hao Wafanyakazi 227 wanatoka maeneo yanayozunguka mgodi huo, yaani Wilaya ya Kahama, ikiwa ni asilimia 19 ya wafanyakazi wote.

**MHE. AZZA HILLAL HAMAD:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pia nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, kwa Majibu yake mazuri. Ninaomba kama hivi ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa uzoefu unaonyesha kwamba wamiliki hawa wa Migodi ya Bulyanhulu na Buzwagi, wamekuwa wakilipia kodi zao pale llala Dar es Salaam. Hivyo kuifanya Wilaya ya Kahama na Mkoa wa Shinyanga kuonekana ikichangia kwa kiasi kidogo kwenye pato la Taifa. Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuamrisha Makampuni haya kulipia kodi katika Wilaya husika?

(ii) Ni faida gani ambazo wananchi wa Kahama na wananchi wa Mkoa wa Shinyanga za kiujumla ambazo wamezipata kutohana na kuwa na Migodi hii mikubwa katika vijiji vyao? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN**

**J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Migodi hii ilipoanza zipo sababu mbili kubwa ambazo zinapelekea kodi mbalimbali zilipwe Dar es Salaam. Kwanza uandikishwaji wa Kampuni hizi ulifanyika Dar es Salaam wakati zinaanza. Kampuni hizi ofisi zao kwa maana ya *Corporate Office* zao ziko Dar es Salaam. Sababu ya pili ni walipaji kodi wakubwa Idara ile kwa upande wa *TRA*, iko Dar es Salaam na Migodi hii yote inaangukia kwenye kundi la walipaji kodi wakubwa.

Hivyo kwa migodi ile ya kati na migodi midogo midogo ambayo inaangukia kwenye kundi la walipaji kodi wa kati yenye inalipia katika maeneo husika ambako migodi ile inafanya kazi. Lakini kwa kesi ya Buzwagi na Buli kwa sababu inaangukia kwenye *group* la walipaji kodi wakubwa, ndiyo maana malipo haya yanafanyika Dar es Salaam.

Lakini kwa suala lake kuonyesha inachangia kiasi gani katika pato la taifa tutaangalia na wenzetu wa Wizara ya Fedha kuangalia kama mahesabu yale ambayo wanayalipa kama yanaweza yakarudishwa katika Mkoa ule wa Shinyanga ili yahesabiwe katika Mkoa wa Shinyanga, tutaangalia taratibu ambazo zinaweza kutuelekeza.

(b) Mheshimiwa Spika, tukianza kuongelea faida za Migodi kwa ujumla ni mambo mengi ambayo yapo. Lakini ninaomba niziweke katika makundi manne. Kundi la kwanza ni sehemu zote ambako Migodi imeanzishwa kumekuwa na fursa nyingi za kibashara ambazo wananchi wamekuwa wakizipata.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ni kwamba migodi imesababisha ukuaji wa miji mingi ikiwemo Mji wa Kahama. Kwenye takwimu inaonyesha wakati migodi hii inaanza miaka kumi (10) iliopita, Kahama ilikuwa na watu 243,000.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. S. J. MASELE)]

Lakini sasa hivi Kahama ina watu 523,000 ni ongezeko ambalo limechangiwa kwa kiwango kikubwa na uwepo wa migodi hii katika Wilaya ya Kahama na hivi sasa tunavyoongea Wilaya ya Kahama ina Halmashauri tatu, ikiwa ni Halmashauri mbili mpya zimezaliwa baada ya ongezeko kubwa la shughuli za kijamii kuongezeka katika Wilaya ya Kahama. Ukiangalia katika maeneo mengine kama Mkoa wa Geita pia umepanda hadhi ya kuwa Mkoa kwa sababu ya shughuli za Migodi kuongeza. Bila kusahau shughuli za kibiasara na za kijamii katika Mkoa wa Geita.

Lakini sehemu nyingine ajira zimeongezeka katika Wilaya Kahama, lakini mwisho kabisa ni shughuli za kibiasara ambazo wananchi wanazifanya *ku-supply* bidhaa mbalimbali katika maeneo ya Migodi ambako Migodi ile ipo.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mrabaha uliowekwa ni wa muda mrefu. Ile asilimia tatu ya Mrabaha. Je, haujafika sasa wakati wa kuongeza huo Mrabaha ili wananchi nao waweze wakafaidika zaidi na Miradi wanayoifanya? (*Makofî*)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza kama lilitivo. Kwanza 0.3 siyo kodi peke yake ambayo inawafanya wenyeji wa pale wafaidike. Hii migodi inalipa Mrabaha ambao kwa dhahabu ni asilimia nne (4%). Inalipa (*Withholding Tax*).

Kwa hiyo, hao wanaokaa karibu na Migodi wanafaidika kutoka kwenye asilimia nne (4%) za Mrabaha. Wao wanakuwa ni sehemu ya wanaofaidika kutoka kwenye (*Withholding Tax*) ni asilimia thelathini (30%). Hapana ni *Corporate Tax* ndio asilimia thelathini (30%) na wao wanakuwa sehemu ya Watanzania wanaofaidika kutokana na (*Withholding Tax*) ya asilimia kumi (10%) mpaka asilimia kumi na tano (15%).

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA NISHATI NA MADINI]

Kwa hiyo, Ndugu zangu siyo tu kwamba Waheshimiwa Wabunge ni kwamba maeneo yale ambapo Migodi ipo wanafaidika kwanza kutokana na chungu kikuu cha Hazina, na bado wanapata 0.3. Kwa hiyo, kwa sasa inatosha. (*Makofii*)

Na. 154

### **Elimu ya Msingi Bure**

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA** aliuliza:-

Sera ya Elimu inasema kuwa Elimu ya Msingi itatolewa bure lakini watoto/wazazi wanalazimika kutoa michango mbalimbali na kwamba ada kwa shule za Sekondari za Kutwa ni Shillingi 20,000/= na Sekondari za Bweni ni Shillingi 70,000/= lakini pia hawa wa bweni wakifanikiwa wapeleke vifaa kama ndoo, jembe, dawati bila kutaja shuka, blanketi na kadhalika.

(a) Je, dhana ya kusema kuwa elimu ya msingi ni bure iko wapi?

(b) Mlolongo wa vifaa vingi vinavyotakiwa wakati wa kujunga na Sekondari, Serikali haioni kwamba ni kikwazo kwa wazazi wasio na uwezo wa kifedha?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**  
aliibuu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Elizabeth Batenga lenye sehemu (a) na (b) kama ifutavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, dhana ya Elimu ye Msingi kuwa ni bure ipo kwa kuwa Serikali bado inagharamia elimu hiyo kwa kiasi kikubwa sana. Serikali hutoa fedha za Ruzuku ya Uendeshaji wa Shule yaani (*Capitation Grant*) ya shillingi 10,000/= kwa kila Mwanfunzi wa Elimu ya Msingi na shillingi 25,000/= kwa mwanafunzi wa Elimu ya Sekondari.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI]

Aidha, Serikali huwalipa Walimu mishahara, kujenga na kuboresha miundombinu ikiwemo nyumba za walimu, madarasa, maabara na Maktaba. Pia Serikali hununua vifaa vyaa kufundishia na vya kujifunzia, vitabu pamoja na kukagua shule. Vile vile Serikali kupitia Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, Sura ya 10 inaelekeza ushirikishwaji wa wadau wengine wa elimu yaani (*Cost sharing*) katika kugharamia utoaji wa elimu wakiwemo wazazi, jamii na mashirika ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali.

(b) Mheshimiwa Spika, orodha ya vifaa vinavyotakiwa wakati wa kujiunga na shule ya Sekondari si kikwazo kwa wazazi wengi wasio na uwezo kwa sababu Serikali kupitia Halmashauri za Wilaya imekuwa na mpango wa kuwabaini wanafunzi wasio na uwezo na imetoa utaratibu mzuri wa kuwasaidia wanafunzi wa aina hiyo kwa kuwapatia mahitaji muhimu.

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti michango holela shulenii, Serikali ilitoa Waraka Na. 8 wa mwaka 2011 ulioagiza kwamba michango yote ya Maendeleo ya shule idhibitiwe kwanza na wanajamii wote, Kamati za Shule, Bodi za Shule, Bodi za Vyuo na Halmashauri husika. (*Makofii*)

Aidha, utaratibu wa kukusanya michango hiyo usiwahusise wanafunzi bali wazazi na walezi wenyewe. Hivyo, natoa wito kwa wadau mbalimbali wa elimu kuendelea kuchangia gharama katika utoaji wa elimu ili kuweza kutekeleza utoaji wa elimu bora nchini, kwani uwezo wa Serikali hautoshelezi mahitaji yote kwa wakati huu.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali madogo ya nyongeza.

Pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize kwanza, kwamba kwa kuwa, ameeleza kwamba Serikali inatoa *capitation grant* ya shilingi 10,000/= kwa mwanafunzi wa Shule ya Msingi na shilingi 25,000/= kwa mwanafunzi wa Shule ya Sekondari.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. ELIZABETH N. BATENGA]

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kulitolea mfano kwa kunitajia tu kiasi cha fedha iliyotolewa kwa shule za Mkoa wa Kagera kulingana na wanafunzi angalau kwa kutaja Wilaya moja tu ya Mkoa wa Kagera?

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kunieleza ni kwa kiwango gani *capitation grant* hiyo imepunguza mlolongo wa michango ya hovyo hovyo wanayotozwa wazazi na kulazimisha watoto wengine kurudishwa nyumbani mpaka michango hiyo ichangwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu naq Mafunzo ya Ufundsi, jibu kwa kifupi kwani muda umekwisha!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundsi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Elizabeth Batenga, kama ifuatavyo:-

Kuhusu swali lake la kwanza kwamba tutolee mfano wa Mkoa wa Kagera kumtajia fedha zilizokwenda za MMEM na MES, hapa sina takwimu lakini kwa sababu Dodoma tuna Ofisi Ndogo hivyo baada ya masaa mawili tu yaani saa saba nikitoka hapa, Bunge la jioni nitakuletea takwimu za Mkoa wa Kagera kwa sababu nitawasiliana na Afisa Elimu wa Mkoa.

Kuhusu michango mashulenii, tumetoa waraka wa mwaka 2011 namba nane kwamba michango mashulenii isitozwe na Walimu Wakuu ama Wakuu wa shule mpaka ipitiwe na Halimashauri na zile Kamati za Shule ama Bodii za Shule zipitie ndiyo ziruhusu michango mashulenii. Kwa hiyo, kama kuna michango holela huko Mheshimiwa Mbunge tupatia taarifa ili tuweze kuchukua hatua kwa wakuu wa shule hawa ambao hawafuati sheria wala kufuata waraka.

**SPIKA:** Tunakwenda Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Mchungaji Luckson N. Mwanjale, atauliza swali hilo.

**Kuboresha Viwnago vya Pensheni kwa Watumishi**

**MHE. MCHUNGAJI LUCKSON N. MWANJALE** aliuliza:-

Viwango vya pensheni kwa wastaafu hapa nchini ni vidogo sana na huathiri uhakika wa maisha ya wastaafu.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha pensheni?

(b) Je, kwa nini mtumishi asikatwe zaidi na Serikali ichangie zaidi ili viwango vya pensheni kwa wastaafu ipande?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijiini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha viwango vya pensheni kwa ajili ya kuwapunguzia wastaafu makali ya ongezeko la gharama za maisha. Ili kukabiliana na changamoto za ugumu wa maisha kwa wastaafu, Serikali inaangalia uwezekano wa kuongeza viwango vya pensheni katika mwaka wa fedha ujao wa 2014/2015. Pamoja na mambo mengine, ongezeko la viwango vya pensheni litategemea zaidi kuimarika kwa mapato ya Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, wazo la Mheshimiwa Mbunge ni zuri na linaweza kutazamwa kwa kadiri itakavyowezekana. Aidha, kuongeza mchango wa mwajiri unategemea pia uwezo wa mwajiri kimapato. Mfano, mchango wa mwajiri ukiongezeka una athari za moja kwa moja kwenye *wage bill* yaani gharama za mishahara ya Serikali au Taasisi husika.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)]

Pia, mchango zaidi wa mtumishi unaathiri kwenye pesa ambazo mtumishi analipwa kwenda nyumbani yaani *take home* baada ya makato ambayo ni msingi wa kuendesha maisha ya leo akiwa bado mtumishi.

Pamoja na wazo la kuongeza mchango wa mwajiri au mtumishi, viwango vya pensheni vinaweza kuboreshwa kwa kuangalia viashiria au vigezo vingine kama vile marekebisho ya viashiria vya umri, riba na kanuni za mafao. Aina ya mafao ya pensheni (lazima au hiari) na kuimarishe mifumo na sheria zinazotumika kuendesha na kusimamia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, maeneo haya yote niliyoyataja yanafanyiwa kazi na *SSRA* ili kuboresha viwango vya pensheni kwa wastaafu. Hata hivyo, watumishi wanashauriwa kutumia fursa zillizopo za mikopo zinazotolewa na taasisi mbalimbali za fedha kama vile *VICOBA* na *SACCOS* ili kuanzisha miradi midogomidogo ya kiuchumi na kujipatia kipato cha ziada kabla na baada ya kustaafu. Hii ni pamoja na kutumia fursa za *MKURABITA* katika kurasimisha raslimali za wananchi kwa ajili ya kuzitumia kweye kudhamini mikopo.

**MHE. MCHUNGAJI LUCKSON N. MWANJALE:**  
Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa, viwango hivi vinakuwa wakati mmoja inakuwa kiwango kilekile kwa muda mrefu.

Je, ni kwa nini sasa Serikali isiongeze au isiweke pensheni kufuatana na mshahara wa sasa uliopo kuliko kuweka kiwango ambacho aliachia kazi?

Swali la pili, kumekuwa na malalamiko mengi hasa kwa wastaafu kwamba wakati mwingine pensheni zao zinacheleweshwa. Je, Serikali inatamka nini kuhusu suala hili? Je, itakuwa tayari kurekebisha hali hiyo?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale, kama ifuatavyo:-

Kuhusiana na suala zima la kukaa muda mrefu katika kiwango kimoja cha pensheni hii yote ni katika mfumo mzima kwa kuwa viwango vya mishahara vinaendelea kuwepo lakini viwango vya pensheni ambavyo vimewekwa na vyenyewe vinategemea kipato.

Lakini kwa sasa hivi kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, *SSRA* ambalo ndiyo shirika linalosimamia masuala ya pensheni linafanya kazi mambo yote hayo ikiwa ni pamoja na kurekebisha viwango vya pensheni kufuatana na mabadiliko ya viwango vya chini vya mishahara.

Kuhusiana na ucheleweshaji katika pensheni hiyo inatokea kwa nadra kutokana na labda watu kutokutambulika vizuri kwa sababu kila baada ya miezi sita anatakiwa mtumishi au mstaafu kwenda kujihakiki. Sasa kama mtu hajajihakiki kwa muda basi wakati mwininge inatokea ucheleweshwaji.

Lakini kwa kiasi kikubwa tunajitahidi sana kupunguza ucheleweshaji na ndiyo maana tunawapa pensheni kabla ya wakati kwa maana kwamba tunatoa *advance* pensheni.

Kwa hiyo, kwa hali hii tutaendelea kuboresha na tunamwomba Mheshimiwa Mbunge na Wabunge kwamba pale ambapo kuna mtu amepata tatizo lolote basi atuone ili tuweze kujaribu kurekebisha haraka iwezekanavyo.

Na. 156

**Matukio ya Watu Kumwagiwa Tindikali**

**MHE. JADDY SIMAI JADDY (K.n.y. MHE. JAKU HASHIM AYOUB)** aliuliza:-

Miaka 49 ya Muungano wa Tanzania tumeshuhudia nchi hii kuwa mfano wa kuigwa kwa amani na umoja wa kitaifa. Hivi karibuni kumekuwa na matishio ya kutoweka kwa amani nchini.

(a) Je, ni watu gani wanaofanya vitendo vyatya kumwagia tindikali watu?

(b) Je, ni matukio mangapi yameshatokea Zanzibar na Mangapi Tanzania Bara na watu wangapi wameshakamatwa na kufikishwa Mahakamani?

(c) Je, ni hatua gani za kiutafiti zinafanywa na Serikali kubaini chanzo cha kumwagiwa tindikali watu na nyumba za Ibada kuchomwa moto?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub (BLW) lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tindikali ni moja ya vimiminika vyenye matumizi mbalimbali ya kila siku kwa binadamu ikiwemo viwandani, mashulen, vyuoni na kwenye vyombo vyatya usafiri kama vile magari na pipipiki. Mazingira haya yamefanya watu waovu kutumia tindikali kudhuru watu wengine kama ambavyo nchi yetu imeanza kushuhudia katika siku za hivi karibuni.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI]

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2008 hadi Desemba, 2013 jumla ya matukio 11 ya watu kumwagiwa tindikali yameripotiwa kutokea hapa nchini, ambapo matukio matano (5) yalitokea Tanzania Bara na sita (6) Tanzania Zanzibar. Jumla ya watu 14 wameathirika katika matukio haya. Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi wa kina wa matukio haya ambapo watuhumiwa 17 wameshakamatwa na kuhojiwa. Kati ya watuhumiwa hao watano (5) wamefikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi na kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Mwanasheria wa Serikali Divisheni ya Mashitaka (*DPP*) Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar imechukua hatua mbalimbali za kufuatilia na kudhibiti matumizi haramu ya tindikali na malighafi zake. Operesheni za pamoja za kukagua waagizaji, watunzaji na wasambazaji wa tindikali zinafanya ili kubaini mianya ya matumzi haramu ya tindikali.

Uchunguzi wa awali wa matukio ya watu kumwagiwa tindikali unaashiria vitendo vya kulipizana visasi kwa sababu mbalimbali. Uchunguzi wa kina kubaini iwapo sababu hizo zina malengo mengine zaidi ya kulipiza visasi unaendelea. Aidha, takribani matukio yote ya kuchomwa moto kwa nyumba za ibada yameshughulikiwa ambapo watuhumiwa 12 walikamatwa na kuhojiwa. Kati yao watuhumiwa watatu (3) wamefikishwa Mahakamani na upelelezi wa matukio mengine unaendelea katika hatua mbalimbali.

**MHE. JADDY SIMAI JADDY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Yaonekana kwamba kuna udhaifu katika upelelezi wa uhalifu wa kutumia tindikali. Je, kwanza Serikali inalielewa hilo? Ni hatua gani ambazo inachukua katika kudhibiti udhaifu huo?

Pili, inaonekana pia kwamba upatikanaji wa tindikali ni rahisi sana. Je, Serikali ina mkakati kudhibiti upatikanaji wa tindikali hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**  
Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya  
Mheshimiwa Jaddy, kama ifuatavyo:-

Kwanza, upelelezi una sehemu mbili, sehemu moja ni  
ya wananchi na sehemu nyingine ni ya Majeshi au Askari  
wapelelezi.

Upande wa wananchi ukiona kuna tatizo basi watoe  
taarifa ambazo Askari wangezitumia kukamilisha upelelezi.  
Inawezekana kuna udhaifu pia kwa wananchi kushirikiana  
na Jeshi katika kufanya upelelezi.

Kwa upande wa upelelezi kwenye vyombo vya dola  
ni kweli kwamba kuna mapungufu ambayo tayari tunayajua  
na tunayafanyia kazi. Hatua ambazo tunazichukua ni pamoja  
na kutoa mafunzo, vifaa, lakini pia na kubadilisha muundo  
wa idara ya upelelezi ambayo hata juzi tumeona mabadiliko  
yamefanyika.

Jambo ambalo tunaweza tukafanya ni kufanya  
tindikali isitumike vibaya, la kwanza ni kuhusu sheria. Nimewahi  
kusema hapa kwamba sheria zinazosimamia tindikali za  
Tanzania Bara na za Zanzibar ni dhaifu na tunahitaji  
kuziimarisha kwa kufanya marekebisho yanayohitajika. Lakini  
pia usimamizi wa sheria hiyo kwa maana ya wale wasimamizi  
wakemia wakuu nao wameanza kuanza kuandaa *guidelines*  
ambazo zitasaidia kujua waingizaji nchini, wasambazaji na  
watumiaji ambao ndiyo *source* ya wahalifu kuzipata.

Na. 157

**Ujenzi wa Barabara ya Lami Kolandoto hadi Kishapu**

**MHE. RICHARD M. NDASSA (K.n.y. MHE. SULEIMAN  
NCHAMBI SULEIMAN)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza mradi wa ujenzi wa Barabara  
ya Lami toka Kolandoto hadi Kishapu?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Nchambi Suleiman, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kolandonto – Kishapu ni sehemu ya barabara kuu ya Kolandonto – Lalago - Mwanhuzi – Sibiti – Njia Panda ya Oldean yenye urefu wa kilometra 337 iliyopanda hadhi kutoka barabara ya Mkoa/ Wilaya mwaka 2010. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali imepanga kuanza kuifanyia upembuzi yakinifu pamoja na usanifu wa kina (*feasibility study and detailed engineering design*) barabara nzima ya Kolandonto – Lalago – Mwanhuzi – Sibiti hadi Njia Panda ya Oldean Mkoa wa Arusha. Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri zinaendelea na ziko katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuifanyia usanifu na gharama za ujenzi kujulikana Serikali itaendelea na taratibu za kutafuta fedha ili kuanza kazi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Serikali kupitia TANROADS, inatenga fedha kila mwaka za kuifanyia matengenezo ya kawaida na ya muda maalum kwa kiwango cha changarawe ili kuimarisha barabara hiyo iweze kupitika majira yote ya mwaka wakati tunaendelea na maandalizi ya kuijenga barabara yote kwa kiwango cha lami.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Waziri amesema kwamba barabara hii inafaniyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Napenda kujua, huu upembuzi yakinifu na upembuzi wa kina utachukua muda gani kwa sababu mwuliza swali anataka kujua barabara ya Lalago, Kalandonto itapata lini lami? Huo upembuzi yakinifu utachukua muda gani?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Richard Ndassa, kama ifuatavyo.

Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Richard Ndassa, kwa kufuatilia kwa karibu kusudio la Serikali la kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Katika utaratibu wa kupata Mhandisi mshauri kitu cha kwanza ambacho Serikali huwa inafanya inamwomba Mhandisi alete kitu kinachoitwa *Expression of Interest* na katika kuonyesha hii tunafanya tathmini muda gani atafanya kazi ile na kwa gharama ipi.

Kwa hiyo, huwa kuna kushindaniwa, siwezi kusema moja kwa moja kwamba watatumia muda gani lakini tunazungumzia kilomita 337 inaweza ikachukua kat i ya mwaka mmoja mpaka mwaka mmoja na nusu katika wastani wa kazi za namna hiyo.

Na. 158

### **Usumbufo Unaojitokeza Sehemu za Mlima Kitonga**

**MHE. PROF. PETER MAHAMUDU MSOLLA** aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa kumekuwa na msongamano mkubwa sehemu ya Kitonga, Wilayani Kilolo katika barabara ya Dar es Salaam kwenda Zambia, hali inayosababishwa na ufinyu wa barabara na mara nyingine kufungwa kabisa kutokana na ajali na kubomolewa barabara kutokana na mafuriko.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kurekebisha hali hii ya usumbufo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Peter Mahamudu Msolla, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua umuhimu wa sehemu ya Mlima Kitonga katika barabara ya TANZAM. Wizara kupitia Wakala wa Baraara (*TANROADS*) tayari ilichukua hatua ya kuifanyia matengenezo ya dharura sehemu ya Kitonga kwa mwaka 2011/2012 kufuatia mvua kubwa zilizonesha mwezi Desemba, 2011 ili kuhakikisha (*lane*) zote mbili zinaendelea kutumika. Aidha, matengenezo hayo yalikuwa ni pamoja na uchoraji wa alama za barabara ili kuongeza usalama na uwekaji wa mabango yanayowatahadharisha madereva wanapopita kwenye eneo hilo lenye mlima mkali. Pia, matengenezo ya kawaida kwa barabara yanafanya kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudhi hizi zinazofanyika, Serikali bado inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa eneo hilo ili kufanya upanuzi wa kutosha kulingana na mahitaji ya eneo hili. Kazi ya usanifu na hatimaye upanuzi itahitaji fedha nyingi. Hivyo, nashauri Mheshimiwa Mbunge afanye subira wakati Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kazi hizi muhimu.

**MHE. PROF. PETER MAHAMUDU MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali napenda kuuliza maswali mawili madogo.

Mheshimiwa Spika, kwanza, Naibu Waziri ameелеza kwamba Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Je, ni lini kazi hii itaanza?

Pili, je, haingekuwa busara sasa kuanza kuangalia njia mbadala badala ya kuendelea kung'ang'ania Mlima Kitonga? Kwa mfano, kuanza barabara kutoka Mji Mdogo

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. PROF. PETER MAHAMUDU MSOLLA]

wa Ilula upitie Mlafu, Isagwa, Kising'a, Lulanzi, kidabaga, Idete, Muhanga, ipite mto Mngeta na hatimaye itokee Kilombero ambapo ni kilomita 160 tu ukilinganisha na kuzunguka njia ya kutoka Iringa, Dodoma, Morogoro ambayo ni kilomita 500?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, kwa pamoja kama ifutavyo:-

Katika kazi ya kufanya usanifu hizo *options* ambazo anazzungumza kwamba tunaangalia pia kwamba je tunaweza tukapata njia mbadala maana aidha unaweza ukasema kwamba upanue palepale au utafute njia mbadala ambayo inaweza tukalitatu tatizo lililopo kwa sasa.

Kwa kuwa barabara hii tunajua kwamba ilijengwa miaka 43 iliyopita na sasa hivi magari mengi yameongezeka. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile haiwezi kukidhi mahitaji ya sasa na ndio maana tumesema kwamba lazima tufanye suala kwamba lini tuaanza ndio maana nasema Serikali inatafuta fedha ili mapema iwezekanavyo tuweze kuanza kazi hii ya usanifu.

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, kama mnayoona muda umetukimbia sana na wachangiaji wako wengi. Waheshimiwa kwa mujibu wa Kanuni ya kutambulisha wageni nitatambulisha wale ambao wamekuja kwa ajili ya mafunzo na kadhalika, wengine sitawatambulisha.

Tuna wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 80 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, naomba wasimame walipo, *Okay*, ahsanteni sana karibu tunzeni heshima ya Chuo chetu ndio peke yake katika Bara la Afrika kilicho kizuri ahsanteni sana. Tuna wanafunzi 40 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara *CBE-Dodoma* na wenyewe wako wapi wasimame, *CBE* ahaa! Ahsante sana, nyie ndio majirani zetu someni kwa bidii pia. (*Makof!*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[SPIKA]

Tuna wanafunzi 70 kutoka Chuo Kikuu cha Mipango - Dodoma wako wapi na hawa, ahsante sana. Tunawashukuruni sana na tuna wageni watatu wametokea Arusha kwa ajili ya mafunzo, wako wapi hawa wageni. Hata hawakutaja, majina ahaa asanteni sana mmekuja kwa mafunzo. Halafu tuna wageni ambao wanaongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu, Mheshimiwa Lazaro Masey, wako wapi hawa ahsante, ahsante sana na wengine ni wake watoto wa Waheshimiwa Wabunge, tunashukuru sana karibuni sana na asante sana.

Eee! Matangazo ya kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo tarehe 19 Desemba, 2013 saa saba (7.00) mchana katika ukumbi wa Msekwa.

Halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba (7.00) mchana watakuwa na Kikao chao kwenye Ukumbi Namba 231.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (*PAC*) Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba na robo (7.15) watakuwa na Kikao Maalum na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) Wajumbe wote wahudhurie katika Ukumbi Namba 231 (Hapa kumbi zinagongana, naomba mka-*sort out* wapi mnakutana).

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Andrew John Chenge, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba na robo (7.15) watakuwa na kikao katika ukumbi wa Msekwa B. Waheshimiwa Wabunge muda ulivyo ni mfupi naomba tuendelee. Katibu, tuendelee.

## MWONGOZO WA SPIKA

**SPIKA:** Nimesema muda mfupi nawe unasema tena mwongozo! Naomba usubiri kidogo, subiri kidogo.

## HOJA ZA KAMATI

**Hoja ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu na Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini Kwamba Bunge Sasa Lipokee na Kukubali Taarifa ya Kamati hizo Pamoja na Mapendekazo na Maoni Yaliyomo Katika Taarifa Hizo**

*(Majadiliano yanaendelea)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**SPIKA:** Mheshimiwa Highness Kiwia, naomba uwe brief.

**MHE. HIGHNESS S. KIWIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naomba mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 68 (7) ukisoma pamoja na Kanuni ya 63 (1).

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 5 Desemba, 2013 wakati wa kipindi cha Maswali na Majibu Mheshimiwa Spika, katika swali langu Namba 30 Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mheshimiwa Hawa Ghasia, alipokuwa akijibu swali langu lililohusu Uchaguzi ambao haukizingatia Kanuni, Uchaguzi batili alitoa majibu ambayo hayakuwa yanaridhisha. Majibu ya uongo jambo lililopelekea Mheshimiwa Ezekia Wenje ambaye aliuliza swali hilo kwa niaba yangu siku hiyo, kwa dada yangu siku hiyo kutaka Mwongozo wako juu ya majibu hayo yasiyordhisha na ya uongo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. HIGHNESS S. KIWIA]

Mheshimiwa Spika ulimwagiza Mheshimiwa Wenje aandike barua na kuleta Ofisini kwako, jambo ambalo limekwishafanyika.

Mheshimiwa Spika, leo ni tarehe 19 Desemba, 2013 na kesho Bunge lako Tukufu linaahirishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Illemela, naomba Mwongozo wako ni lini Mheshimiwa Waziri Hawa Ghasia, atakanusha uongo huo na kutoa fursa ya Uchaguzi halali kwa Wananchi wa Manispaa ya Illemela na haki iweze kutendeka. Nakushukuru Mheshimimwa Spika, naomba Mwongozo wako. (*Makofii*)

**SPIKA:** Nimefurahi kwamba umeisemea ile barua ambayo nilimwagiza Mheshimiwa Ezekia Wenje, maana nataka kumwuliza huyo Mjumbe alikuwa sawa sawa huyu kama hakufanya nilichomwagiza. Sasa kama barua iko Ofisini kwangu tena imekuwaje tena si mimi ndio nitakayejibu. Kwa hiyo, naomba unisubiri nitajibu mimi kama ipo Ofisini kwangu.

Jana nadhani umeme ulikatika kwa hiyo tukawa tumeahirisha shughuli zetu kabla ya wakati na ukicheki orodha tuliyonayo hapa tuna wachangiaji 38 jambo ambalo haliwezekani. Kwa hiyo, tutakuwa na Wachangiaji asubuhi yote hii. Mchana tutakuwa na wachache halafu tutaomba watoa hoja waweze kujiblu.

Kwa hiyo, kwa kuanzia sasa naambiwa kwamba jana Martha Mlata alikuawa anaongea wakati umeme ulipokatika dakika saba unadai dakika saba tu, halafu atafuatiwa Mheshimiwa Zambi. Nafikiri alitajwa kwa hiyo Mheshimiwa Martha Mlata na wengine nitawataja baadaye. (*Makofii*)

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nashukuru kupata nafasi hii nimalizie dakika nilizokuwa nimeanza jana.

Mheshimiwa Spika, wakati nazungumza nilikuwa nimewapongeza *REA* kwa namna ambavyo wanaenda kwa kasi kwa ajili ya kusambaza umeme Vijijini, nikawa nimegusia kwamba tatizo kubwa ambalo wanalipata ni upungufu wa fedha ambazo tumewapangia lakini zimekuwa zikienda kwa awamu na hili tatizo Mheshimiwa Spika mimi naliangalia kwa mtazamo tofauti kidogo.

Mheshimiwa Spika, nchi yoyote hasa nchi zilizoendelea zimekuza na kujenga uchumi wake kwa wananchi wake kutoa kodi kupitia Wafanyabiashara. Lakini hapa kwetu Nchini tunategemea sana fedha ambazo zinakuwa zimekusanya na *TRA* ili ziweze kutoka tuweze kuendesha miradi yetu.

Lakini tatzikubwa ambalo nalionna hapa Mheshimiwa Spika *TRA* pamoja nakwamba wanafanya juhudii kubwa sana katika kukusanya mapato ili waweze kukidhi mahitaji ambayo sisi tunakuwa tumepitisha Bajeti hapa kuna vikwazo vikubwa ambavyo wanakutana navyo, vikwazo ambavyo wanakumbana navyo hasa pale wanapoweka mikakati na mbinu mbalimbali ya kuweza kuangalia na kukokotoa hata kile kidogo ambacho kinabakia mikononi mwa Wafanyabiashara maana Wananchi wanakuwa wamelipa kodi lakini tatizo ni kwamba risiti hawapewi. Kwa hiyo, risiti wasipopewa ile fedha inapotea bila kwenda mahali ambapo inahusika.

Hivyo nilikuwa naiomba sana Serikali iendelee kuwaelimisha Wananchi ili waone umuhimu wa kuchukua risiti, pale wanaponunua bidhaa kwa sababu ile hela wanayokuwa wameitoa wanapunjwa, maana inabaki kwa yule mfanyabiashara na wala haiingii Serikalini, maana ile hela ni haki yao itawarudia wao kwa ajili ya maendeleo yao. (Makof)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MARTHA M. MLATA]

Mheshimwa Spika, tunahitaji sana umeme vijijini ili vijana wetu, kwa mfano kule Singida mimi nahitaji sana Umeme kwa sababu tuna mashine za kukamua mafuta ya alizeti, tunategemea vijana wetu wajajiri kwenye sekta hiyo. Bila umeme hatutaweza kufanikiwa.

Tuna shule za Sekondari ambazo tunajenga maabara, tunahitaji umeme ufile kule lakini bila kufanya hivyo tunaweza tukakwama, tunaweza tukalaumiana lakini, kumbe kuna fedha zinamwagika bila sisi kujuja au tunajua lakini hatujali. Hivyo ninaiomba sana Serikali iweke mkazo kwamba Wananchi wapewe elimu ili waweze kudai risiti pale wanapokuwa na risiti ziwe zile zile halali, hasa kupitia mashine za risiti ili hela ile isiweze kupotea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa naomba nzungumzie pia kwenye upande wa Madini. Mheshimiwa Waziri naomba niongeze jambo moja tunaomba *Madini House*. Mjenge jengo la *Madini House* ili vijana wetu wapate mahali pa kuuzia madini yao ambayo wanakuwa wamechimba. Vijana wengi wamekuwa wakipunjwa na walangazi, wanunuua kwa bei ya chini, wao wanaenda kuza kwa bei kubwa hivyo tunaomba *Madini House* kwa ajili ya kuuzia vito na madini mengine yote. Vijana waweze kujuja ni wapi atakwenda kuuzia madini yake.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba pia Serikali mnapotangaza mnapotoa tamko kwamba hili eneo ni la wachimbaji wadogo ninaomba msibadilishe, mlibadilisha kule mkalama. Eneo lile mlisema hili ni la wachimbaji wadogo wadogo, eneo la Kopa lakini baadaye mkabadilisha mkatoa leseni kwa wale wenye leseni kubwa kwa kweli inaleta simanzi, inaleta masikitiko sana na inaleta migogoro isiyokuwa na lazima. Hivyo ninaomba Naibu Waziri wa Nishati na Madini, alitamka kwamba lile eneo lilitengwa kwa ajili ya Wachimbaji wadogo, Serikali ikatoa leseni kwa wachimbaji wakubwa warudishiwe wachimbaji wadogo wadopo.

Mheshimiwa Spika, hilo jambo halijafanyika hivyo ninaomba sana Serikali izingatie hilo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MARTHA M. MLATA]

Lakini nilikuwa na swali pia hivi mtu akikamatwa na madini anataka kutorosha anataka kuuza kwa njia za kinyemela ni nani wa kumpeleka mtu huyo Mahakamani ni *TMAA* au ni Kamishna wa Madini nilikuwa naomba nipatiwe jibu hilo kwa sababu hapo naona kuna watu wanakamatwa kisheria mnakosea matokeo yake yule mtu anaondoka na madini kwa sababu mmekosea sheria. Tulikuwa tunaomba tujue nani anapaswa kumshitaki mtu anayekamatwa na madini *TMAA* au ni Kamishna wa Madini?

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba tu niwapongeze Wizara ya Sayansia na Teknolojia kwa minara ambayo inaendelea. Lakini pia nipongeze juhudhi kubwa ambazo *TCRA* wanafanya kuhakikisha kwamba Televisheni zote kuanzia *TBC*, Televisheni ya Taifa na Televisheni zingine wanalipa kazi za wasanil ambazo wanazitumila, huo mtambo ambaao utakuwa unagundua na kuhakiki ni Televisheni gani ni redio gani imeweza kutumia kazi za Wasanii.

Ninawapongeza *TCRA* kwa sababu *push mobile* ambaao ndio wao wamefunga hiyo mitambo na nina hakika itaanza hivi karibuni itakuwa ni ukombozi kwa kazi zote za wasanii ambazo zinatumika. Ninaomba Mheshimiwa Spika hilo jambo wasanii wapewe taarifa ili wakae mkao wa kupokea mabilioni kutoka kwenye Televisheni zetu. Mkao wa kula kwa sababu *push mobile* tayari wameshafunga mitambo ya kuhakiki kazi zetu zinazotumika kwenye Televisheni zote, kwenye redio zote, hapo hakuna kupunjwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa ni Mheshimiwa Godfrey Zambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Gaudence Kayombo.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia taarifa za Kamati mbili ya Miundombinu pamoja na ile ya Nishati na Madini zilizowasilishwa jana. Niwapongeze wawasilishaji kwa kuwasilisha taarifa za Kamati na wakionyesha kazi walizofanya lakini pia na kushauri Serikali katika maeneo ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi. Lakini kabla sijazungumza, sijachangia taarifa hizo mbili Mheshimiwa Spika nataka niseme mambo mawili hivi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 6 Desemba, 2013 nilifiwa na mdogo wangu anayenifuata lakini nilipata watu wengi sana ambao walikuja nyumbani kwa ajili ya msiba ule na idadi ilikuwa kubwa ilituzidi na inawezekana wengine hatukuwaona au kuwashukuru kwa kazi kubwa ambayo walitusaidia kwenye msiba ule. Naomba nitumie nafasi hii niwashukuru sana wote ambao walikuja kutufarji katika msiba ule wa mdogo wangu na naomba Mungu amrehemu alipolala.

Lakini pia leo tumepata taarifa za kufiwa na Katibu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Iringa ambaye pia amewahi kufanya kazi kule Mbeya na Mbozi Ndugu Emmanuel Mteming'ombe. Ninaomba pia Mwenyezi Mungu airehemu roho yake na alale mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, Chama cha Mapinduzi (CCM) ndicho kilichounda Serikali inayotawala na juzi Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) katika kuisimamia Serikali alikuja kufanya ziara katika Mkoa wa Mbeya na Mikoa mingine.

Ninaomba nitumie nafasi hii au fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Abdulahman Omar Kinana, kwa kazi kubwa sana aliyoifanya katika ziara hiyo kwa kuisimamia Serikali vizuri sana. Rai yangu kwa Serikali ni kuomba Serikali isije ikamkatisha tamaa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. GODFREY W. ZAMBI]

Lakini kubwa zaidi imwunge mkono ili imani ya Watanzani ambayo wameanza kuionyesha kwa Chama chetu CCM isije ikapotea na ibaki kama ilivyo, hilo naliomba sana.

Lakini pia nimwombe Katibu Mkuu aendelee na ziara hizi kwa sababu ameamsha ari ya Watanzania na wana CCM ambaao imani yao ilianza kupotea. Kwa hiyo, naomba sana. (*Makofi*)

Lakini pia Mheshimiwa Spika, niseme jambo moja jana wakati yalipotolewa maneno maneno fulani alisimama Mheshimiwa David Ernest Silinde, akasema Zambi kala hela hakusafiri na kwamba.....

**SPIKA:** Mheshimiwa naomba hili uliache mnapoteza muda lakini haliwasaldii Wananchi mnapoteza muda naomba hili uliache naomba sana endelea kuchangia mambo mengine.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, naomba sana taswira inayoenda kwa Nchi na kwa Wananchi na wanani pigia simu kwamba nimeiba hela.

Hili ni jambo baya kwa sababu hela ya safari Mheshimiwa Spika, taratibu zipo kama hujasafiri ziko taratibu ambazo hela inarudishwa na ni Mbunge wa ajabu sana au Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) wa ajabu sana ambaye angeenda safari Nchini Dubai na Uingereza aache kwenda kwenye Ziara ya Katibu Mkuu wa Chama kinachotawala kwa sababu amechukua pesa ambayo inaweza ikarejeshwa na ina utaratibu wa kurejeshwa. Kwa hiyo, hili nilitaka nilitolee msimamo huo Mheshimiwa Spika. (*Makofi*)

Lakini pia, Sasa Mheshimiwa Spika nichangie, jana Ndugu David Ernest Silinde, akichangia alisema Serikali ichukue hatua kwa ajili ya kuondoa msongamano pale Tunduma na akasema Wizara ya Uchukuzi na ni bahati

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. GODFREY W. ZAMBI]

Mbaya sana Mbunge wa Jimbo hajui kinachoendelea lakini Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Mbeya, anajua kwamba msongamano wa magari Tunduma ulishaondolewa na Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi alipopita Tunduma. Alizungumza na Serikali akawaambia wafungue mpaka pale. Mpaka ulishafunguliwa, *Custom wanafanya kazi* saa 24 na leo ninavyokwambia hapa hakuna msongamano Mjini Tunduma. Lakini Mbunge wa Jimbo, hajui ni bahati mbaya sana ndio Wabunge waliopo hao.

Lakini pia nimpe taarifa hata Mbunge leo nilikuwa nazungumza na Wizara ya Maji imepeleka shilingi millioni 100 Tunduma kwa ajili ya kuhangaika na tatizo la maji pale Tunduma. Kwa hiyo, mimi kama Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, naisimamia Serikali kuona kwamba matatizo katika Mkoa wa Mbeya yanatatuliwa. Sasa kama Mbunge hajui ni bahati mbaya sana, lakini nawaomba wananchi wa Momba na Mbozi kwa ujumla kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inafanya kazi kwa nguvu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala jingine ambalo ningependa nilizungumze kweli niwapongeze sana hawa Mawaziri wawili (2) ambao tunajadili taarifa zao hapa karibu watatu (3) Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe, Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, lakini pia na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Mawaziri hawa wanafanya kazi kubwa sana. Yanaweza yakawepo matatizo ambayo siyo ya kwao moja kwa moja, lakini yanatokana na mfumo ambao inawezekana ni makusanyo tu ya pesa.

Lakini kwa maana ya kazi kufanya hawa Mawaziri, mimi nawaaminia sana, wanafanya kazi kubwa sana na Watanzania wawe na matumaini nao. Mimi nina imani watafanya kazi ikiwa watapata *support* ya Serikali na naomba Serikali pamoja na wanaoisemea Serikali. Lakini Serikali pia iwave *support* ili waweze kufanya kazi vizuri zaidi. (*Makofii*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. GODFREY W. ZAMBI]

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, atuhakikishie tu vile Vijiji ambavyo viko kwenye mpango wa *REA* wa kupatiwa umeme na kwa sababu Mkoa wa Mbeya inawezekana Mikoa mingine Wazabuni hawakupatikana. Tuliambiwa kwamba Wazabuni wameshindwa kupatikana na wametangaza upya.

Tunaomba sasa Waziri awahakikishie Wananchi wa Mkoa wa Mbeya katika maeneo yale ambayo yalikuwa Zabuni hazijapatikana, Wakandarasi hawajapatikana atuambie ni lini sasa Wazabuni wanapatikana na kazi ya kupeleka umeme katika maeneo au Vijiji vilivyoainishwa basi inaanza mara moja, naomba Waziri atueleze hilo. (*Makofi*)

Lakini kingine, ninaomba pia Profesa Sospeter Muhongo, Waziri wa Nishati na Madini, atueleze hatima ya Mradi wa Mkaa wa Mawe Kiwira. Maana jambo hilo limezungumzwa muda mwangi sana na hatuoni kama linafikia mwisho hivi karibuni. Kulikuwa watu wanafanya utafiti wa Makaa ya Mawe kule Magamba Mbozi, kule walishasimama. Tunaomba pia tujue maendeleo ni nini. Maana yake na hili wananchi wamekuwa wanauliza sana, maendeleo yake ni nini tukijua itatusaidia wananchi kuwa pia na imani.

Kwa kaka yangu Dkt. Harrison Mwakyembe - Waziri, ninaomba tu nishauri suala la *TAZARA*. Suala la *TAZARA* limekuwa ni jambo ambalo limezungumzwa zaidi ya miaka kumi, lakini hakuna ufumbuzi unaoendelea. Wafanyakazi wa *TAZARA* waliopo na wale waliostaafu, wanafanya kazi katika mazingira makubwa sana. Juzi Katibu Mkuu wa Chama Chama cha Mapinduzi (CCM), Ndugu Abdulrahman Kinana, alipita *TAZARA* akaongea na wafanyakazi, wamemlalamikia sana. Kwamba ni kama vile Serikali imetelekeza Wafanyakazi wa *TAZARA*.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. GODFREY W. ZAMBI]

Kama tatizo ni Serikali ya Zambia, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, tunaweza hata sisi tukaendesha TAZARA kwa upande wetu na bado tukapata faida, kuliko hali iliyopo sasa hivi. Kama kikwazo ni TAZARA Sheria ya TAZARA ya mwaka 1995, kwa nini isije hapa Bungeni tukaibadilisha? Maana yake mfumo wa kwamba lazima Wazambia ndiyo wawe wanaendesha Reli ya TAZARA, lakini uendeshaji wao unakuwa wa mashaka; hatuwezi kwenda na wala hatuwezi kuwatendea haki Wafanyakazi wa TAZARA ambao kwa muda mwingu sana wamekuwa wanateseka. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri Mwakyembe, awaonee huruma Wafanyakazi wa TAZARA. (*Makofi*)

Hivi ninavyozungumza, Mheshimiwa Spika, na tumekuwa tunazungumza hapa Bungeni. Wafanyakazi ambao wamestaafu zaidi ya miaka mitano iliyopita, mpaka leo hawajalipwa haki zao. Hivi unategemea wafanyakazi ambao wametumia miaka 20, miaka 30; wanastaafu hawajapata haki zao miaka zaidi ya mitano, wanaishije! Wakati mwagine tuwaonee huruma watu ambao wametumika kwa uaminifu, na tutafute njia ambazo tunaweza tukawakomboa na wakaweza kuishi vizuri na wakajiona kama waliweza kutumikia nchi yao vizuri. Niombe sana jambo hilo lifanyike

Lakini Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa nizungumze ni kwa upande wa Barabara. Niombe sana. Najua Mheshimiwa Magufuli hayupo, lakini Naibu Waziri nimewona yupo. Liko suala la Barabara ambazo Mheshimiwa Rais aliziahidi katika Mkoa wa Mbeya. Naomba nizitaje chache. Kuna barabara ambayo inatoka Kikusya kule Kyela kwenda Matema, bado imepewa sehemu ndogo sana ya kutengenezwa.

Ni barabara ya kilometra 39. Tumepewa lami karibu kilometra 20. Tunaomba barabara hii inapofika mwaka 2015 basi walau iwe imetengenezwa kwa kiwango cha kuridhisha na wananchi waendelee kuwa na imani na Serikali yao.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. GODFREY W. ZAMBI]

Pili, iko barabara ya kutoka Itumba kule lleje mpaka Isongole. Barabara hii pia ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Tunaomba na yenyewe hatua zichukuliwe ili ianze kujengwa. Kuna barabara ya kutoka Rujewa kule Mbarali kwenda Mafinga, na yenyewe pia ipatiwe ufumbuzi ili iendelee kujengwa.

Kuna barabara ile ya Mbeya – Chunya ambayo inaendelea kujengwa, lakini tunaomba pia na yenyewe Serikali iipe umuhimu sana. Kuna barabara ya kutoka pale Mlowa kwenda Kamsamba, tunaomba barabara hii tuipe kipaumbele kwa sababu barabara hii inabeba nusu ya uchumi wa Wilaya ya Mbozi; lakini pia nusu ya uchumi wa Wilaya ya Mombasa. Sasa ikibaki katika hali iliyopo leo, bado hatuwezi kufanya shughuli za Kiuchumi zikaenda vizuri katika maeneo hayo.

Ninaomba sana sana Serikali itilie mkazo katika maeneo hayo ili tuwatendee haki Watanzania nao waweze kufanya shughuli zao za kiuchumi vizuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nimwombe basi kaka yangu Dkt. Harrison Mwakyembe mwisho kabisa, kuna baadhi ya watumishi au kuna fedha ambazo ziko chini yako, watumishi hao wamekuwa wana-act kwa muda mrefu sana. Mimi nafahamu kwamba mpaka sasa hivi *SUMATRA* Mkurugenzi alishastaafu, lakini anafanya kazi kwa muda. tunaomba basi mpate mtu mwininge ambaye anaweza akafanya kazi pale ili wafanye kazi kwa imani ili kusukuma maendeleo.

Lakini pia *TAA* najua Suleiman amekuwa anakaimu kwa muda mrefu sana. Hivi kuna tatizo lipi? Kama mtu anafanya kazi vizuri, mpeni ili afanye kazi kwa imani zaidi. Maana ukikaimu wakati mwininge unakosa nguvu ya kufanya maamuzi fulani, kwa sababu unasema nikifanya hivi watani ondoa. Kwa hiyo, tunaomba muwathhibitish. Tulisema kama mnaona mtu hafai, basi mtafuteni mtu mwininge anayefaa.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. GODFREY W. ZAMBI]

Lakini mimi nina imani Ndugu Suleiman nimefanya kazi naye Mamlaka ya Hali ya Hewa, tulikuwa tunakutana na najua ni mtu ambaye ana uwezo. Kama ana uwezo, mpeni ili aweze kufanya kazi vizuri zaidi hasa asimamie vizuri ujenzi wa Viwanja vya Ndege, kazi ambayo inaendelea sana kote nchini. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo, Mheshimiwa Spika, nasema naunga mkono hoja zote, na naomba sasa nikae. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Asante sana. Mimi sijakuita, una nini!

**MHE. DAVID ERNEST SILINDE:** Mwongozo wako Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo, haya. Mwongozo kuhusu nini?

**MHE. DAVID ERNEST SILINDE:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kwa mzungumzaji wa mwisho aliyejewa amepita.

Mheshimiwa Spika, mzungumzaji wa mwisho ni Mbunge na Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Mbeya, vile vile ni Kamishna wa Bunge. Anafahamu taratibu zote za safari. Kuchukua fedha bila kwenda safari ni makosa. Alichukua fedha za PAC hakwenda safari. Alichukua fedha za michezoni, akaenda siku moja akageuza. Jumla ya shilingi milioni 13.

Sasa Mheshimiwa Spika, mtu anapotumia Bunge lako kujitetea kwa kukiuka taratibu kama ni sehemu ya Bunge inaruhusiwa? Lakini jambo la pili, nimpe tu taarifa zote alizozisema, nazifahamu kama Mbunge wa Jimbo. Asante sana. Naomba mwongozo wako kama amefuata taratibu hizo.

**SPIKA:** Wabunge nimesema, kama mlichukua hela bila ya safari, mnarudisha. Si basi. Wote *without exception*. Wote na ninawajua na ninayafanya kazi yake. Kwa hiyo, wote waliochukua fedha bila safari wanarudisha Ndio utaratibu wa Serikali. Nashangaa nyie mnaendelea kuzungumza haya maneno. Wote ambao hawakwenda safari watarudisha na ndivyo inavyotakiwa kuwa. Kwa hiyo, wote wajue hilo. Siyo kwamba siwafahamu, wote watarudisha *without exception*. Nyie mnaposema sema maneno shauri yenu, lakini wote watarudisha. (*Makofî*)

Nilimtaja Mheshimiwa Gaudence Kayombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Mwambu, atafuatiwa na Mheshimiwa Rebeca Mngodo. (*Makofî*)

**MHE. GAUDENCE CASSIAN KAYOMBO:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nafasi ya kuongelea hoja hizi mbili. Lakini pia nawapongeza Wenyeviti kwa *presentation* zao nzuri sana, na Mawaziri wa Wizara husika katika maeneo haya pia wanafanya kazi vizuri sana. (*Makofî*)

Lakini pia ningependa kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba Bunge letu linapoanza kila siku linaanza kwa sala. Katika ile sala tunaomba hekima, Mwenyezi Mungu atujalie. Kwa hiyo, tunapochangia ni vizuri kukumbuka kwamba tumekwishamwomba Mungu.

Tatu, nataka kuongelea Miradi ya REA (Umeme Vijijini). Ningependa kuiomba Serikali kwa kushirikiana na *TANESCO*, ifanye *mapping*. Kwa sababu katika Miradi hii ukiangalia, kuna Wilaya ambazo zimeendelea mbele sana katika mambo ya umeme; kuna zingine ziko katikati, zingine ndiyo kwanza hawana umeme kabisa. Sasa tunapajaribu kuzisaidia zote kwa mara moja bila kuweka mkazo zaidi kwa zile ambazo zimechelewa, utakuta kwamba sehemu moja ya nchi inapata maendeleo ya umeme na sehemu nyingine ya nchi haipati maendeleo ya Umeme. (*Makofî*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. GAUDENCE CASSIAN KAYOMBO]

Nashukuru sana Wizara imewahusisha Wabunge katika jambo hili. Ningependa pia iwahusishe hasa Mameneja wa *TANESCO* katika Wilaya ili waweze kuainisha maeneo yote vizuri zaidi, ili umeme huo uwe kwa faida ya kila Mtanzania. Mimi napenda kuongelea hasa katika Jimbo la Mbanga ambalo hakuna kijiji chenye umeme mpaka sasa, hata kule Nyasa ni hivyo hivyo. Mimi nafikiri Serikali ingeweza kuweka mkazo zaidi katika maeneo haya ili tuweze kwenda kwa pamoja vizuri sana. Lakini kazi mnayofanya Waziri pamoja na *REA* wenyewe, ni kazi nzuri sana. Nawapongeza na naiomba Serikali iendelee kutoa fedha. (*Makofi*)

Jambo la pili Mheshimiwa Spika, ni Umeme. Umeme tunaopata sasa hivi ni ghali sana, senti 45 za dola. Lakini kulikuwa na nafasi kubwa sana ya kupata umeme kwa bei nafuu. Tunayo Makaa ya Mawe pale Ngaka. Lakini tumekuwa tukijadiliana na wawekezaji. Wawekezaji wale wanajadiliana na Serikali, wanajadiliana na *TANESCO* kwa miaka mitatu. Tanesco wanatumia shilingi bilioni 4.5 kila siku. Fedha hizi zingeweza kununua mitambo ya kufua umeme ule wa Makaa ya Mawe na tungepata umeme wa beinafuu zaidi. (*Makofi*)

Sasa nilitaka hawa Mawaziri wanisaidie, kwa nini tumejihusisha katika majadiliano hayo kwa muda mrefu, badala ya kutatua tatizo letu la umeme. Kwa sababu Makaa ya Mawe ni yetu wenyewe, yako chini ya *NDC*. Kwa nini tumeendelea kujadiliana na hawa wawekezaji kwa muda mrefu? Mimi sielewi.

Kama *NDC* ni sehemu ya uwekezaji ule, kwa hiyo ni Serikali yenyewe. Kwa nini tumechukua muda mrefu namna hii, na tumeingia ghamama ya muda mrefu kwa miaka mitatu kila siku shilingi bilioni 4.5 zinaondoka. Mimi nilifikiri pengine *TANESCO* wangeweza kuwezesha, wakajenga huu mtambo ili mambo yetu yaweze kuwa mazuri zaidi na kuondokana kabisa na mambo ya *capacity charges*; kuliko kuacha kila kitu kwenye *Private Sector* hasa ukizingatia kwamba wenzetu wa *NDC* wako kwenye mradi huo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. GAUDENCE CASSIAN KAYOMBO]

Lakini niliaka pia Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini anisaidie, pengine Waziri wa Viwanda na Biashara. Kwa nini huu mgodi bado uko chini ya *NDC*, kwa sababu tumeunda Shirika la *STAMICO* linaloshughulikia habari za madini. Kwa nini shughuli za mgodi kama huu zisingehamishiwa tu *STAMICO* ili hiyo *reporting system* iwe ya haraka na urasimu unaondoka, kuliko sasa *NDC* aongee kwanza na Waziri wake wa Viwanda na Biashara, atoke hapo aende akaongee na Waziri wa Nishati na Madini; wakati tuna-specialize institution ambayo inashughulikia kama vile ambavyo tunayo *TPDC*. Ningependekeza kwamba wangefikiria kuoanisha majukumu ya *NDC* na majukumu ya *STAMICO* ili kuweza kurahisisha maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumwomba Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, katika mpango wa maendeleo wa miaka mitano, iko Reli ya Mtwara - Mbinga - *Mbamba Bay*. Ningependa tu kwa nafasi hii atueleze ujenzi wake umefikia wapi, kwa sababu wananchi hao wanasubiri kwa hamu sana reli hiyo na hasa ukizingatia kwamba chakula cha nchi hii kinatoka katika Mikoa hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu wachimbaji wadogo wadogo. Hapa sina maneno mengi, lakini ningependa sana kumwalika Waziri au Naibu wake anayeshughulika na mambo ya Madini na yule anayeshughulika na mambo ya umeme, wangefika katika Wilaya za Mbinga na Nyasa, kuja kujionea wenyewe adha inayopatikana kule juu ya wachimbaji wadogo wadogo. Pia matatizo ya umeme. Nafikiri mkifika mtaweza ku-appreciate matatizo ambayo tunayo. Tunawasubiri kwa hamu, hata kama mtafika Krismas yenyewe, tutawapokea.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuishukuru sana Serikali. Nilipokuwa naingia hapa Bungeni, tulikuwa na Mheshimiwa Komba tulikuwa tunaimba sana habari ya barabara ya kutoka Songea kwenda Mbinga mpaka Nyasa. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu na kuishukuru Serikali kwamba barabara kutoka Songea mpaka Mbinga imekamilika. Tunayo mabasi sasa yanatoka Dar es Salaam

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. GAUDENCE CASSIAN KAYOMBO]

mpaka Mbinga, unafika siku hiyo hiyo hatulali tena njani. Tunawashukuruni sana sana sana. Lakini ziko ahadi za ile barabara ya kutoka pale Mbinga kwenda *Mbamba Bay*, Mbinga kwenda Lituhi na kuna ahadi pia ya Waziri Mkuu na hasa ukizingatia usafirishaji wa Makaa ya Mawe, ya barabara ya kutoka pale Kitai kwenda Lwanda na kwenda Lituhi. Lakini pia nikumbushe ahadi za Mheshimiwa Rais za barabara ya kutoka pale Mbinga Mjini kwenda Litembo Hospitali, hospitali kubwa sana, karibu kila Mbunge hapa anaifahamu.

Mheshimiwa Spika ulikuwa Mkuu wa Mkoa kule, unaifahamu vizuri. Ile barabara tena inatia aibu. Pale Mbinga mjini, Halmashauri imeweka barabara zake zote lami, isipokuwa barabara hii ya Serikali Kuu haijawekewa lami. Kwa hiyo, nilikuwa nakumbushia ahadi za Mheshimiwa Rais. Pamoja na barabara ya kutoka pale Nyoni kwenda Mkoa. Hizi ni ahadi za Mheshimiwa Rais, ningependa kuzikumbusha ziweze kutekelezwa. (*Makofii*)

Baada ya kusema haya Mheshimiwa Spika, mimi ya kwangu yamekwisha. Nawashukuruni sana, nawapongeza Mawaziri endeleeni na kazi. Wananchi wanaitambua, na nawaombeenii kwa Mwenyezi Mungu muendelee na Baraka zake na nguvu za kutekeleza, kuwasaidia wananchi wa Tanzania. (*Makofii*)

Ahsante sana Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Salome Mwambu akifuatiwa na Mheshimiwa Rebecca Mngodo.

**MHE. SALOME DAUDI MWAMBU:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nami nafasi hii ili niweze kuchangia. Kwanza kabisa nazipongeza Kamati zote kwa kazi yao waliyofanya, halafu vile vile napongeza kwa mafunzo yao waliyokwenda kupata nje. Ninachokiomba Serikali, basi Serikali izingatie yale waliyoyaleta wayaingize katika kuyafanya kazi. Wayaweke katika mkakati. Siyo watu wanakwenda kujifunza, wanatumia fedha nydingi za Serikali;

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. SALOME DAUDI MWAMBU]

Iakini wanaporudi hakuna kinachoendelea. Kwa hiyo, naiomba Serikali izingatie. Mambo mengi mazuri sana yameletwa, mfano katika Ujenzi wa Barabara, wenzetu kule Malaysia walifanikiwa vipi. Naomba Serikali izingatie hilo.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye masuala ya barabara (ujenzi), kwa kweli napongeza. Na namshukuru Mheshimiwa Rais kwa ahadi yake aliyolahidi kutujengea Daraja la *CDT*, hilo Daraja sasa hivi linajengwa na makandarasi wako barabarani wanatengeneza. Ila isipokuwa kitu kimoja, wakati wanatengeneza barabara kilomita 25 kufika kule Daraja la *CDT*, walikata mazao ya watu wakiahidi (Kata ya Mpambala) kuwa watawalipa. Mpaka sasa hivi wananchi wa Kata ya Mpambala hawajalipa. Sasa hivi wameingia katika hali ya kuhangaika na njaa. Naomba Serikali itekeleze, kwa sababu kama waliharibu wao wenyewe; wakakata mazao kabla hayajakomaa wakisema kuwa watayalipa hayo mazao; na tayari utafiti ulishafanyika. Lakini nashangaa sijui kitu gani kinakwamisha. Wananchi wana shida, hawana chakula. Naomba hilo litekelezwe. Suala lingine Mheshimiwa Spika, ni kuhusu barabara ya kutoka Mwanangili, Kitumbili, Lelembwe, Yulansoni hadi Msingi. Hii barabara imekuwa kero kwa muda mrefu, haipitiki. Na sasa hivi mvua zikeanza, maana yake mawasiliano yameshakatika. Hawawezi kwenda popote kupata huduma, wanashindwa kufuata pembejeo. Barabara haipitiki. Akina mama kwenda kujifungua kwenye Kituo cha Afya Kinyangiri, wanashindwa kuvuka. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba kama hii barabara na fedha zilitengwa milioni 350; hii fedha kwa nini hailetwi ili kazi ya kuitengeneza hiyo barabara ianz? Ninaomba basi kwamba hizi fedha zikija, zielekezwe moja kwa moja kwenye Wilaya na Mkalama. Tulikuwa ni Wilaya moja na Wilaya ya Iramba Magharibi, Iakini mafungu mengi bado wanashahau wanaelekeza Magharibi. Ukitimba wa kutoa hiyo hela kutoka Magharibi kuileta Mashariki, unakuwa ni mkubwa mno. Naomba moja kwa moja Wilaya zote zinazohusika, hela zielekezwe Wilaya ya Mkalama, akaunti zote tumeshafungua. (*Makof!*)

[MHE. SALOME DAUDI MWAMBU]

Vile vile kuna barabara ndogo tu ya kilometa tatu aliyoahidi Mheshimiwa Rais, ya kuunganisha kutoka Iguguno Shamba mpaka Iguguno Mjini, iunganishwe ili magari yaweze kuingia. Lakini mpaka sasa hivi hiyo barabara bado na kwenye bajeti ipo ilisomwa. Mheshimiwa Magufuli alinuka akaahidi kuwa tunajenga mara moja. Hiyo barabara mpaka sasa, jamani hata kilometa tatu zichukue miaka mingapi? Ninaomba Wizara ya Ujenzi ilifuatilie hili kwa karibu. Kwa sababu mapato mengi tunashindwa kuyathibiti pale Iguguno. Iguguno mpaka sasa hivi mpango mkakati wetu, tunataka kujenga Soko la Kimataita hapo Iguguno. Halafu vile vile, na Stendi Kubwa. Usiku watu wanashushiwa mbali, wanashindwa kwenda kwenye majumba yao. Mimi naomba tu hilo suala, kale kabarabara kajengwe jamani. Vitu vingine Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, ni vya kutoa amri tu. Sivyo vya kuja mpaka huku Bungeni tulumbane, tuongee kitu ambacho kilikuwa kidogo sana. Kilometa tatu ni ndogo sana kwa Serikali ya Tanzania. Mimi naomba hiyo barabara ijengwe.

Mheshimiwa Spika, vile vile nilikuwa naomba hawa ndugu zangu Wahazabe watengenezewa miundombinu ili waweze kufikika. Barabara ni mbaya, hazifikiki kwa haraka. Sasa hivi wana matatizo ya kuingiliwa na wafugaji na wakulima. Wanakwenda wanawaingilia huko wanafyeka pori lao, hao watu naomba tuwape hifadhi. Mpaka sasa hivi wamebaki takriban watu 1,000 tu, tutawapoteza. Ni unyama gani amba Tanzania pamoja na kuwa tunasifika kwa kuwa ni nchi ya amani, sasa hawa watu mazingira yao yanazidi kuwa magumu. Na hatuwezi kuwalazimisha wakalingana na mtu wa sasa hivi. Kwa sababu wenyewe bado wako kwenye mabadiliko. Waliosoma historia nafikiria wanaelewa "*Evolution of Man*". Bado hawajafikia mtu wa sasa hivi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika, huwezi ukamlazimisha hata umpige umwambie kula ugali, hali. Yeye anategemea pori ndio maisha yake. Miundombinu wajengewe hawa watu waweze kufikiwa kwa haraka. Pale palipo na matatizo Serikali iweze kuwasaidia. Ninaomba sana hilo litekelezwe. Hawa watu wameingia kwenye Wizara mbili tatu. Wizara ya Ardhi, wapo. Mazingira, wapo. Yaani nikiwa na maana kuwa Wizara ya Utalii wapo huko nako. (*Makof!*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. SALOME DAUDI MWAMBU]

Mazingira wapo, yaani nikiwa na maana Wizara ya Utalii wapo huko nako, Miundombinu nako wapo. Sasa wasaidiwe na Wizara ipi? Ni tamko tu la Serikali hawa watu wawekewe mipaka yao ya pori lao wasiingiliwe. Wale waliowaingilia nawaomba waondoke kwa amani tu kwa usalama, waache kukata miti kwa sababu uhai wa hawa watu unategemea Pori la Mwangeza na Mwidibu. Wanategemea chakula, wanategemea dawa na mizizi, tuhakikishe makabila mengine hayawaingilii.

Mheshimiwa Spika, suala lingine napenda niongelee kuhusu mawasiliano. Jamani Wilaya yetu ina Kata 14 lakini minara ipo mitatu tu na hiyo minara bahati mbaya ilijengwa katika mstari mmoja. Kwa hiyo, mawasiliano ya simu kusambaa yaende katika Jimbo zima au Kata zote hamna, hayafikiki. Ninaomba Wizara ya Mawasiliano iangalie sana pale Makao Makuu tuwekewe mnara, mawasiliano ya simu ni shida sana, kazi zinafanyika kwa matatizo. Nakumbuka Mheshimiwa Rais, alipokuwa anaomba kura, alipokuja kwetu Mkalama aliahidi akasema, hizi Wilaya mpya atahakikisha nazo zinapata huduma zote kama Wilaya za zamani, hospitali zitajengwa za wilaya, vituo vya polisi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hata sasa hivi Wananchi wanajitolea kujenga vituo vya polisi, wafanyakazi hamna. Ninaomba hilo nalo pamoja na kuwa siyo la Wizara, lakini nitamke lisikike Wizara inayohusika ishughulikie, vituo vimejengwa, tumejenga vituo vya polisi wafanyakazi hamna na ujambazi unaendelea. Kila siku mnasikia magari yanatekwa ule Ukanda wa Iguguno, Iguguno, Sekenke hapo katikati. Tunaomba tuongezewe wafanyakazi na magari ya doria tupewe. Wilaya haina magari, hakuna magari ya doria halafu vilevile hata Mkuu wa Wilaya hana gari ambalo anaweza akakimbia haraka akaangalia mambo ya wilaya yake yanaendaje. Tunaomba tupewe magari mapya, tusiambiwe tugawiwe, mtu ukimwombwa akugawie nguo atakupa iliyoisha. Kwa hiyo, ule utaratibu tuliopewa wilaya ya zamani tugawiwe jamani hatukupata

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. SALOME DAUDI MWAMBU]

magari bali tulipewa mabovu na hela ya kutengeneza hatuna. Naomba hilo Serikali iliangalie kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nilisema namwita Mheshimiwa Rebecca Mgodo. Naomba aanze Mheshimiwa Naomi Kaihula, atafuata Mheshimiwa Rebecca Mgodo! Nina sababu ndogo tu.

**MHE. NAOMI A. M. KAIHULA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa nafasi hii na afya kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuchangia katika hoja hizi.

Kweli hizi hoja ni muhimu na zinaingillana na hoja nydingi; kwa mfano, ukizungumzia miundombinu unazungumzia chakula, unazungumzia afya, unazungumzia elimu, unazungumzia vitu vingi sana, unazungumzia biashara na viwanda. Kwa hiyo, hata unapokwenda kulizungumza kwa dakika kumi muda hautoshi. Pia unapozungumzia masuala kama haya yamezungumziva sana, yamefanyiwa mikakati sana na mpaka hapa inabidi tupongeze kwa juhudini zilizofanywa na Wizara zote zilizohusika. Wizara hasa ya Miundombinu imefanya kazi nzuri nydingi. Pia Nishati wamejitahidi lakini bado. Mimi napenda kusema, tunapozungumza kama Wabunge tunazungumza kwa ajili ya kujenga, tunazungumza kwa ajili ya kuona Wananchi wanaendelea kuwa na matumaini. Unajua nchi inapokosa matumaini ndipo ambapo inatokea fujo na vita. (*Makofii*)

Moja ambalo ningesema kubwa, watu tumezungumza mikakati, tumezungumza maombi, bajeti zilizopita tumezikumbusha zipo hapa lakini tatizo hasa la msingi huwenda tunalo hatutaki kilitaja. Tusipofanya hivyo, bila shaka tunarudi kulekule kutokuweza kutatua. Kwa hili ningependa nizungumzie moja; kwa mfano, suala la miundombinu. Masuala ya barabara na reli jinsi yanavyohusiana. Mtanisamehe sana, sisi tupo upande wa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. NAOMI A. M. KAIHULA]

Watchdog na kwa kweli kazi ya Watchdog ni kuwa jasiri na kuwa muwazi kueleza kitu ambacho ni kweli na kisicho kweli kijipambanue.

Suala la miundombinu, barabara na reli linatatiza lakini halipaswi kututatiza. Kwa sababu gani? Inasemekana kwamba, reli hazitiliwi mkazo ama haziwekewi mafungu kwa sababu tu zitapokonya biashara za watu binafsi ambao wamewekeza katika malori makubwa ya mafuta, ya mizigo, ndani ya nchi na nje ya nchi. Sasa hili suala inawezekana likawa ni kweli kwa sababu hata ikiwa vipi kama reli haitatengamaa, barabara hata zikitengewa fedha nyingi zikatengenezwa kila wakati hazitafanya kazi.

Swali langu lilikuwa hivi; kwa uzuri tu kusudi tuweze kutatua; tunaomba Wizara husika na wahusika wote wanaohusiana na waweze kutupa orodha ya wafanyabiasha wa malori makubwa na mafuta na mizigo yote ambayo inapita katika hizi barabara kuu ambazo zinanyima reli kutotengenezwa. Kwa sababu ni wazi kwamba, kama reli zingekuwa zimetengenezwa, bila shaka hii mizigo ambayo inaharibu barabara, uzito, sijui huko kila wakati mizani malori yameungana, tabu tupu, hii isingekuwepo. Wengine wamekwishasema kabisa kwamba, pia pengine tusingeona kwamba na wenzeni sisi ni waharibifu tunachelewesha mizigo nje na bandari zetu zikakosa kazi.

Kwa hiyo, naomba watakapokuja hapa au muda mwingine watuambie hizo biashara zipo katika mikono ipi kusudi tunapokaa chini kutatua tuweze kujua tunashughulika na akina nani hapa? Hili suala ni la wazi, *transparency*. Watu wengine wanashindwa hata kufanya kazi mka sema ooh, Waziri huyu au sijui Mkurugenzi huyu ni dhaifu kumbe siyo dhaifu, tatizo ni wale ambao wanafanya makusudi ili zile reli zisitengenezeke wao waendeleze biashara ubinafsi. Lazima tujue kama Wabunge kwamba ni mojawapo ya ugonjwa ambao umo katika nchi yetu sasa hivi wa ubinafsi ambao unafanya Wananchi wasipate huduma zao. Hilo moja.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. NAOMI A. M. KAIHULAJ

La pili linanitatiza kidogo, tumezungumzia suala la nishati. Kweli nishati ni muhimu mno kupita kiasi kama nilivyosema, inaunganika tena inarudi kule kule kwenye reli, kwenye mizigo, kwenye kilimo, yaani kuna *linkages*. Kitu gani kinafanya nishati isiihuke? Kinachonitatiza zaidi, niki-*declare interest*, mimi nipo kwenye Kamati ya Uchumi, Biashara na Viwanda na nimekuwa kwenye Kamati hiyo kwa mihula miwili sasa. Kuna wakati tulizungumzia kwamba, makaa ya mawe kule Ngaka na Kiwira, yakipewa kipaumbele bila shaka yataleta umeme ambaao ni rahisi. Badala ya senti 45 tutakatwa pengine senti 7 au 5, lakini kitu cha ajabu sana ambacho kinanitatiza sielewi kwa nini, mimi nawaheshimu sana kwa mfano Mheshimiwa Profesa Muhongo na Kamati zake ni wataalamu lakini pia naamini wana hofu ya Mungu. Naamini kabisa.

Kitu gani kinafanya mkaa wa mawe ambaao upo tayari hata mikakati hata watu wamejitolea kwa mfano Waswidi kujenga sijui nini visifanyike watu wang'ang'anie tu umeme wa maji ambaao umekwishatuangusha, umetuletea matatizo mpaka leo? Suala hili nauliza watuambie kwa nini hawataki kuendeleza vyanzo vingine vya nishati?

Upopo wa bure Mungu aliotupa jamani toka tumeanza hii Tanzania na akili yenu yote wataalamu wetu kwa nini hamtaki kuweka vipaumbele hivi na mkafanya juhudhi mkaweza kutupatia nishati inayotokana na upopo. Sijui kuna nishati zinazotokana na jua, ipo. Kwa nini vinashindikana wakati Mungu ametupa jua kubwa, jingi kila wakati, lakini kwa nini inashindikana toka tulipoanza? Kwa nini tunang'ang'ania kufanya vitu kwa matukio? Tukikatiwa umeme kama jana tulivyoadhirika, wewe *just imagine* hata ukizungumzia juu ya ulinzi, hili ni mojawapo ya tatizo kubwa la ulinzi; kukatikiwa umeme Viongozi wa nchi wako ndani ya Bunge wanakatikiwa umeme? Aibu! Ni tatizo kubwa kama hamjui kwamba ni tatizo la ulinzi, linaweza likafanya hata watu wakajuzulu. Lakini niwaambie hapa Tanzania kuna vitu ambavyo tunavichanganya tafadhali

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. NAOMI A. M. KAIHULA]

na hivi vitu ni lazima tukae chini tumwombe Mungu atusaidie.

Lazima tuelewe vitu. Watu wakisema *democracy*, *democracy* siyo hii tunayofanya ya mtu kufanya kitu akakaa akachukua akapita tu. *Democracy* ikipita kiwango inakuwa ni fujo, *too much democracy results to anarchy*. Sasa tunakoelekea humu Tanzania nawaambia wala siyo demokrasia ni fujo. Sasa hili suala ni lazima tuliweke katika *right prospective* tuangalie. Fujo zinatendeka hapa ndiyo maana mambo hayaendelei. Watu wakashindwa kutekeleza ni lazima wawajibike. Korea wamefanya hivyo, mjomba wa Rais kafanya vituko akaishia kunyongwa.

Narudi kwenye suala langu la mwisho kwa kuwa muda umeisha. Lazima watu wawajibike, ni lazima Bunge hilli lione jinsi gani vitu vile tunavyovisema vinatekelezwa. Kwa mfano, watu wanaofilisi wamekaa hapa wanafanya viwanda haviendi, wanafanya Miradi yote ya Serikali haiendi, wanapaswa kufilisiwa ni matajiri wa kutupwa. Kwa mfano, hawa wa magari walete majina yao tuangalie, tutamwomba Mungu sana na kufunga na tutaomba nchi nzima itusaidie kufunga tuweze kutoa maamuzi ambayo ni sahihi. Tusikae kulalamika, unaanzia Mawaziri wanalamika, Wakurugenzi wanalamika, Wananchi wanalamika, kila mtu analalamika; kwa nini iwe hivyo jamani? Mtu ukipewa kitu kufanya, kifanye kwa moyo wako wote na kwa kumwogopa Mungu na watu waliokutuma hii kazi. Kama huwezi kwa uaminifu na utakuwa na heshima zaidi jiuzulu, waambie mimi jamani sitaweza.

Mheshimiwa Spika, mwisho, namalizia Mheshimiwa Muhongo, gesi iliyotoka tunataka na sisi tushiriki Wananchi Wazalendo. Nami nasema ukweli tushiriki Wazalendo. Ahsante sana nashukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Rebecca Mgodo, atafuatiwa na Mheshimiwa Yussuf Hussein.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Kwanza, ni-*declare interest* kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu.

Ningependa kusema kwamba, ujenzi wowote wa maendeleo ya Taifa lolote ambalo liko huru hautakiwi kuwa na *break*. Ninasema hivyo kwa sababu inaelekea katika kulijenga Taifa letu kuna mahali tuliweka *break* na hii nimeiona baada ya ziara za Kamati ambapo napenda nimshukuru sana Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, alitupa nafasi tukaweza kuitembelea Tanzania kuona miundombinu ya Bandari. Tulifika Itege Mbeya, tukaenda Tanga na kwa kweli tulipofika katika maeneo yote yale, kwangu mimi kama Mtanzania ninaipenda nchi yangu, nilisikitika kuona utafikiri tuko nyuma miaka sijui mingapi, labda ni 20 au 30.

Nikakumbuka kuna wakati ulimwenguni kulikuwa na m dororo wa uchumi ambapo na Tanzania na sisi tulikuwa mojawapo. Pengine pale tulipoacha kuijenga nchi kwa kutumia mipango ya maendeleo iliyokuwa ikipangwa kwa miaka mitano mitano badala yake tukaanza kuwa na *projects* nyangi nyangi; nadhani tulipoanza kuwa na *projects* ndogondogo nyangi ndipo wajanja walipoinuka na kuanza kuiibia nchi na kuitafuna. Hivi sasa tumefikia mahali ambapo nikitazama kwa maeneo ambayo tulifika, Tanga ilivyo nzuri lakini hakuna *u-busy*, siyo *busy*, Bandari haipo *busy*. Ukifika Mwanza haipo *busy*, hakuna shughuli zinazofanyika za haraka haraka za kulijenga Taifa. Nikaona tunahitaji kufanya uwekezaji mkubwa ambao unaweza kuleta mageuzi ya maendeleo katika nchi hii.

Nalishukuru Bunge lako, Mheshimiwa Spika na wewe mwenyewe, ulitupa nafasi ya kwenda Malaysia kujifunza, tukaona jinsi ambavyo kile kisiwa kidogo kimepiga maendeleo makubwa. Nikaona maadam Tanzania tumeamua kujifunza kutoka Malaysia, ni vizuri basi tukaangalia wao wanawezaje ku-*monitor* Miradi yao, *projects* kubwa kubwa tuliambiwa kwamba zipo mikononi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. REBECCA M. MNGODO]

mwa sekta binafsi. Kwa historia fupi ambapo tumekuwa na uwekezaji wa madini ambayo hayakumnufaisha mtu ye yote ndiyo maana nasema tunahitaji tujifunze kutoka Malaysia, wao wanaisimamiae Miradi yao, wanazidi kuiamini sekta binafsi na ambapo sekta binafsi imekuwa kama ndiyo *engine* ya kuleta mageuzi ya maendeleo katika nchi yao.

Najua hata hii *BRN* tumeiga kutoka kwao, tume-*copy* kutoka kwao, siyo vibaya lakini tuone wao wanaita *Big Results Now* kutokana na nini? Kuna nini nyuma yake hata wakaona ni *Big Results Now?* Pengine sisi tunaweza tukalichukua hilo neno *Big Results Now; Big Results Now from what?* Kuna nini nyuma mbona sisi ni umaskini mtupu, ni tabu tupu halafu tunaona ni *Big Result*. Hata hivyo, tujifunze wao wamevezaje kusimamia Miradi yao hata hawajaweza kuilihi na wanaweza kuwa na maendeleo makubwa.

Mheshimiwa Spika, nikiangalia upande wa reli, katika Taifa lolote najua watu wengi hapa mmesafiri na mmeona treni ndiyo ambayo inaweza ikaleta urahisi wa kusafirisha mizigo na ikaleta urahisi wa kubeba watu wengi zaidi. Hivyo, ninaamini kabisa kwamba ni vyema tukaenda kwa *standard gauge* kwa sababu *standard gauge* ipo *faster* kuliko *one meter gauge*. Siku za nyuma nilikuwa nikimsikia Mheshimiwa Waziri akisema, *one meter gauge, standard gauge*, nilikuwa simwelewi. Nashukuru baada ya kwenda Malaysia *at least* nimeelewa kwamba ni kweli *standard gauge* ni *the best* kwa sababu ni *faster* na inaweza kubeba uzito mkubwa zaidi wa mizigo. Hata nchi jirani ya Kenya ambayo imepata Uhuru baada yetu, wao tayari wana mradi ambao ultakiwa uishe Novemba wa Reli ya *Standard Gauge* kutoka Mombasa – Nairobi – Kampala – Kigali mpaka Juba. Lazima na sisi tuangalie jinsi ya kuingia katika uwekezaji mkubwa ambao tutaweza kuleta mageuzi makubwa katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, najua pengine itaonekana ni vigumu lakini tukumbuke tulipopata Uhuru, wakati Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, alipoanza *from zero*;

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. REBECCA M. MNGODO]

ni kweli alichukua mikopo lakini je, ile mikopo ililipwa? Je, ile mikopo tulisamehewa? Lazima na sisi tuwe na *vision* tuangalie, kuliko kuendelea kujenga nchi yetu kwa kuikarabati karabati, tuangalie jinsi pia ya kujenga upya kabisa, kwa kuanza upya kama nilivyoona Malaysia, karibu asilimia 90 ya *projects* zao kubwa kubwa, miundombinu, wanafanya ujenzi mpya na siyo kukarabati zaidi. Ninapoangalia Miradi mingi inakuwa kama tunakarabati zaidi kuliko kuanza upya kabisa.

Ninapenda niongelee pia kuhusu *TAZARA*, mamlaka ambayo nimeifahamu kwa muda mrefu kwa jinsi ambavyo inatia huzuni. Tunaambiwa Mkurugenzi Mtendaji lazima atoke Zambia. Mimi sielewi maana yake nini? Kwa nini lazima atoke Zambia; ni kwamba, Watanzania hawana uwezo au hakuna Mtanzania anayeweza kuiendesha *TAZARA*? Ningependa sana Sheria Namba 4 ya Mwaka 1975 iangaliwe upya, kwa sababu ninaamini kwamba, kuna Watanzania wanaoweza kuiendesha *TAZARA* na ikafanya vizuri. Kwa hiyo, tusiendelee kufanya *second class citizen*, sisi tusiwe tu *second class* hata Watanzania wanaweza kabisa kuiongoza *TAZARA*.

Ningependa Wabunge wa Tanzania na Wabunge wa Zambia ikiwezekana wakae pamoja kutafuta namna ya kuweza kuibadilisha Sheria ile ili reli ambayo naamini ni ya *standard gauge*, iweze kufanya kazi na iweze kuzalisha kama ilivyokuwa ikizalisha siku za nyuma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa pia kwamba, Mkurugenzi Mtendaji huyu kutoka Zambia ambaye ninaamini pia Kiswahili hajui, kwa hiyo, hana mawasiliano yoyote na Watanzania, kwa muda mrefu hivi sasa amekuwa akiishi hotelini na katika hoteli amekuwa akilipiwa *bill* zake kwa dola huku akiwa na nyumba ambayo angeweza kuhamia.

Mheshimiwa Spika, ningependa mamlaka husika na nina uhakika Mheshimiwa Waziri ana mamlaka katika mikono yake na anaweza kabisa kuhakikisha Mkurugenzi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. REBECCA M. MNGODOJ]

Mtendaji huyu akahamia katika nyumba yake ambayo amepewa na Shirika ili kuwapunguzia mzigoto Watanzania, wavuja jasho ambao wanalipa kodi na ili tuweze kusonga mbele. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie kidogo kuhusu Mbeya, kwa sababu nilikuwa kule Mbeya nikashuka katika *Airport* ya Songwe ambayo kwa kweli nilipokuwa nashuka pale nilijisikia kama ninashuka Johannesburg, tofauti labda ni majengo, lakini ile mandhari ya pale ni nzuri. Tatizo tulilolipata wakati wa kwenda mjini ni msongamano mkubwa wa magari, badala ya kufika kwa dakika 15 MJINI Mbeya, tulitumia karibu saa mbili. Kwa hiyo, ningeomba sana kwa upande wa barabara ambazo zinakwenda *Airport* zitengenezwe, ziboreshwani, labda mkakati ufanyike jinsi ya kuweza kufungua barabara nyingine ya kufika MJINI watu waweze kufika MJINI kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo Dar es Salaam pia, kuna barabara ya kutoka Mbezi mwisho inayopita Marambamawili inaweza ikaboreshwa, kuliko watu wanaotoka katika maeneo haya kwenda Morogoro wanalahazimika kupita Ubungo ndipo waende *Airport*. Barabara ile ninaamini kabisa inaweza ikatengenezwa vizuri na hata kuwekwa lami ikiwezekana. Tanzania ni nchi tajiri. Nilikuwa nasoma kwenye gazeti jana, Taarifa za *IFM*, Tanzania imekwishakufikia zaidi ya asilimia 25 kwa kuwa na utajiri wa rasilimali zao wenywewe. Kwa hiyo, ninaamini tuna utajiri tunaweza tukafanya hivyo. Ila tunaomba wale wanaohusika wakaliangalie hilo pia.

Mheshimiwa Spika, nadhani kwa hayo machache niishie hapo. Ahsante. (*Makofij*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mgodo, ahsante sana. Sasa nilisema namwita Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, atafuatiwa na Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, halafu atafuatiwa Mheshimiwa Modestus Kilufi na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla atafuatiwa. Wale waliochangia zaidi ya mara moja hawapati nafasi.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Awali ya yote, nami nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kupata fursa ya kuchangia hoja zilizopo mbele yetu mchana huu wa leo. Napenda kusema kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi macho na masikio ya Watanzania wote walio ndani ya nchi na nje ya nchi na hata wasiokuwa Watanzania, wanaelekeza macho yao sasa hivi Tanzania katika suala zima hili la gesi na mafuta. Kwa hiyo, napenda niishauri Serikali kwamba, tunapaswa kuwa makini zaidi, siyo Watanzania wote wanaopenda neema hii, kwa sababu shoka halikati bila ya mti, lakini pia hata na walio nje ya nchi siyo wote wanaopendelea neema hii kuwepo kwa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hapa nataka niishauri Serikali mambo matatu katika hili. La kwanza, Serikali iwe inatoa taarifa sahihi na kwa wakati kuhusiana na masuala ya haya ili wale wenyewe nia mbaya ya kupotosha hili basi wasipate nafasi ya kuwapotosha Watanzania juu ya suala hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mfano hivi karibuni kulikuwa na kongamano pale Chuo Kikuu, watu walitumia nafasi ile kujieleza na walitumia vyombo vyao vya habari kuelezea namna gani suala la gesi na mafuta ambavyo Watanzania hawashirikishwi. Mungu bariki Waziri husika alikuwepo pale, akatoa majibu, akatoa maelezo ambayo kila Mtanzania aliyekuwepo pale na kila ambaye hakuwepo pale lakini alisikiliza, alitosheka na maelezo hayo. Kama hakuwepo hali ingekuwaje? Upotoshaji ungekuwa mkubwa na ile dhana ambayo ilielezwa pale ingekubalika mionganoni mwa watu na tungefikia pabaya. (*Makof*)

Kwa hiyo, ninaishauri Serikali iwe inatoa taarifa sahihi na kwa wakati ili upotoshaji ukitokea basi uendane na ile taarifa, iwe mtu anakusudia sasa kufanya ubaya, lakini taarifa imetolewa kwa wakati. Hilo la kwanza.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN]

Mheshimiwa Spika, la pili, ninachotaka kukizungumza hapa ni suala zima la kuchanganya siasa na utaalami. Mimi ninaiomba Serikali iwaachie wataalam wafanye kazi zao za kitaalam na wanasiasa wafuatilie wataalam wao wanafanya nini kulingana na sera, kanuni na utaratibu ambaao umepangwa kwenye nchi. Wasiwaingilie wataalam, kama tunataka maendeleo kweli, tuwape nafasi wataalam wetu wafanye kazi zao kitaalam halafu kama kuna hoja basi tuwahoji kama wanasiasa, lakini tusiwaingilie katika utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Spika, hapa nina maana gani? Nina maana tuwape nafasi sasa Mawaziri wetu au watu tulio wapa dhamana waweze kuajiri watu kulingana na utaalami wao. Siyo leo Mheshimiwa Waziri labda anahitaji watu 20, wanaomba kazi pale, wanahitaji kuajiri watu 20, waenda pale na vimemo vya wanasiasa nisaidle huyu hata utaalami hana. Haya mambo tuachenii kama tunataka kwenda mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika hili, hivi karibuni binafsi nilitembelea Oman, wale njia zao tatu kuu za uchumi, dhahabu ambayo tunayo hapa, mafuta na gesi, lakini huwezi kukuta mgeni katika sekta hizo. Ni watu ambaao wanafanya kazi wenyewe, ni wazalendo wenyewe, hata ukimkuta mgeni basi huyo ni mtaalam *expert* ameajiriwa pale kwa kazi maalum, lakini wanaofanya kazi katika sekta hizo ni wazalendo wenyewe. Sisi tumetembea huko katika Kamati hukuti Mtanzania katika lile bomba la gesi linalotandikwa pale, hata ukimkuta ni kibarua tu, beba hili, fanya hili, lakini hatuna watu pale.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kuwa watumwa katika nchi yetu endapo hatutawaruhusu wataalam hawa wakaweka watu ambaao ni Watanzania Wazalendo wakawenza kurithi ile kazi ambayo tunataka wao waje waifanye. Kwa hiyo, naomba sana siasa na utaalami vitenganishwe kama tunataka maendeleo ya haraka sasa.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN]

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ni la uzalendo. Lazima wale ambao tunawapa dhamana hii wawe wazalendo kweli kweli na kama si wazalendo basi tujaribu kuwapa elimu ya uzalendo, waelewe kwamba wao ndiyo wenye jukumu la kuipeleka Tanzania hapo tunapotaka. Kwa hiyo, uzalendo unahitajika zaidi katika masuala haya ili tuweze kufikia maendeleo kamili.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, ambalo nataka kulizungumzia ni suala la watu ambao wamepewa vibali vya uchimbaji katika nchi yetu, lakini hadi leo hawajafanya kazi maeneo waliyopewa. Kuna wazungumzaji wenzangu wamepita hapa wakasema kuna watu wanachukua maeneo halafu wanakuwa madalali. Sasa mimi naiomba Serikali na kwa sababu kuna Waziri makini na Wasaidizi wake katika Wizara hizi ambazo tunachangia hapa, wale wote ambao wamepewa vibali na hawajayatumia maeneo yale kama inavyotakiwa, wanyang'anywe mara moja maeneo yale yarudi Serikalini na Serikali iwave wale ambao wana uwezo wa kuyafanya kazi wafanye kazi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ni lazima hapa tuwe makini kweli, hatuwezi kufikia maendeleo ya kweli kama tutakuwa na wawekezaji uchwara. Wawekezaji vishoka, wawe wa ndani ya nchi, wawe wa nje ya nchi. *We should to have right investors in Tanzania now.* Kama hatuna *right investors*, kama ni Wazalendo, kama ni Watanzania, kama ni *foreigners*, lakini wawe ni *right investors*, hapo tutafikia maendeleo ya kweli. Tukipata watu wababaishaji, anakuja anachukua maeneo yetu, anakaa pale anasubiri mtu aje aingie ubia, hatuwezi kufikia Waheshimiwa Wabunge. (*Makof!*)

Kwa hiyo, ni lazima tuwe na *right investors* na tuweke mkakati sasa vipi tutawenza kuwapata *right investors*. Hata hawa wanaotoka nje wanakuja hapa wajanja wajanja tu. Mimi nilikuwa katika sekta ya uwekezaji, ninafahamu haya; kuna mwekezaji mmoja alikuja anataka eneo kabla hajapewa lile eneo basi alilipiga picha kwa njia ya *aerial photograph*, akachukua ile picha akaenda

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN]

kuomba mkopo katika Benki za kwao kwamba tayari amepata eneo la kuwekeza. Sasa wawekezaji wa namna hiyo ni lazima tuwe makini sana na ndiyo pale niliposema kwamba, wataalam wetu tuwaachie wafanye kazi zao kitaalam. Kwa sababu wao ndiyo wataweza kufanya upembuzi wa kujua kwamba huyu ni *right investor* na huyu siyo *right investor*.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni kengele ya kwanza, niende katika suala la tatu na la mwisho. Nije katika masuala ya miundombinu, uchukuzi, nimalizie hapo. Limezungumzwa suala la ndege katika hotuba yao hapa ukurasa wa 16 na 17. Kama miezi miwili iliyopita nilikuwa naangalia kipindi cha je, tutafika, nikakuta kuna wawekezaji kutoka nje wamekuja ni wa Oman nadhani, wanaelezea kwamba wataleta ndege nane kufufua Shirika letu la Ndege.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme hapa, wawekezaji wakitaka kufufua Shirika la Ndege, Shirika la Reli, Shirika gani, kama Watanzania hatujakuwa tayari, hatujaweka uzalendo mbele, kwa kumtegemea labda Waziri tu awe *active* au Naibu Waziri au Katibu Mkuu, lakini waliobaki hawapo hivyo, hatutaweza kufikia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, jamani hatujifunzi kutoka kwa wenzenetu! Wakati inavunjika iliyokuwa *East African Community*, karibu tulikuwa na ndege sawa kati ya Kenya na Tanzania, leo Kenya wako wapi, sisi za kwetu kwa nini zimekufa? Leo tunatumia *blue band* ya Kenya wakati sisi tuna Kiwanda cha *Tanbond* pale Mwanza kiko wapi? Leo tunaagiza plastiki kutoka Kenya, tulikuwa na Amboni pale hata ndoo ya maji ikidondoka kutoka kichwani na maji haivunjiki nini? Vyote hivi vimekufa! Tutasema Mawaziri hawa, tutawalaumu, anaweza akawa Waziri sawa, lakini Waziri ni Waziri tu walio chini yake je? Jamani tunashindwa nini hapa kuchukua hatua. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, napata shida kweli, tunashindwa kuchukua hatua kwa sababu gani au kuna mkono wa mtu

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN]

hana? Sasa leo wenzetu, juzi tu tunasema Rwanda wamekwenda mbele kuliko Tanzania, aah kwa nini wamefika huko? Ni kwa sababu wamekuwa *committed*, Viongozi wamekuwa *committed*, Watendaji wamekuwa *committed*. Sisi hatuko hivyo. Sasa naomba tusioneane haya kama tunafika mahali tunataka kwenda mbele, basi tusioneane haya ni lazima tuwe wakweli, ni lazima tufanye kazi kwa uhakika kabisa tukiwa na maana anayetaka, asiyetaka Waheshimiwa tumwachen. Kuna methali inasema kama tunataka kwenda mbali twende pamoja, kama unataka kwenda haraka nenda peke yako.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nafikiri nisingoje kengele ya mwisho, niishie hapo. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Nashukuru sana kwa kuniokolea muda. Sasa nitamwita Mheshimiwa Yussuf Khamis, atafuatia Mheshimiwa Kilufi, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, Mheshimiwa Mariam Kisangi na Mheshimiwa Chiku Abwao.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa ruhusa yako. Kwanza, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama katika Bunge hili. Pia nachukua fursa hii kuwapongeza Wenyeviti wote ambao wamewasilisha Ripoti zao.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, kwa hiyo, kwa kiasi kikubwa nitatazama upande huo.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tu tulipata fursa ya kutembelea migodi iliyopo Kanda ya Ziwa; Geita Gold Mine, Africa Barrick Gold Mine, Bulyankhulu, Buzwagi, North Mara, Nyamongo na Kijiji cha Wachimbaji Wadogo Wadogo Buziba.

Mheshimiwa Spika, nitaanza hapa Buziba. Ukiingia Buziba hakuna tofauti kubwa na Kariakoo kutohana na harakati zilizopo pale na watu walivyo wengi mahali pale.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS]

Kwa tathmini tulioifanya ambayo siyo rasmi hapapungui karibu pana mashimo 1000 mpaka 700 hivi ya wachimbaji wadogo wadogo. Wachimbaji wadogo wadogo hao wanachimba katika hali duni sana, wanatumia teknolojia ya zamani sana. Ukiiangalia teknolojia wanayoitumia inaharibu mazingira kwa kiasi kikubwa, kwa sababu wanatumia miti, katika kila shimo ambalo wanachimbia pembe nne basi inabidi wapange miti katika pembe zote nne zile ili wapate kwenda kwa usalama kujihakikishia maisha yao, kwa kuepusha maporomoko ndani ya mashimo yale.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali iwaangalie sana wachimbaji wadogo wadogo, wanatumia nguvu nydingi, lakini pia wanachimba madini katika hali ya kuhatarisha maisha yao. Hilo la kwanza. Wapatiwe zana za kisasa, wapatiwe elimu ambayo itakuwa inakwenda sawa na kazi wanayoifanya.

Jambo lingine katika hapa mkusanyiko uliopo pale umekusanya watu wa aina mbili, wanawake na wanaume. Vijana wanatumia nguvu nydingi katika kufanya kazi ile na bila shaka wanachoka na wakichoka nadhani mapumziko yanahitajika. Kwa hiyo, naomba *TACA/DS* wawepo, watu wa ushauri wawepo, kuwaongoza vijana wale ili nguvu kazi zile tuzilinde zisipotee. Si hivyo tu, pia mahali pale kwa mkusanyiko wa watu walivyo, kuna watu wengi, kukitokea ugonjwa wa mlipuko ni hatari sana. Naiomba Serikali mahali pale paangaliwe vizuri, iwepo *dispensary*, wawepo wataalam wa afya ili kuwaongoza vijana wale wafanye kazi zao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, nikiondoka hapo sasa hivi nataka kwenda North Mara, Nyamongo. Upo Mgodi ule, lakini ukiingia katika Mgodi ule ile hali utakayoiona yale magari yamezungushiwa waya wa chuma kama susu hivi, viro vyote ubavuni kwa dereva kote zimejengewa nyaya za gari. Tulitaka kujua nini maana ya waya zile, tukaambiwa panakuwa na mashambulizi mengi, Wananchi ukitoka na

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS]

magari yale wanayapiga mawe vibaya vibaya, kwa hiyo, ile imekuwa kama kinga ya kujihifadhi wale.

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo ambalo linatokana na dhana ambayo Wananchi wanahisi wawekezaji wanachukua mali zao pasipo wao kunufaika. Hili ndiyo tatizo, wawekezaji wanavuna dhahabu, wanavuna almasi, wanavuna kila kilichopo pale, lakini Wananchi wa sehemu zile hawafaidiki na matunda yale. Sasa ndiyo wanaingia katika ugomvi, chuki, husuda na kila kitu.

Kuliondoa hili inabidi pia Serikali yetu iwe makini kabisa kwa sababu wawekezaji wengine wanapeleka fedha zile za levy ambazo zinakwenda katika Halmashauri, lakini labda kuna wajanja fulani au mchwa wanakula fedha hizi zinakuwa hazifanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, fikira yangu napendekeza zile fedha wale wawekezaji wawakusanye Viongozi wa Halmashauri na Viongozi wa Vijiji, wachague Mradi upi ambao wanataka kufanyiwa, ikiwa barabara, ikiwa shule au jambo lingine muhimu lolote ambalo linakwaza katika kijiji kile. Wale wawekezaji watafute wakandarasi wautengeneze Mradi wakimaliza waukabidhi, wakishaukabidhi Wananchi watakuwa kidogo wamenufaika na malalamiko yataondoka. Vinginevyo, fedha zile zikipelekwa Halmashauri, juzi tu katika kuchangia TAMISEMI, Halmashauri zimelaumiwa sana kwa sababu zimegeuka mchwa zinakula kila kitu. Kwa hiyo, itakuwa hilo ni tatizo. Pia hapa hapa katika Mradi huu wa Nyamongo, nawapongeza kwa dhati kabisa, kwa sababu pale pale tulishuhudia shule mbili za sekondari ambazo ni nzuri tena za kutosha, nyumba za walimu, vyoo, wamejenga vizuri tu na wamejenga dispensari ambayo ina hadhi ya Kiwilaya. Kwa hiyo, wamepiga hatua nzuri na mimi hapana budi niwapongeze kwa hili.

Mheshimiwa Spika, nikiondoka hapo sasa nakuja Wakala wa Kusambaza Umeme Vijiji (REA). REA inafanya kazi nzuri, lakini nayo inakwazwa na matatizo yanayozikwaza

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS]

Taasisi zingine za Serikali. Tatizo ni kwamba, bajeti wanayotengewa ni ndogo na bajeti hiyo hiyo ndogo wanayotengewa haifiki kwa wakati. Tumewapa jukumu kubwa la kueneza umeme vijiji ambao ni muhimu kwa maendeleo ya Wananchi wetu walioko vijiji, lakini sasa wanashindwa kufanya kazi zao kutokana na ufinyu wa bajeti. Waathirika wakubwa wa kupandishiwa mafuta ya taa ni Wananchi wa Vijiji.

Mheshimiwa Spika, tulipitisha katika Bunge hili hili katika kuondoa uchakachuaji wa mafuta kwamba, bei ya mafuta ya taa na bei ya dizeli ziwekwe karibu sawa sawa ili kuondoa uchakachuaji. Wananchi watumiaji wengi wa mafuta wanatoka vijiji, tangu yalipokuwa hayajapandishwa bei na yalipopandishwa bei ni wale wale ambaao ni wanaathirika. Tulitegemea labda huu umeme uwafikie haraka labda waondokane na tatizo hili, lakini si kweli kama tutaweza kupeleka umeme vijiji haraka haraka na hili tatizo kuondoka. Kwa hiyo, bado Wananchi wa vijiji wanabeba mzigo mkubwa wa kununua mafuta ya taa kwa mahitaji ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge hili hili ilipitishwa kwamba, faida itakayopatikana katika mafuta ya taa na dizeli ile tofauti pale basi kunapatikana faida karibu shilingi bilioni sita. Shilingi bilioni tatu wapewe REA kwa ajili ya kueneza na kusambaza umeme; sasa sijui hili limefika wapi? Wapewe REA fedha ya kutosha wawaondolee Wananchi matatizo ya umeme vijiji. Keshokutwa kutakuwa na mpira wa Kombe la Dunia, utakuta vijana wengi lazima wafuate katika miji mikubwa kwenda kuangalia mpira sasa inakuwa kidogo si nzuri. Wengine watakaokwenda hawarudi tena vijiji, kwa hiyo, Taifa linapata hasara nguvu kazi inapotea.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, bomba lililoenda Mtwara, Kamati ilipata bahati ya kulitembelea na kwa kweli tumeona kazi nzuri inayofanywa na inayokwenda kwa *speed*; na kama tutakwenda vizuri basi mradi ule ndiyo unaweza ukaleta Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now*). Kwa kuwa Mradi ule ni mkubwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS]*

na endelevu, bado tatizo lilelile wananolizungumza kila Mbunge anayesimama hapa kwamba, hatukuwatayarisha Vijana wetu wa Kitanzania kushiriki katika mradi ule. Tumepitia katika nyanja zote kutoka mwanzo mpaka Madimba Mtwara Vijijini, utawakuta wafanyakazi wote ni Wachina. Sasa nilikuwa nafikiria *step* ya kwanza kuanza Mradi ule basi Watanzania wawepo pale na wao wachukue ujuzi ule ili walismamie vizuri bomba lile. Hata hivyo, hatujachelewa, nawapongeza sana *TPDC* kwa kusimamia Mradi ule, lakini tutafute Vijana wa Tanzania wapewe elimu ili wasimamie Mradi ule.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nasema ahsante sana. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana kwa kuokoa muda. Namwita Mheshimiwa Kilufi, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla ajandae na Mariam Kisangi atafuatia.

**MHE. MODESTUS D. KILIFI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wanambarali, naomba nitumie nafasi hii kwa masikitiko makubwa, kupokea taarifa ya kifo cha ndugu yetu, kijana wetu mpendwa, Ndugu Emmanuel Mteming'ombe, ambaye alikuwa Katibu wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Iringa na sasa ametuacha. Kwa kweli kwa Wanambarali ni pigo kubwa, alikuwa kiongozi mashuhuri ambaye tulintumainia na kumtegemea sana. Nawapa pole sana ndugu zangu wote Wanambarali, Mwenyezi Mungu, aiweke roho yake mahali pema peponi; amina.

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu na mimi naomba nichukue nafasi hii kuchangia hoja za Kamati hizi mbili ambazo kwa kumwogopa Mwenyezi Mungu, naomba niwashukuru sana hawa ndugu zangu Mawaziri wanaongoza Wizara hizi ngumu, nyeti na jitihada nydingi ambazo wanazifanya, asiyeziona basi bahati mbaya, kwa sababu watu tuna tofautiana mitazamo. Nichukue nafasi kuwapongeza kwa dhati kabisa kwa kazi nzuri mnayoifanya. Ndugu zangu, naelewa ugumu mnaoupata, lakini nataka niwahakikishie, ongezeni jitihada na bidii kunusuru maisha

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MODESTUS D. KILUFI]

ya Watananzania, watumikieni kwa bidii zote, kama binadamu hawataelewa Mwenyezi Mungu atawalipeni.

Mheshimiwa Spika, nikianza na suala la mawasiliano kwa maana ya miundombinu hasa barabara. Barabara ni kiungo muhimu sana kwa maendeleo na hasa kuunganisha Wilaya na Wilaya, vijiji na vijiji kwa maana ya kusafirisha mazao kutoka eneo moja kwenda eneo lingine. Nimekuwa nikisema hapa Bungeni mara nydingi kuhusiana na suala la barabara ya kutoka Igawa kwenda Ubaruku kupitia Rujewa, ni barabara ambayo ni muhimu hata Taifa linajua. Tunasafirisha sana mchele na mchele mwangi unaoliwa Dar es Salaam na maeneo mbalimbali unatoka Mbarali. Cha kushangaza, kama ni sifa sielewi tuwe na sifa za namna gani, kule tuna viwanda zaidi ya kumi na mitambo mikubwa ya kukoboa mpunga, lakini barabara ndiyo hiyo.

Mheshimiwa Spika, sasa ndugu yangu Mheshimiwa Magufuli, Waziri wa Ujenzi, namshukuru ameniahidi, lakini namwomba Mwenyezi Mungu ajalie kwa kweli hii barabara ikamilike, tena tumeomba kwa kiwango cha lami nyepesi, suala ambalo limekuwa gumu sana. Tuna Miradi mingi ya Kilimo, tuna mashamba makubwa, uwekezaji, tuna mazao mengi, lakini barabara zake hazifai hasa wakati wa mvua huwa hazipitiki kabisa. Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi aliniahidi kwamba, angetembelea kule Mbarali na Wanambarali wanakusubiri uje ili pengine ujionee mwenyewe hali halisi ilivyo. Kwa hiyo, tunatumaini Mheshimiwa Magufuli alivyoniahidi kwamba hii barabara atahakikisha inafika Ubaruku, nadhani atafanya hivyo hatawahadaa Wananchi wa Mbarali.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ahadi vilevile ya barabara. Najua barabara katika nchi hii kama tutafanikiwa kuunganisha Wilaya na Wilaya, Mkoa na Mkoa, tutaweza kusafirisha mazao kutoka vijiji kupeleka mahali ambapo soko linaweza likapatikana kwa urahisi. Tuna barabara vilevile ya kutoka Rujewa kwenda Madibira kwenda Mafinga, nilimwomba ndugu yangu Waziri wa Kilimo aje ajionee hali halisi na aliniahidi kwamba atakuja, aone

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[MHE. MODESTUS D. KILUF]*

hali halisi ya uzalishaji wa zao la mpunga lililopo kule. Japo tumekosa soko najua siku moja litapatikana, aone hali halisi na hii barabara imekuwa ikiahidiwa muda mrefu toka wakati wa Mheshimiwa Mjengwa, sasa sijaelewa. Naomba ndugu zangu, kwa kweli Watanzania, Wanambarali, tunawaheshimu sana na tunaheshimu sana Serikali, ahadi kwa barabara hii kila wakati kuahidiwa bila ya kuitekeleza utekelezaji wake kwa kweli hatutaelewa kabisa kama Serikali hii kweli inaona umuhimu wa eneo lile muhimu lenye maeneo mengi ya uzalishaji wa zao la kilimo cha mpunga lakini miundombinu yake ni mibovu.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na tatizo kidogo juu ya barabara hii kwa utekelezaji wake kwamba ndugu zetu wa Maliasili walituomba kwamba barabara ile imepita jirani mno na hifadhi, kwa hiyo, wangeomba sehemu fulani wachepushe. Ilikuwa mwaka 2011, sisi tukakubali kwa nia nzuri, haipo ndani ya Hifadhi imepita pembezoni mwa Hifadhi, tukaona ni nia nzuri. Mwaka umepita sasa mwaka 2012 hakuna kilichofanyika, tuko mwaka 2013 utekelezaji unataka kuanza hawajafanya chochote. Nawaomba ndugu zangu wa Maliasili, wasitulee kikwazo juu ya utekelezaji wa ujenzi wa barabara hii. Sisi tulishawapa muda kama wameshindwa wakubali kwamba *survey* iliyofanyika ndio iwe hiyo hiyo kwa sababu ile barabara kimsingi kwa ramani ambayo ipo, wote tuliona kwa pamoja barabara ile haipo ndani ya Hifadhi. Tusije tukaletewa kikwazo eti nini hakijakamilika; hapana, tuliwapa muda wa kutosha, kama wameshindwa basi sisi tutaendelea na utekelezaji wa kujenga barabara hiyo tusiwekewe kikwazo.

Mheshimiwa Spika, upande wa reli, hainiingji akilini kwa nini Reli ya TAZARA imefika mahali mpaka imekuwa kama haina maana hivi na Reli ya Kati inaonekana haielewekieleweki. Hivi Mheshimiwa Waziri wahusika na hii miundombinu lazima pale kuna kitu ambacho kimejificha hatukioni; haiwezekani TAZARA ilikuwa inabeba abiria wengi, inasafirisha mizigo mingi sana, inafika mahali inaanguka kiuchumi inashindwa kuijendesha. Mimi hainiingji akilini, lazima kuna ulaji pale ambao bado haujagunduliwa kama

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MODESTUS D. KILUFU]

siyo kwenye tiketi basi kuna kitu kinafanyika kibaya. Haiwezekani chombo kama kile muhimu kikawa kinakufa hakiwezi kujiendeleza. Naomba Mheshimiwa Waziri anayehusika na Serikali kwa ujumla, ufanyike uchunguzi wa kina, kuna kitu pale kibaya ambacho kinaendelea kinafanya hizi reli zetu zisiende vizuri.

Mheshimiwa Spika, Reli ya Kati kama ambavyo mchangiaji aliyetangulia alivyosema kwamba, tumekuwa tukipata wawekezaji lakini wasio waadilifu. Tumewapa wawekezaji ile reli lakini hakuna kilichofanyika mpaka leo ile reli haijakamiliika. Nikuombe sana ndugu yangu Waziri Mwakyembe, kule Mbarali wakati wanajenga hii Reli ya *TAZARA* walikuwa wamekusudia kufikisha reli hiyo mpaka Mbarali kwa maana ya *NAFCO* ilikuwepo kwenye Mpango. Sasa sikwambii kwamba sasa hivi, lakini uiweke nayo kwamba tunahitaji Reli ya *TAZARA* ifike Mbarali pale Ubaruku ili mashine zinazokoboa tuachane na malori tuwe tunapakia wakati mwingine kwenye treni tufikishe mzigo kwenye eneo la soko kwa maana Dar es Salaam kwa urahisi zaidi. Siyo hiyo tu, kuangaliwe na maeneo mengine ya uzalishaji kama vile Kapunga kwenye shamba ambalo sasa hivi limechukuliwa na *Southern Highland* kwa maana ya ukulima mkubwa; kuna mashamba makubwa kule nako tufikirie baadaye kuona kama tunaweza tukaunganisha reli ikaenda kule ili usafirishaji wa mizigo kufika kwenye soko uwe rahisi kuliko kutegemea magari peke yake.

Mheshimiwa Spika, niende upande wa nishati na madini. Naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Muhongo, Waziri wa Nishati na Madini pamoja na Naibu wake, kwa kazi nzuri mnayoifanya, endeleeni na jitihada hizo. Tafuteni fedha mahali popote Wabunge tutawaunga mkono, msingojee tu Mipango ya Serikali, inawezekana tusifanikiwe. Fanikisheni jambo hili ni muhimu kwa Uchumi wa Taifa na ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi wetu. Mimi nilikuwa nikisema siku zote kwamba, Kata zangu 20 zilizopitiwa na umeme ni nne tu, sasa hao Wananchi sitegemei kama watakuja kupata maendeleo kama nishati ya umeme hakuna.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. MODESTUS D. KILUF]

Mheshimiwa Spika, tumejenga shule za sekondari kila Kata, tuna zahanati, lakini zote hizi hazina huduma ya umeme; haya siyo maendeleo. Nifafikiri Mheshimiwa Waziri wa Elimu nadhani yupo ananisikiliza, mahali ambapo kuna shule ya sekondari ambayo haitaweza kufikiwa na umeme huu tunaouzungumza sasa wa huduma ya umeme vijijini kwa maana ya *REA*, basi jitihada za makusudi zifanyike mhakikishe hata umeme wa *solar* unapelekwa kwenye shule. Kuiendesha shule sasa hivi bila umeme ni kurudi karne ambayo haijulikani hata kuitaja. Haiwezekani tukawa na zahanati vijijini, tukawa na shule za sekondari, lakini hazina umeme na tukasema tuna Mpango wa Maendeleo. Kwa hiyo tuhakikishe umeme unafika vijijini.

Mimi nashukuru kwamba, Kata ya Madibira kwenye Mpango imo pamoja na Kijiji chake cha Ikoga na vijiji vyote vinavyozunguka Kata ya Miombweni, Ipwani, Mawindi, pale Sekondari mpaka kule Manyenga na vijiji vyote, Kata ya Mapogoro, Utengule Usangu, Mahongole, Ruhija, Vijihi vya Ukwavila vyote, Uturo, Kata ya Himalilo Songwe, Kata ya Igava, Kata ya Luhanga na maeneo mengine ya Vijihi vya Wilaya ya Mbarali sasa nimeona vimeingia kwenye Mpango.

Mheshimiwa Spika, ninakuomba kwa dhati kabisa, Mpango huu usipotekelezwa kwa kweli imani na Serikali itakuwa ndogo. Hawa Wananchi wameshajua na hii mimi nawapelekea na naenda kuwaonesha ndugu zangu Mpango wa Serikali ndiy huu, sasa kama hautatimia sijui tutakuwa na lugha gani? Kwa jitihada ambazo naziona Mheshimiwa Waziri unazifanya na naomba ninapoondoka hapa nipewe ni wakala gani amepewa kazi ya kusambaza umeme Wilaya ya Mbarali. Nitafuatilia kabla sijaondoka kuhakikisha napata wakala waliopangiwa kusambaza umeme wa huduma ya vijijini kwa maana ya *REA* Wilayani Mbarali, sitaondoka mpaka nimejua ni nani wamepangiwa Mbarali.

Mheshimiwa Spika, tunazo bandari zetu, hizi bandari kama zitasimamiwa vizuri nina uhakika ni chanzo kikubwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MODESTUS D. KILUFI]

cha Uchumi wa Taifa hili. Pale bandarini kuna ubabaishaji. Mheshimiwa Waziri kwa bahati nzuri naomba niseme nipo kwenye Kamati ya PAC, tumejaribu kukutana na watendaji wa pale, pale panataka umakini sana, inaonekana kuna ubaguzi.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ni ya pili.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Ooh! Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Namwita Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Kisangi, atafuatiwa na Mheshimiwa Chiku Abwao, Mheshimiwa Rose Sukum na Mheshimiwa Abdallah Mteketa, nafikiri naweza kufika huko.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Awali ya yote, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa mara nyiningine tena kutujalia uhai na kutuwezesha siku hii ya leo kutekeleza majukumu yetu hapa ndani ya Bunge. Pili, nakushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa kunipa fursa hii nami nitoe mchango wangu kwenye hoja hizi mbili za Kamati muhimu katika Bunge letu. Tatu, nitumie fursa hii kuwapongeza sana Wenyeviti wenzangu hawa wa Kamati hizi mbili na Kamati zao kwa ujumila, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuisimamia Serikali katika kipindi chote kilichopita, lakini pia kwa uwasilishaji mzuri wa Taarifa zao mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, pia nitumie fursa hii kuwapongeza Mawaziri, wanafanya kazi nzuri katika Wizara zao. Nitumie fursa hii kusema kwamba, Serikali iongeze jitihada za kukusanya mapato ili ziweze kuhakikisha bajeti ambazo Mawizara haya yamepangwa zinatukufu kama zilivyopangwa na Mawaziri hawa wanatekeleza majukumu

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA]*

yao ipasavyo bila shida. Vinginevyo, tutakuwa kila siku tunapiga kelele hapa Mawaziri hawafanyi kazi, Mawaziri mizigo, kumbe hata fedha za kutekeleza majukumu yao hawajapatiwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuweka kumbukumbu sahihi, naomba nitumie fursa hii kutamka kwamba, ninaunga mkono hoja zote mbili zilizoko mbele yetu. Nianze sasa kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Kwa hoja ya Kamati ya Nishati na Madini, nitumie fursa hii kumkumbusha Mheshimiwa Naibu Waziri, ndugu yangu *Comrade Masele*, Mbunge wa Shinyanga Mjini, ahadi alizozitoa kwenye kikao ambacho tulikifanya pale Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, baina yake, Mbunge wa Jimbo mimi nikiwepo na wahanga wa mgodi pamoja na Wajumbe mbalimbali kutoka katika Halmashauri yetu, tukidai mambo makubwa matatu, moja lilitkelezwa kwa kiasi fulani lakini mawili hayajatekelezwa mpaka leo. Mojawapo likiwa zile fedha za ushuru wa huduma ambazo zimesalia zilipwe kabla watu wa mgodi wa uchimbaji wa dhahabu pale Nzega ile Kampuni ya *Resolute Tanzania Limited* haijaondoka.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii maana nitakuwa mtovu wa shukrani nisiposema jitihada za Mheshimiwa Masele na wenzake kwenye Wizara kwa kuzingatia harakati ambazo mimi binafsi nilizanzisha pale Nzega kudai ushuru wa huduma, zilizaa matunda kwa kiasi fulani mwaka jana kwa Halmashauri yetu kupatiwa jumla ya shilingi 2,340,000,000, fedha ambazo tulikuwa tumedhulumiwa Wananchi wa Nzega kwa zaidi ya miaka 15. Namshukuru Mungu, zilipatikana na zimepatikana kwa ufuutiliaji wetu, lakini pia kwa uelewa mpana na utayari wa Mheshimiwa Muhongo pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Masele, bado tunawadai hawa watu fedha karibu shilingi bilioni nne. Mheshimiwa Masele, nakumbuka ultoa ahadi ya kuwanyima kibali watu wa *Resolute* cha kusafirisha dhahabu kwenda nje ya nchi mpaka walipe fedha hizo. Sasa siyo mpaka tena tupige mkwara wa maandamano

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA]*

ndiyo Mheshimiwa Masele ukumbuke ahadi yako na uanze kuitekeleza.

Mheshimiwa Masele naomba uniepushes na kikombe hicho, tekeleza ahadi yako, watu wa Nzega wapate ushuru wa huduma wa shilingi bilioni nne ambazo zimesalia na kama ulikuwepo Bungeni juzi utakuwa umeona watu wa Nzega tuna mkakati mzuri wa kufanya matumizi sahihi ya fedha hizi kwa kuanzisha Benki ya Watu wa Nzega, Benki ya Jamii ya Nzega (*Nzega Community Bank*). Sasa ukituletea na hizo shilingi bilioni nne zilizosalia, kwa hakika benki yetu itaanza vizuri na tutaweza kuwakopesha Wananchi kwenye *SACCOS*, tutaweza kukuza uchumi wa Wananchi ambao wanahangaika kutafuta mitaji. Naomba ulisimamie hilo.

Mheshimiwa Spika, ahadi yake ya pili, Mheshimiwa Masele alipofika pale Nzega na kufanya kikao kirefu sana na mimi pamoja na wenzangu alituhaidi kwamba, atahakikisha watu wa Mgodi wanaleta fedha ya kifuta jasho kwa wachimbaji wadogo wadogo waliokuwa wakichimba katika maeneo ya Mgodi wa Resolute, wakaondolewa kwa nguvu za *FFU* na hatimaye wakakosa haki zao na sasa wapo *stranded* nje ya Mgodi kwa zaidi ya miaka 15 wakiishi maisha duni sana.

Mheshimiwa Masele uliwahurumia watu hawa na ukasema utaendelea kuwabana watu wa Resolute waweke fedha katika Mfuko ambao ultushauri wewe mwenyewe tuuanzishe wa wachimbaji wadogo wadogo wa *ku-rehabilitate* maeneo yanayozunguka Mgodi pamoja na nyumba za watu hawa ambazo ziliathiriwa; hivyo, tunaomba pia utekeleze ahadi hiyo.

Mimi sitarajii utasubiria mpaka tufanye maandamano, tulikuwa tumeahidi wakati ule wa kwenda kuvamia ule Mgodi, najua sasa utatekeleza ahadi hiyo ili tu kuniepusha ndugu yako na kikombe cha kuitwa msaliti. Sasa naomba utekeleze hilo.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA]

Nitumie fursa hii kumpongeza sana kaka yangu, Mheshimiwa Dkt. Makyembe, kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara ya Uchukuzi. Jana amesemwa sana hapa, lakini niseme tu kama watu mna vita vyenu nya Urais, mumwache kaka yangu msimletee matatizo. Mwacheni atekeleze majukumu yake, anafanya kazi nzuri na sisi tumeiona na tunaitthamini. Wananchi wameona ndiyo maana ile treni kule Dar es Salaam wameibatiza jina la Treni ya Mwakyembe. Endelea kufanya kazi hiyo nzuri na nikupe ushauri tu kwamba, uangalie pia uwezekamo wa kutengeneza *multi model city transit* pale Dar es Salaam ambayo itahusisha uchukuzi kwenye maji, lakini pia uchukuzi wa *trams* kwa maana ya kutengeneza miundombinu hata kama haitajengwa leo, huko tunapoenda siku zijazo kuwe na namna ya kufanya *redesigning* ya ule mfumo wa mabasi yaendayo kasi pale Jijini yaweze kuruhusu pia uwepo wa *trams* katikati ya Jiji la Dar es Salaam. (*Makofii*)

Tukifanya hivyo leo maana yake miaka mitano ama kumi ijayo, ukizingatia kwamba, Mzee Muhongo anataka kuanzisha *sovereign bond* ya fedha zinazotokana na *windflow gain tax* kwenye gesi, tutakuwa na pesa nyngi. Miradi mikubwa kama hii ya *trams* kwenye miji yetu itawezekana. Leo kweli hatuwezi kujenga lakini tuwe angalau na *designs* ambazo zinaruhusu kupanuka na kukua kwa miji yetu katika hali ya kisasa zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie fursa hii kumwomba Waziri wa Nishati na Madini hususan ndugu yangu Mheshimiwa Mwakyembe, nimwache pembeni, Mheshimiwa Massele, pale Nzega bwana tumegundua mgodi mpya wa kuchimba dhahabu. Eneo la Mwanshina ni nje kidogo ya mgodi uliopo sasa. Wamegundua Wananchi na wanachimba pale. Baada ya kuanza kuchimba na kuanza kupata pesa nyngi, tayari Serikali imeingilia imewazuia Wananchi wasichimbe pale. Sasa tunashindwa kuelewa; wanasema lile ni eneo la mgodi sisi Wananchi wa Nzega tunashangaa, wao mgodi wameupigia fensi eneo lao linajulikana, sisi tupo nje sasa kwa nini tunazuiwa tusichimbe dhahabu huko nje maana ndani hatuingii?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA]

Sisi ni wastaarabu, siyo kama wale ndugu zangu wa kule Nyamongo, huwa wanaingia kule kule kwenye Mgodi wa Wazungu. Wazungu wanasema tena na huku nje kwao na wakati wao wanaondoka! Hebu lifuatilie hili, uongee na Mkuu wa Wilaya asimamishe huo mkakati wake wa kupeleka FFU pale kuzuia Wananchi wasichimbe, awaruhusu tu waendelee kuchimba ili waweze kukuza mitaji yao.

Wizara ya Ujenzi, kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Magufuli, unafanya kazi nzuri, nakuomba uhakikishe unatekeleza ahadi ya kukamilisha Barabara ya Nzega – Tabora, ambayo aliitoa Mheshimiwa Rais kwenye kampeni zetu za Uchaguzi mwaka 2010. Barabara hiyo ikamiliike kabla ya mwaka 2015; vinginevyo, ucae ukijua kabisa mimi kurudi hapa Bungeni itakuwa kitendawili. Sasa kama umechoka kuniona humu Bungeni basi endelea kuchelewesha kupeleka fedha kule Nzega na utakuwa na uhakika mwaka 2015 hautaniona tena, maana hii ni ahadi ya Chama cha Mapinduzi ambayo mimi natakiwa kuisimamia na ninakuomba sana kuhakikisha ahadi hiyo inatekelezwa kwa wakati.

Daraja la Russu kule Nzega ni la *TANROAD*, limevunjwa na maji mwaka jana na mimi nilishasema hapa Bungeni kwamba, lilijengwa chini ya kiwango na hivyo mvua zilliponyesha tu mwaka jana likavunjika, kudhihirisha kwamba pengine mimi ni *engineermzuri* zaidi kuliko waliosimamia ujenzi wa daraja hilo. Ninaomba sasa Mheshimiwa Magufuli, upeleke fedha pale daraja hilo liweze kufanyiwa ukarabati liweze kuendelea kutumika kwa sababu ni kiunganishi kikubwa cha Wananchi wa Jimboni kwangu.

Pia daraja lingine limevunjika kule Nihele na Chomochankola kuunganisha Wilaya ya Nzega na Wilaya ya Igunga, nalo ni la *TANROAD*, tunaomba pia lijengwe likamiliike.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, kuna mtu mmoja hapa jana alipokuwa akizungumza alitumia

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA]

muda wa Bunge hili vibaya sana kwa kuhangaika sana na mambo ya Nzega. Juzi nilimkumbusha kwamba ya Nzega atuachie Wananzega wenyewe, hayamhusu yeye mtu anatoka Ole huko shambani.

*(Hapa kengele lilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili, afadhalii imegongwa maana hayo! Sasa tuendelee na Mheshimiwa Mariam Kisangi, atafuatiwa na Mheshimiwa Chiku Abwao. (*Kicheko*)

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Hotuba hizi za Wenyeviti.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda niwapongeze Wenyeviti wote wa Kamati hizi, kwa kazi nzuri waliyoifanya. Napenda niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wa Chama cha Mapinduzi wa Kamati hizo zote kwa kazi kubwa wanayoifanya. Wizara hizi zinafanya kazi. Serikali inafanya kazi. Mimi nilizaliwa miaka 50 iliyopita, Mkoa wa Dar es Salaam kulikuwa hakuna barabara wala gari, tulikuwa tunatembea kwa miguu kutoka Temeke hadi Ilala na Kariakoo. Leo magari na madaladala kila kona, yale ni maendeleo makubwa. Serikali ya Chama cha Mapinduzi inawajibika ipasavyo. Kila palipo mazuri mabaya hayakosekani, hilo ni jambo la kawaida. Mimi naipongeza sana Serikali yangu kwa kazi wanayoifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitachangia katika masuala mbalimbali lakini mengi yameshazungumzwa na wenzangu sitayarudia. Nitazungumzia suala zima la Mradi wa Mabasi Yaendayo Kasi katika Mkoa wa Dar es Salaam. Mradi ule kwa sasa napenda niipongeze Serikali kwani imeshaonesha sura. Sura halisi ya Mradi ule imeonesha kwamba, sasa tuna maendeleo. Iwapo Mradi ule utakamilika, basi tutakuwa na maendeleo makubwa katika Mkoa wa Dar es Salaam. Mimi naipongeza sana Serikali, lakini kila palipo na mazuri mabaya hayakosekani. Katika kipindi hiki cha ujenzi wa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. MARIAM N. KISANGI]*

Mradi ule, kweli kujenga au kukarabati nyumba iliyoharibika au chombo chochote kilichoharibika kazi yake ni kubwa. Wajenzi wale nawapongeza sana kwa sababu wanafanya kazi katika wakati mgumu, magari yanatembea barabarani huku na wao wanajenga. Hiyo ni kazi ngumu, naipongeza sana ile kampuni iliyoshika ujenzi wa barabara ile. (*Makofii*)

Kinachotupa shida, msongamano wa magari katikati ya Jiji umezidi kuwa mkubwa. Juzi niliongea hapa kwenye maswali na leo nasisitiza tena, naiomba Serikali waangalie yale maeneo ambayo yapo tayari kabisa, yameshakuwa tayari waweze kufungua ili tuweze kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, sasa nitazungumzia uboreshaji wa reli. Reli ni roho ya Tanzania, reli ni maendeleo ya Tazania na ni Uchumi wa Tanzania. Kupatikana kwa Reli ya Kati hii, ikizinduliwa ikifunguliwa ikiendelezwa vizuri, itatusaidia sana katika kukuza Uchumi wa Tanzania. Mimi naiomba Serikali ifanye juhudhi ya makusudi kabisa ili reli yetu iweze kuboreshwa na kufanya kazi yake vizuri kwa maendeleo ya Tanzania.

Reli ya *TAZARA* ni mkombozi wa watu amba wana uwezo mdogo. Reli hii inabeba Watanzania wengi wanaotoka Dar es Salaam kuelekea Mikroani. Reli ile ilikuwa mkombozi mkubwa, lakini kila siku tunaisikia ina hile na lile. Pamoja na juhudhi za Mheshimiwa Waziri, namwona jinsi anavyowajibika na anavyoenda kufuatilia ile reli. Mimi naomba niwashauri muendelee kuboresha reli ya kutoka Dar es Salaam mpaka Zambia ambayo inapitia pale Mbeya, inasaidia sana Wananchi wa kawaida kupata usafiri wa bei nafuu na ulio salama.

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie tena ujenzi wa boyla la *SBM*. Serikali ilikuwa na nia njema sana ya kujenga lile boyla la *SBM* kwa lengo la kufanikisha mpango wa uletaji mafuta kwa pamoja. Sasa boyla lile cha kushangaza lina mlango mmoja tu wa kutoa *diesel/hakuna petrol*. Kamati ilitembelea pale na naomba *ni-declare*

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[MHE. MARIAM N. KISANGI]*

interest, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati ya Madini kwa kipindi chote nilichokuwa hapa Bungeni. Kweli Mradi ule ulienda kwa juhudhi kubwa hata sisi Wanakamati hatukuutaraja ule utaenda kwa wakati, lakini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tumefanikisha. Panapo mafanikio ipo changamoto, iweke sehemu nayo ya kuleta *petrol* isilingize *diesel* peke yake, vinginevyo, lundiko la bei kule inabaki kuwa vilevile. Naomba Serikali ilizingatie hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niende sasa kwenye upande wa nishati na madini. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Timu yake. Upande wa Nishati jamani, umeme pamoja na maneno yote yanayosemwa lakini ya juzi siyo ya leo! Giza linakuja lakini na sababu zinatolewa, mimi naipongeza Wizara. Nitaelezea tu, kuna changamoto kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alivyokuwa anasema kwamba, kuna miundombinu, ujenzi wa miundombinu na kukatikakatika kwa umeme.

Mheshimiwa Spika, mimi narudia tena, ukuaji wa Jiji la Dar es Salaam sijui hata linakua vipi? Tukiangalia mfano mdogo tu, juzi tulikuwa na tatizo la Barabara ya *Kilwa*, tulikuwa na barabara moja, Serikali ikajenga barabara mbili zile. Leo barabara zile hazitosh! Jinsi gani Mji unakua kwa spidi hazitosh, ukifika Mtoni hakuna barabara unakwenda Mbagala Rangi Tatu, yaani ni foleni mnakwenda hivi mpaka unavuka Kongoi yote ni foleni. Sasa hii inaonesha jinsi gani jiji lile linakua kwa kasi sana. Naiomba Serikali, mipango yake iangalie sana kwa kipindi kijacho kwa Jiji hili la Dar es Salaam.

Mfano mwingine juzi juzi nikiwa kwenye Kamati hapa, Serikali imejitahidi kujenga mitambo ya umeme; Kisutu tukapata transforma kubwa, Mbagala, Buguruni, Mwananyamala, hiyo yote ni juhudhi za Serikali. Baada ya muda umeme unakatika, vile vifaa havitosh, sasa tunajenga *sub-station* nyingine. Kwa hiyo, niangalie pamoja na juhudhi zote za Serikali na Wizara jinsi gani inaweza kulishughulikia suala la umeme. Iangalie jinsi gani na spidi ya ukuaji wa jiji lile. Tutakuwa ni tatizo kubwa, tunakuwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. MARIAM N. KISANGI]*

tunawekeza hela nyingi kwenye vitu, baadaye vile vitu havifai tena, tunatakiwa tulete vingine vipyta, hili ni tatizo. Kwa hiyo, tuangalie mipango yetu kwa muda ujao tulilenge Dar es Salaam kwa kipindi kijacho itakuwaje na ukuaji wa miji. Nilisema waangalie, napenda ni-*declare interest*, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mipango Miji Manispaa ya Temeke. Vifaa vinavyotolewa huko Kibada ujenzi wa nyumba na nini na kila anayejenga anahitaji umeme. Sasa Serikali inajitahidi na Wananchi wanajitahidi kutaka maendeleleo. Kwa hiyo, hapa kuna changamoto ambayo tunatakiwa tuiangalie.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la umeme Kariakoo. Miundombinu ndiyo, umeme unakatika maeneo mengi, lakini wafanyabiashara wa Kariakoo, Kariakoo nilmefanya uchunguzi umeme unakosekana mara nyingi sana. Pale ni Kitivo cha Biashara; Kariakoo sasa hivi ukienda kuna Wanajigeria, kuna makabila tofauti yanakuja kununua biashara Kariakoo. Mimi naomba tuangalie uboreshaji wa umeme Kariakoo, angalau na ule mkusanyiko wa watu, watu wapate hata hewa ya ziada ya feni; vinginevyo, tutaibua maradhi. Watu ni wengi Kariakoo, lakini pia yale ma-generator kila generator lina mlion na moshi wake, ule ni uchafuzi wa mazingira. Naiomba Serikali, wafanyabiashara wa Kariakoo walipe kodi lakini pia na huduma muhimu wapewe katika kuboresha biashara zao.

Mheshimiwa Spika, mengi yamezungumzwa na wenzangu, mimi niliona niangalie yale ambayo hayakzungumzwa na wenzangu. Naunga mkono hoja hiyo, nazidi kuwapongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, iendelee hivyo, Mwenyezi Mungu atatubariki. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante. Namwita Mheshimiwa Chiku Abwao, atafuatiwa na Mheshimiwa Rose Sukum halafu Mheshimiwa Abdul Mteketa!

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Nishati pamoja na Miundombinu.

Awali ya yote, ningeomba kusema maneno machache. Ofisi yako imetuwekea utaratibu mzuri sana Wabunge, ambapo kabla ya Bunge tumekuwa tunakaa katika Kikao cha *Briefing*, kikao ambacho kiliwekwa kwa makusudi tuweze kujadiliana mambo yetu yanayotuhusu, ambayo tunaweza tukazungumza upana na kwa nafasi kubwa. Cha kusikitisha, badala ya kukitumia kipindi hicho cha *briefing* ambacho ultiuandalia tunakuja kuumbuana ndani ya Bunge.

**SPIKA:** Tulishalitolea uamuzi, naomba uendelee kujadili mengine.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Spika, najua na sina nia yoyote ya kulirudia wala kuzungumza isipokuwa naomba kusisitiza kwa Wabunge wenzangu kwamba, tutumie vizuri ile siku. Kama kuna hoja zozote ambazo zinatukwaza tuzungumze siku ya *briefing* ambapo ndiyo mambo yetu yote tutamalizia huko. Hilo lilikuwa ndiyo lengo langu ili kujaribu kukumbushana na wenzangu tujiveke vizuri.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sasa nirudi katika hoja iliyopo mbele yetu. Mimi kama Mbunge wa Mkoa wa Iringa, nimekuwa nikifanya ziara mbalimbali. Katika ziara zangu nimeelekeza nguvu yangu katika vijiji, Majimbo ambayo yako nje ya Mji wa Iringa. Mkoa wa Iringa umepata bahati ya kuwa na vyanzo vya umeme ambavyo vinaingia kwenye Gridi ya Taifa, kuna Mtera, Kihansi na Kilolo. Kwa bahati mbaya Mkoa huu wa Iringa na hasa katika maeneo ambayo yana vyanzo hivyo vya umeme, jitihada za Serikali za kuhakikisha watu wa kule wanifuai na umeme, zimekuwa ni ndogo sana. Nilikuwa Kilolo wakati wa uchaguzi mdogo, Kijiji kimoja cha Nyangande, Wananchi walilalamika sana wakanionomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na kwamba, umekuja kwenye kampeni, tunakuumba utupelekee kilio chetu, hili suala la umeme tunesahaulika

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. CHIKU A. ABWAO]

pamoja na kwamba, sisi ndiyo tunaotunza hiki chanzo cha maji ambacho kinazalisha umeme, lakini sisi wenyewe hatuna umeme na kwa kweli nilikaa gizani kipindi chote cha kampeni mpaka nilipomaliza.

Zaidi ya yote, nielekeze kwenye Jimbo langu ambalo nimekuwa nikipeleka nguvu zaidi kuhakikisha Wananchi malalamiko yao waliyonitura niyafikishe leo. Ninaomba pia Waheshimiwa Wabunge wanielewe maana siku zote nikigusa Jimbo la Isimani, inaonekana kama kuna chuki ama kuna lolote hapana. Mimi kama mwanamke tuna jitihada ya kushika Majimbo. Wanawake wote ndani ya Bunge hili, naomba tupeleke nguvu zetu kushika yale Majimbo hasa ambayo tunaamini kwamba, yana malalamiko mengi ama Wananchi wana shida wanataka tuwawakilishe Bungeni tuache kuangalia upande mmoja.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hilo nimefanya kazi sana Jimbo la Isimani. Jimbo la Isimani ambalo lina Taarafa tatu, lina Kata 12 na vijiji 67. Katika vijiji vyote hivyo 67, kuna umeme katika vijiji visivyo zidi saba. Wananchi wa Isimani wanalia sana suala la umeme na kama nilivyosema, umeme unaanza kwoa unapita juu kwa juu Wananchi wa kule hawana umeme. Wakati wananiomba nije nizungumzie suala hili wamesema wanaona kabisa jitihada za Serikali maeneo mengi yanapelekewa umeme, lakini wao wamekosa nini? Mpaka iwe vijiji saba tu na hata katika vijiji hivyo wanamshukuru sana Baba Paroko anayeitwa Salvatory, alikuwa upande wa Isimani zamani, sasa hivi amehamia upande wa pili wa Isimani, ambayo ni Idodi. Kwa hiyo, Wananchi wanalia, vijiji vingi wameniomba kwa majina kabisa naomba nivosome kwa sababu sina uzoefu sana na vijiji vya kule. Vijiji ambavyo vina umeme ni Migori, Makutopola na Mtera. Huo ni upande wa Tarafa ya Isimani. Upande wa Pawaga ni Boliboli na Idodi yenyewe, lakini maeneo mengine yote kwa kweli ni shida. Wana shida sana Wananchi wa Isimani, wameniomba niwaletee ujumbe huu na pia ninavyoleta ujumbe nisisemwe, kwa sababu Iringa pamoja na bahati ya kupata Wabunge ambao ni Mawaziri, lakini pengine kutokana na shughuli nyingi za

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[MHE. CHIKU A. ABWAO]*

Kiserikali, wanashindwa kuwawakilisha. Kwa hiyo, wameomba mimi niwe mdomo wao Isimani kwamba, niwe nasema, inawezekana wengine wamepata umeme kwa sababu wanasmewa ndani ya Bunge hili. Kunakuwa na watu wanadai, kuna watu wanauliza maswali, wanawasemea kwa niaba ya Wananchi wale ambao wanawawakilisha, lakini hawa ambao wanawakilishwa na Mawazari kutokana na shughuli nyngi za Mawaziri inashindikana kuwajibika kwenye Majimbo yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Mawaziri wahusika mpeleke nguvu hizi Jimbo la Isimani, Wananchi wa Isimani wana kilio kikubwa, hawana umeme, wanaishi katika mazingira magumu sana. Kutokana na kukosa umeme wanazidi kuwa maskini. Kwa sababu unajua umeme pia ni mtaji kwa wafanyabiashara. Umeme unamfungua mtu akili hata kusema afanye biashara gani, hata wawekezaji hawafikirii kwenda Isimani, Isimani ni kukavu kuna shida, hakuna maji, hakuna umeme, unakwenda kule ukafanye nini?

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe ninayezungumza hapa, pamoja na kwamba nilitangaza nagombea Isimani watu wananicheka, wanasmaje wewe unachaguaje Jimbo gumu hilo? Utaendaje kugombea Jimbo ambalo miundombinu katika nchi hii imesahaulika? Mimi nasema kwa nia njema kabisa, kwa sababu lengo langu ni kuwasaidia Wananchi ndiyo maana nimekuwa mwanaasiada ili niweze kupata fursa ya kushiriki katika kuhamasisha maendeleo ya maeneo ambayo pengine kwa kukumbusha kwangu, Serikali pia inaweza ikatazama kule. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi nimesimama leo ajenda yangu kuu ni hii kwamba, Wananchi wa Isimani wana kilio kikubwa. Jimbo lenye Tarafa tatu, Kata 12, Vijiji 17, lakini havizidi Vijiji saba vyenye umeme. Jimbo ambalo ni la siku nyngi siyo jipya kusema limeanza juzi. Jimbo ambalo linawakilishwa Bungeni miaka yote. Jimbo ambalo Wananchi wa kule wangalipwa fadhila na Chama cha Mapinduzi na hili nimekuwa nikilisema hata kama nitaonekana

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. CHIKU A. ABWAO]

mchonganishi. Nimekuwa nikizungumza kwenye Jimbo kwamba, muwaone hawa watu wa CCM hawana fadhila msiwachague, kwa sababu jinsi mnavyowachagua badala ya kuwalipa fadhila na mapenzi mnayowaonesha kwa kuwatendea wema kuhakikisha kwamba ninyi ndiyo mnahudumiwa zaidi, ndiyo kwanza mmetoswa wanaenda kubembeleza Majimbo ambayo yamenyang'anywa yako kwenye Upinzani ndiyo wanapewa huduma. (*Makof*)

Nimekuwa nikisema hivyo, inawezekana ni kauli ya uchonganishi lakini ukweli ni kwamba, inatokana na uhalisia ambaao upo katika eneo hilo. Wabunge wa Isimani wamesema tena wanasema Mheshimiwa Spika wetu mtu wa Mkoa wa Iringa na yeye ana machungu na Serikali kuona Mkoa wake pia hauna maendeleo. Kwa hili nalo pia linaleta uzito mwingine tena kwamba, Iringa ni Mkoa ambaao tuna bahati kubwa kupata Vlongoz ambapo Majimbo yetu yanekuwa yanatisha kwa maendeleo, lakini kibaya zaidi, ndiyo maeneo ambayo yako nyuma sana kimaendeleo ukiacha Iringa Mjini. Labda kwa sababu Iringa Mjini watu wajanja, maana wao wakiona Mbunge huyu hafai wanamtoa wanamchukua mwingine, tumekuwa tukiopokezana mara CCM mara CHADEMA. Hii nayo nafikiri imikuwa ni changamoto ya maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nimeongea hapa kwa njema kabisa, naomba niwakumbushe Mawaziri wetu, katika harakati za kuhakikisha nchi yetu inakuwa na umeme, wapeleke nguvu katika Majimbo haya hasa Isimani pia na Kilolo. Kilolo nao wamenituma ingawa sitaki kusemea sana, kwa sababu sijafanya kazi kule, nisije nikasemea maeneo ambayo sina uhakika nayo. Nimeamua kusemea eneo ambalo nina uhakika nalo. Iringa tunakosa kusonga mbele kwa sababu ya miundombinu. (*Makof*)

Ukirudi hata katika masuala ya barabara ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili. Mimi mkoa wangu ni Njombe!  
(*Kicheko*)

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Umetuhama lakini ulikuwa Iringa. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa naomba tuendelee na Mheshimiwa Sukum, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Mteketa!

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa na mimi fursa ya kuweza kuchangia hoja za Kamati hizi mbili. Niwapongeze Kamati zote mbili kwa kutoa Taarifa zao nzuri na maoni ambayo yanajenga nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la nishati chini ya Mpango wa Matokeo Makubwa ya TANESCO, ambayo imepewa Miradi 28, kwa lengo la kupata umeme wa kutosha nchini. Mimi ninapata mashaka sana kwa sababu umeme wenyewe wanaouzungumzia wanazungumzia suala la majenereta. Sasa kwa kipindi cha bajeti taarifa iliyotolewa ni kwamba, takribani trilioni mbili zilitumika kwa ajili ya kununua mafuta mazito kuendeshea hizo jenereta kwa ajili ya kupata umeme wa kutosha. Sasa nadhani ifike wakati tuelekeze nguvu kubwa kwenye umeme wa maji ili tuweze kuondokana na matumizi makubwa.

Ninazungumzia hivyo kwa sababu wenzetu Wakala wa Bonde la Rubada wana uwezo wa kuzalisha umeme wa megawati 2,011 kwa kutumia maji ya Mto Rufiji. Sasa kwa nini Serikali isikope fedha kuelekeza kule ili tuweze kupata umeme wa nafuu na wa kutosha nchi nzima na pia kwa nini tuisiangularie suala la umeme wa maji kwenye mito mingi ambayo ipo ndani ya nchi yetu tukiekelea upande wa Kaskazini mito ni mingi kwenye Milima ya Meru mito ni mingi kwenye Mlima wa Kilimanjaro mito pia ipo mingi na kwenye maeneo ya Ngorongoro na pia upande wa Kusini

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. ROSE K. SUKUM]

vivyo hivyo; kwa nini tusiekeleze nguvu huko tukaondokana na gharama kubwa kama hiyo?

Mheshimiwa Spika, si busara Serikali kukumbatia gharama, tuondokane na hizo gharama kubwa tupate umeme wa kutosha.

Naelekea kwenye upande wa *REA*. Wakala wa Nishati Vijiji wanafanya vizuri na wanafanya kazi yao nzuri pamoja na *TANESCO*. Baadhi ya Watumishi kwa kweli vitu wanavyofanya kule vijiji siyo vizuri. Kwanza, umeme unasuasua kufika kwa Wananchi. Vijiji vyenyewe vilivyochanguliwa ni vichache kwa wengine ni vingi. Mimi nashindwa kuelewa kwa nini uwiano haulingani Wilaya na Wilaya! Kwa nini Wilaya nydingine inakuwa na vijiji kama 52 au vituo 52 vya kupata umeme, Wilaya nydingine kama Hanang inakuwa na vituo 12? Kwa nini hamna uwiano kwani watu wengine hawahitaji huo umeme?

Mimi nina uhakika kwamba, tunahitaji. Umeme mwingine wala haupo mbali. Sijui wafanye hiyo *survey*, unaweza kukuta uko kilomita tatu; kwa mfano, Hilbado ipo kilomita tatu kutoka Singa A. Singa A wana umeme Hilbado hawana. Kwa nini wasitumie hiyo busara kuweza kuvuta umeme kwa urahisi kwa ajili ya kuwafikia watu wengine? Wengine wapo barabarani umeme umepita juu chini hawana umeme. Hivi ni kwa nini tusitumie utaratibu mzuri *REA* ikafikisha umeme kwa watu wote. Mimi nadhani sasa hivi inafikia mahali wenzetu wa *REA* tuangalie ni jinsi gani umeme unawafikia Wananchi wote. Tunahitaji umeme kwa ajili ya mawasiliano. Bila kufanya hivyo, hatutaweza kuleta maendeleo. Kubwa zaidi, Watumishi wamekuwa wabahirifu au wanyonyaji. Watumishi wengi utakuta wanawaambia hakuna nguzo ya umeme wakati Mwananchi halipii hiyo nguzo. Kwa nini Mwananchi alipie nguzo ya umeme wakati *REA* imepewa pesa na Serikali kwa ajili ya kuendesha huo mradi?

Wakati mwingine wanasema hakuna mita watu walipie, wakati hela zimeshatolewa kwa ajili ya kuongeza

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[MHE. ROSE K. SUKUM]*

huo umeme. Mimi nadhani tuangalie ni suala lipi ambalo linatakiwa litumike kwa ajili ya kuleta maendeleo ndani ya Wilaya zetu zote nchi nzima kwa ajili ya suala la umeme wa REA na TANESCO.

Mheshimiwa Spika, nichangie kuhusu suala la madini. Kumekuwa na vitendo vya wizi, udanganyifu na utoroshaji wa madini nchini. Haya madini yangetosheleza kabisa kwa maendeleo yetu. Mimi nashukuru sana Kamati imeenda kutembelea nchi za wenzetu na jinsi gani wamejifunza namna ya kudhibiti matumizi au utoroshaji wa madini au ni jinsi gani wanapata yale mapato. Sisi tumeelekeza sana nguvu zetu kwa ajili ya mikataba mibovu. Hivi ukiniambia kwamba, kwenye madani STAMICO wanawekeana asilimia 50 kwa 50. Hivi 50 kwa 50 huku huyu mtu anatorosha hayo madini bado wewe hujafaidi unasema asilimia 50. Umepata wapi hiyo asilimia 50 wakati ametorosha madini?

Wao wenyewe wameeleza kabisa kwenye taarifa yao kwamba, takribani tani 20 za dhahabu huzalishwa, lakini zinazotolewa kwenye Mamlaka zinazohusika ni tani mbili, ina maana kwamba, tani 18 zote zimetoroshwa. Kwa upande wa *Tanzanite* ni kilo moja tu inayopelekwa au inayotolewa kwa taarifa, lakini kilo tatu zote zimetoroshwa. Sasa siyo hizo tu, hawa ni wachimbaji wadogo wadogo; je, kwa wale wachimbaji wakubwa wanatorosha kiasi gani mbona hamjatueleza? Kamati ilienda kuangalia kwa wachimbaji wadogo wadogo tu, kwa wachimbaji wakubwa tunataka kujua pia taarifa yao ikoje. Hebu tuipate vizuri kwa sababu tuna mashaka sana na wachimbaji wakubwa zaidi kwamba wanatorosha madini yetu hapa kwetu Tanzania na tunakosa maendeleo kwa sababu ya utoroshaji huo mkubwa.

Pamoja na kwamba, wamesema Mererani pale wamejenga sijui shule sijui wamejenga nini, nendeni mkaione Mererani ilivyo; inachekesha hiyo barabara ya kilometra moja ya kitu gani, barabara ya kilometra moja wanatosha watu wa Mererani kuchimba. Wao wamechukua madini mengi wanatakiwa watengeneze barabara nzuri mpaka

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. ROSE K. SUKUM]

ifike Barabara ya Moshi – Arusha ya lami kwa sababu wanachukua hela nyingi sana wenzetu wa madini. Vivyo hivyo madini kwenye maeneo ya Mwanza, wenzetu wanachimba madini ya dhahabu Shinyanga na Mwanza. Mle ndani mawe yaliyochimbwa ni makubwa sana na mengi mno. Ukikuta vijiji vilivyozunguka pale hali ni mbaya sana.

Tunasema eti wenzetu wanasaidia sana vijiji nya jirani, hawasaidii vijiji wala hawawasaidii wale wachimbaji wadogo wadogo wanawaonea na hata wafanyakazi wao wanawaonea. Kwa hiyo, tunatakiwa kuangalia ni jinsi gani tunaboresha sasa haya madini yetu sisi Watanzania tufaidi. Kwa hiyo, kitachotakiwa wao katika mikataba yao ibadilishwe, Serikali ichukue asilimia 60 wao wachukue 40, kwa sababu wao huku wanaiba, mle ndani huwezi kuruhusiwa kuingia wanaingia wenyewe. Hata hawa Wataalam wetu wa *TMA* hawaingii mle ndani, kuingia ni vigumu.

Sisi tukienda pale kama Wabunge tunaambiya hamna kuingia mwisho ni hapa, hata wale ni hivyo hivyo. Watasema tunaingia lakini siyo kweli hawaoneshi hali halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie miundombinu, ujenzi. Mimi kwanza niwasifie sana upande wa ujenzi ...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili, ahsante sana. Namwita Mheshimiwa Mteketa!

**MHE. ABDUL R. MTEKETA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi naona umenipa nafasi nzuri na ninakuwa mchangiaji wa mwisho katika kipindi hiki. Kwanza kabisa, napenda kuwapa pongezi Wenyeviti wote wa Kamati hizi ambazo tunazijadili. Pili, nawapongeza Mawaziri wote watatu ambao mimi nawaita *Big Three*, kazi yao inaonekana na wastahili sifa sana. (*Makofii*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. ABDUL R. MTEKETA]

Zaidi, napenda kujikita katika Jimbo langu hasa hasa nikianza na nishati. Kilombero inakua na tuna gridi mbili; Gridi ya Kihansi na Gridi ya Kidatu. Ifakara sasa ni Mji Mdogo, umeme unahitajika sana, lakini kuna kero ya umeme ambayo haijawahi kutokea Duniani; kila wiki umeme unakatika tunaweza kukosa siku tatu, siku nne, bila umeme na sababu za maana hakuna. Sasa tunashangaa tatizo hili linatokana na nini! Tunamwomba Bwana Muhongo, nimeongea na Bwana Simbachawene, japo kidogo kujaribu kutembelea Ifakara mwone tatizo hili linasababishwa na nini.

Vijana wengi wana mashine za mpunga wanashindwa kusaga na unajua mpunga unafuata juu, wakianika ukishakauka kwenda kusaga kama umeme hakuna ukilala unaharibika unakuwa chenga. Kwa hiyo, wanapata hasara sana na watu wengine wanaofanya biashara zingine, ndugu zangu wengine wameshazungumza.

Pili, nakwenda kwenye miundombinu, tunaishukuru sana Serikali ya Tanzania hasa Rais wetu kwa ahadi yake ya Daraja la Kilombero, amelijenga sasa hivi linaendelea. Ninatoa shukrani nyngi sana kwa hilo. Pia kuna barabara kutoka Kidatu kwenda Ifakara, hiyo bado ina matatizo, ina lami kilomita 16 tu ambapo kilomita kama hamsini na kitu bado hazina. Sasa mtu anatoka Dar es Salaam mpaka Kidatu ni kama maili 330 kwa muda wa saa nne, lakini akitoka Kidatu kwenda Ifakara anachukua tena saa nne, kilomita 70. (*Makofii*)

Tunaomba tuangalie kitu hicho na sisi kidogo tufaidike, kwa sababu kule kuna wawekezaji wengi, *KPTL* wanatengeneza mashamba ya mpunga huko Mgeta na vilevile wanalalamika kuhusu miundombinu. Pili, nataka kusema kwamba, Tanzania tukiachia Serikali tu kila kitu ifanye Serikali, inakuwa ngumu lazima tuangalie na wawekezaji. Tuwaone wenzetu wanaotengeneza barabara kwa kutumia wawekezaji, tusiogope kwamba mtu akija kuwekeza kwenye barabara halafu akilipa *road*

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. ABDUL R. MTEKETAJ]

toll Wananchi watalalamika, hapana. Hivi hatuwezi kuendelea, tuwaache wawekezaji wawekeze, *road toll* ziwe kama kawaida.

Ziara yetu tuliyokwenda juzi tumeona Malaysia kuna *road toll* na barabara zile wametengeneza *Private Sector* na wale *Private Sectors* wanavichunga wenyewe Serikali hawana tena tabu ya ku-repair zile barabara. Tunaomba vitu kama hivi Serikali yetu iviangalie sana, msiogope, tumewachagua kutuongoza, lawama zitakuwepo, fanyeni kazi kwa Watanzania. Nabii Issa alienda Jerusalem, alipokelewa vizuri sana, watu wakatandika kanga, lakini siku ya kusulubiwa ni wale wale waliotandika kanga walipiga mayowe msulubuni, msulubuni. Kwa hiyo, msiogope, tusiogope tusianze kuleana. Kama unaona kitu kipo kinaweza kufanya kazi kinaweza kuleta tija kwa Wananchi kifanye usiogope. (*Makof*)

Bwana Mwakyembe, ulikuja na kasi nzuri sana *Airport* ukakamata watu ukawawaweka ndani wapi huko wakifanya shughuli nyingi sana zikaonekana lakini mwisho wake hatujui ni nini? Unga uliokamatwa umegeuka kuwa unga wa muhogo, lakini hapa Watanzania wameshaathirika pale *Airport* wamefukuzwa kazi na wengine wamepelekwa Mahakamani. Hao watu waliupeleka unga wako mjini wamesharudi hawachukuliwi hatua. Sasa tunawaonea huruma wenzetu wanaofanya kazi pale wamekamatwa kwa kosa gani kama ule kweli ni unga wa muhogo? (*Makof*)

Tunaomba kabisa vitu kama hivyo tukianzisha na tunapovimaliza vionekane visiwe kama vinaharibika tu, vinakaa kimya watu hatuelewii vinaishia wapi. Tunawasifu sana, tunawaamini sana, nyinyi ni *talk of the country*, watu watatu ninyi; Magufuli, Muhongo na Mwakyembe, tunawasifu sana, lakini kazi zenu msianze kuogopa na kutishwa, mlivyoanza na spidi yenu nendeni. Muwe radhi kufa kwa Watanzania kwa sababu mmechukua majukumu hawa Watanzania wanawaamini. Fanyeni kazi hiyo vizuri zaidi. (*Makof*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. ABDUL R. MTEKETA]

Mheshimiwa Spika, tatizo langu lingine linakuja kwenye simu. Nimepiga kelele sana habari ya simu Masagati huko watu mpaka wanapanda juu ya miti. Tulishawaambia wahusika walituambia ikifika Desemba mwishoni minara itakuwa imeshafika Masagati lakini mpaka leo hata dalili hazionekani kadhalika na Uchindile. Tunaomba Serikali iangalie vitu hivyo. Msilogope kutafuta watu wa ubia, msilogope *investors*. *Nyali Bridge* Mombasa waliweka *investors*. *Kenya Government* ilishindwa enzi hizo, *investor* akaweka *Nyali Bridge* watu wakawa wanalipa *tolls* pale mpaka jamaa pesa yake imerudi. Kwa hiyo, tusilogope kama kuna madaraja, kama kuna nguzo za simu, tuwaagize watu ambao wanaweza kutufanya kazi. Watu wanakaa na mahela mengi sana nje wanashindwa mahali pa ku-*invest*.

Ukija Tanzania kuna tatizo vilevile, *Tanzania Investment Centre* mwekezaji akitaka kuomba anachukua miaka mitano, anaomba tu, anakaa tu. Sasa hiyo kitu inakuwa siyo halali. Tuangalie *investors* wanaweza kuisaidia Serikali yetu kwa vitu vingi sana.

Mheshimiwa Spika, sitaki kupoteza wakati wako, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante. Muda tulionao hautoshi, kwa hiyo, siwezi kumwita mtu mwингine. Mchana tukija tutakuwa na wachangiaji kutoka sehemu ya Wabunge watatu tu, maana ninyi mnapochangia mnagusa sekta zinazohusika, kwa hiyo, itabidi wajibu. Naibu Waziri wa Madini dakika kumi, Naibu Waziri wa Nishati dakika kumi, Waziri wa Nishati na Madini dakika kumi, Waziri wa Ujenzi dakika kumi, Waziri wa Sayansi na Teknolojia dakika kumi, Waziri wa Uchukuzi dakika 20, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu atapewa dakika 30 na Mwenyekiti wa Nishati na Madini dakika 30. Kwa hiyo, siku itakuwa imekwisha.

Sina matangazo mengine. Mchana watakoanza yuko Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Deo Sanga na Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, ni hao watatu.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[SPIKA]*

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.57 mchana Bunge lilitifungwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala. Tunaanza na Mheshimiwa Pindi Chana, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Sanga!

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi. Nianze kwa kuwapongeza Wenyeviti wawili waliowasilisha Hoja ya Miundombinu na Masuala ya Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu imefanya vizuri sana katika suala zima la mawasiliano hususan barabara. Barabara nyingi zimejengwa, maeneo mengi yalikuwa hayafikiki, lakini leo hii tunashuhudia yanafikika na hivyo nawapongeza sana Mawaziri wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikubaliana hapa kwamba, tuwe na barabara ambazo zinaunganisha Mikoa na Mikoa na Wilaya na Wilaya. Leo nataka nizungumzie barabara inayotoka Njombe – Ludewa – Manda; hii ni barabara tumeomba muda mrefu ijengwe kwa kiwango cha lami. Tangu nikiwa msichana mdogo chipukizi, barabara hii tumekuwa tukizungumzia sana na hadi leo hii watu tuna-graduate mpaka *Ph.D* barabara hii bado tunaizungumzia. Ningemba sana barabara hii iangaliwe kwa jicho la huruma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ya kutoka Njombe – Ludewa – Manda ikikamilika kuna daraja la Mto Ruhuhu, daraja hili linaunganisha Mkoa mpya wa Njombe na Mkoa wa Ruvuma. Kwa hiyo, sambamba na barabara hii, pia nakumbushia Daraja la Mto Ruhuhu ambalo

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. PINDI H. CHANA]

tukishaunganisha pale Mikoa hii miwili inakuwa ni rahisi sana. Wakija Viongozi kwenye ziara Mkoa wa Njombe wanaunganisha tu pale kwenye Jimbo la Captain Komba, Mwalimu wangu, wanaunganisha kwenda Ruvuma, wamemaliza kazi; kuliko utoke tena Ludewa, uje mpaka Njombe uanze *round* nyingine kuelekea Ruvuma, ghamama ni kubwa, watatumia mafuta mengi, muda na siku hizi tunaambiwa muda ni fedha, *time is money*, kwa hiyo, ningombwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi *point* tunazozisema siwaoni Wataalamu wetu kama wapo humu ndani wanazichukua labda kama wanaangalia kwenye TV, lakini naiomba sana Serikali kwamba, Wataalamu ni lazima wawepo hapa Bungeni wahakikishe wanachukua kila kitu na *Hansard* ili kuona *a way forward* na mipango ya muda mrefu. Kwa hiyo, barabara hii ni muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya hizi za Mkoa wa Njombe, Wilaya ya Makete, Wilaya ya Ludewa ni wazalishaji wazuri sana wa mahindi, lakini kutokana na barabara tunategemea mnunuzi mmoja tu wa mahindi ambaye ni Serikali (*SGR*), kwa sababu wafanyabiashara binafsi kutokana na barabara hawafiki kununua mahindi maeneo haya. Kungekuwa na barabara za lami hata masoko ya mahindi tunayolima kwa wingi, hadi leo yapo mengi, ingekuwa ni rahisi sana, tunapata bei nzuri ya mahindi, lakini leo hii tunaitegemea Serikali peke yake; wanaita *SGR* pale Makambako ndiyo ikanunue mahindi, wafanyabiashara wengi wanaishia maeneo ambayo kuna lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kwa niaba ya Wananchi wa Mkoa wa Njombe, hususan Wilaya hii ya Ludewa pamoja na Makete, lakini Barabara ya Makete natoa shukrani za dhati imejengwa vizuri, bado maeneo machache. Barabara hizi ningombwa sana zizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Ludewa pamoja na uzalishaji mkubwa tunalisha nchi nzima mahindi, pia ina madini ya chuma na makaa ya mawe. Madini haya ni

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. PINDI H. CHANA]*

lazima yasafirishwe kwenye barabara za uhakika, bila barabara miundombinu sahihi itakuwa bado ni changamoto kubwa. Ninaomba pia katika mipango ya muda mrefu tujenge reli inayotoka pale inaunganisha hadi Makambako kwenye Jimbo la Mheshimiwa Deo Sanga, *Jah People*, itasaidia sana kubeba madini haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba katika *Long Term Plan* masuala ya reli yafikiriwe. Vinginevyo, tutakuwa tunaweka mara kwa mara kwenye mipango yetu, *Vision 2025*, kwenye *Long Term Plan*, lakini utekelezaji wake unakwenda polepole. Kwa hiyo, ningeomba sana barabara hii pamoja na daraja hili la Mto Ruhuhu, ambalo litasaidia mawasiliano katika Kata ya Ruhuhu, Masasi, Mkomping'ombe, Ludewa unakuja mpaka Wilaya ya Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hii nizungumzie pia Barabara za Dar es Salaam. Dar es Salaam pale ni pa wote, watu tuna Mikoa yetu, lakini Dar es Salaam pale ni pa wote, lazima tupite Dar es Salaam. Dar es Salaam msongamano umekuwa mkubwa, lakini mimi nina jambo moja; kwa nini *exit* ya kutoka Dar es Salaam kwenda Mikoa mingine yote ipo moja tu Ubungo?

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi juzi hapa pale Ruvu kuna gari lilitondoka likaziba, yaani kulikuwa kuna foleni inafika mpaka Chalinze, kwa sababu hakuna njia nyngine ya kuingia Dar es Salaam zaidi ya Ruvu. Watu wengine walikuwa wanajaribu kuzunguka Bagamoyo, ambayo ni changamoto kubwa. Lazima tubuni njia za kuingia Mkoa wa Dar es Salaam isibakie njia moja tu maana vinginevyo ikisha-*block* Kibaha, ikisha-*block* Ruvu inabidi utumie ndege au usubiri mpaka kile kilicho-*block* kiwe *unblocked*. Watanzania wote milioni 43 tunaliona hilo na Wataalamu wetu tunaliona hilo, lakini ni lazima tupate kitu kinaitwa *break through*. Haiwezekani mji mkubwa kama Dar es Salaam barabara ya kuingilia ni moja tu, hata kama mtu anakuvizia anakusubiri tu Ubungo pale maana hamna njia nyngine, atafika tu hapa Ubungo. Lazima tubuni njia za

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. PINDI H. CHANA]

kuingilia Dar es Salaam ziwe kadhaa kushoto, kulia, watu waweze kuingia katika Jiji letu la Dar es Salaam. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeomba sana, hii ni mara ya pili ninalizungumzia jambo hili, ningeomba tutape ufanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kwenye kipengele cha barabara, mawasiliano; wakati tunaelekeea *Christmass* na Mwaka Mpya mara nyingi sana usafiri wa Wananchi wetu huwa unapanda, kwa hiyo, hapa naizungumzia *SUMATRA* ambayo lengo lake ni kudhibiti usalama na usafiri barabarani. *SUMATRA* watusaidie, wale wawakilishi wetu nyakati za *Christmass* na Pasaka wanasaferi sana, tunaomba nauli zisipande hata nukta moja. Tunaomba mawakala wasitumike maana ofisi zinajulikana, lakini hawa *SUMATRA* wamekuwa sana katika Mikoa kama Dar es Salaam, katikati ya Mikoa, kule vijijini nauli kutoka *point* moja kwenda *point* nyingine nyakati za mvua, nauli zinapandishwa sana hovyohovyo. Hawa *SUMATRA* kule vijijini ni lazima waonekane kudhibiti hizi nauli kupanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mawasiliano ni muhimu sana. Nchi za wenzetu, kama nilliyosema juzi, nimepata bahati ya kutembelea nchi kadhaa hivi karibuni, Kenya, Ghana, India na pia bado nina nafasi ya kwenda nchi nyingine hivi karibuni mara nitakapomaliza Bunge. Nchi za wenzetu mawasiliano yako *very clear*. Sasa hivi wameenda hadi kwenye hatua inaitwa ya *Wi-Fi*; yaani mtu yuko kwenye basi ana *Google*, nadhani wale Wataalamu mnaelewa ninachomaanisha, anatumia *internet*, lakini sisi kwetu ukifika Mikumi tu kwenda llula hakuna mawasiliano, hakuna *Voda*, hakuna *tiGO*, hakuna *Celtel*. Wale ndugu zangu Wanyalukolo wa Mbeya, Ruvuma, kote wanajua. Kuna maeneo makubwa muhimu hayana mawasiliano hata ya simu tu, achana na hiyo *internet* hata ya simu; kweli kizazi hiki cha *dot com* mawasiliano ya simu kwenye barabara kubwa, maeneo makubwa, hii changamoto inatoka wapi, si kuweka mnara tu pale?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. PINDI H. CHANA]

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kitu cha kuweka mnara mawasiliano yanaendelea maana kukiwa na mawasiliano watu watazungumzia familia, watazungumzia biashara, mzunguko wa pesa utakuwa mkubwa, *TRA* wanapata faida, maisha bora kwa kila Mtanzania, tunapunguza umaskini na kadhalika.

Suala la mawasiliano ni muhimu, kwenye barabara hizi kubwa kuna *emergency*nyingi, mawasiliano mengi; eneo la Mikumi hadi Ilula kuna eneo linaitwa Ruaha Mbuyuni, unashindwaje pale kuweka mnara mawasiliano yakawepo? Pamoja na maeneo mengine, kwa mfano, unakuta kuna eneo kama kule Ludewa eneo la Mwambao, Kata za Manda, Kata ya Lupingu, nako mawasiliano ni changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile maeneo yale wanatumia sana usafiri wa meli. Zile meli zikifika kule eneo la Mwambao wa Wilaya ya Ludewa na Nyasa hakuna gati, akina mama wanapanda meli kwa kudumbukia kwenye maji, inawekwa ngazi ndiyo wanapanda. Lazima kuwe na gati, meli ikifika watu washuke vizuri kwa usalama. Ningeomba sana maeneo haya yazingatiwe kwa kiasi kikubwa; maeneo ambayo hayana mawasiliano kwenye barabara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la mizani ....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Pindi Chana. Mheshimiwa Deo Sanga!

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa na mimi nafasi nichangie. Kabla sijachangia, naomba nitoe pole kwa janga

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. DEO K. SANGA]

lililotokea jana katika Mji wangu wa Makambako na hususan katika eneo la Magegele, kuna Shule yetu ya Msingi, jana kupitia shoti ya umeme madarasa yote yaliungua na mabweni. Shule hii inaitwa Siglip. Kwa hiyo, nawapeni pole sana ndugu zangu wa Makambako. Nachukua nafasi hii kuwashukuru wale wote waliofanya kazi ya kuokoa mabweni haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu Zimamoto jana ilitoka Njombe ilipofika mabweni tayari yalikuwa yameshaungua. Tuna gari pale lilihakuja siku nyingi, liliipata ajali na limeshatengenezwa lipo gereji lipo tayari. Serikali haijalipa hela ili gari lile lianze kufanya kazi iliyokusudiwa. Ombi langu kwa Serikali, naiomba ikalipe deni ambalo gari lile limeshatengenezwa lipo tayari, hili lingeweza kuokoa janga ambalo jana lilikuwa kubwa katika Mji wa Makambako.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niingine kuishukuru Serikali kwa namna ambavyo imekuwa ikifanya kazi nzuri, hususan Mawaziri watatu ambao wamewasilisha hoja hii. Nianze na barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali, barabara sehemu nyingi sasa zinapitika baina ya Kijiji na Kijiji na Barabara Kuu na kadhalika. Kuna barabara kuu ambayo ilikuwa inatengenezwa ya kutoka Dar es Salaam kwenda Tunduma, imeshatengenezwa kutoka lyofi kipande kile mpaka Iringa, kutoka Iringa mpaka Mafinga, ombi langu kwa Serikali, tunaomba barabara sasa ya kutoka Mafinga kwenda Igawa iweze nayo kuingizwa kwenye mpango wa kutengenezwa ili barabara hii ya *Highway* iwe nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu lingine kuhusu barabara; Mheshimiwa Rais alipokuja juzi katika Mkoa wetu wa Njombe, naishukuru Serikali kwa kutupa fedha za kufanya kazi ya upembusi yakinifu katika Barabara ya kutoka Njombe hadi Lupembe. Barabara hii upembusi yakinifu utakamilika mwezi wa tatu. Ombi langu, Mheshimiwa Rais, alituahidi kwamba, barabara hii itaingizwa kwenye bajeti

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. DEO K. SANGA]

ya 2014/2015 ili iweze kutengenezwa lami. Kwa hiyo, niwaombe sana jambo hili litekelezwe kwa sababu kule kuna uchumi mkubwa wa chai, mbao na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie suala la umeme. Naishukuru pia Serikali kwa namna ambavyo sasa imeweza kutusogezea huduma za umeme katika nchi hii na hususan katika Jimbo langu.

Suala la umeme katika Mji wangu wa Makambako, kuna eneo moja lina kama nusu kilometra tu kutoka pale mjini katika Kata ya Mji Mwema unapokwenda Mashujaa, kunaitwa Ikwete B, ni nusu kilometra tu na hawana umeme pale na wanaishi katika Mji huohuo wa Makambako. Ombi langu kwa Serikali, naomba sana na Naibu Waziri ananisikia hapa kwamba, eneo hili lipatiwe umeme kama ambavyo watu wengine wamepata. Eneo hili ndiyo lile ambalo Naibu Waziri ulipita wakati ule, hawa watu wa MCC wameshatengeneza miundombinu, ombi langu, wameshafunga *transformer*, Mradi huu haujakabidhiwa ili umeme huu uweze kuwashwa na Kitongoji hiki ambacho nimesema ni nusu kilometra kutoka pale walipoishia MCC waweze kupata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mradi huu mkubwa ambaao ulikuwa unatoka Makambako kwenda Songea, ambaao mlituahidi kwamba, ungeanza mwezi Oktoba na sasa ni Desemba, ambaao ulikuwa unapitia katika Kata yangu ya Lyamkena, Igongolo, Kichiwa, Tagamenda na Namatembwé. Ombi langu ni lini Mradi huu utaanza ili Wananchi wawe na imani kama ambavyo mlipita mkawaambia Oktoba shughuli hii ingweza kuanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii nizungumzie Reli ya TAZARA; namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, amefanya kazi kubwa nzuri na tunamwombea sana aendelee na kazi hii. Ombi langu sasa ili TAZARA hii irudi iwe kama zamani inamilikiwa na Serikali mbili, Serikali ya Tanzania na Zambia, hivi kuna tatizo gani kuwarudisha tena Wachina waweze kusimamia reli hii?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. DEO K. SANGA]*

Tatizo liko wapi ili kusudi shughuli hii ya Reli ya Uhuru ya TAZARA, maana ilikuwa inaitwa Reli ya Uhuru ya TAZARA, iwe kama zamani?

Mheshimiwa Naibu Spika, maana sasa pamoja na Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, kujitahidi amefanya kazi nzuri sana, lakini bado inasuasua. Kama ambavyo mchana wenzangu wamechangia kwamba, ni kwa nini tusiepukane tuwe tunaimiliki sisi wenyewe Watanzania badala ya hivi sasa inamiliikiwa na Zambia?

Mheshimiwa Naibu Spika, mawasiliano; katika Jimbo langu tunaishukuru Serikali kuna mawasiliano mazuri, lakini yako maeneo ambayo mawasiliano hakuna. Nilisema kipindi kile cha mwaka jana, mwaka huu mwanzoni nimesema kwamba, kuna Kata moja inaitwa Ikondo na Kijiji cha Ikondo kuna umeme kule tangu enzi upo, siyo huu wa *Grid'ya Taifa*, upo umeme pale ambao watu wa *SEFA* walishauweka. Tatizo kubwa kule kuna wakulima wakubwa sana ambao wanalima, kuna mazao ya maharage, mahindi, mananasi na kadhalika. Tatizo hawa watu wanakosa mawasiliano, wanapotaka kufanya mawasiliano ili kupata soko, wamekuwa wakati fulani wakipanda kwenye miti, wameshadondoka watu zaidi ya saba kule, wengine wamevunjika viuno, nitakosa kura mwenzenu kule. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana ili watu hawa tuwaokoe wasivunjike viuno ni vizuri tupeleke mawasiliano. Naomba sana Waziri wa Mawasiliano, tuhakikishe tunapeleka mawasiliano katika Kata hii ya Ikondo na Kijiji cha Ikondo. Umeme upo wa kutosha kabisa wa siku nydingi. Kwa hiyo, ombi langu ni kuwaokoa watu hawa ili wasiweze kudondoka kila wakati wanapopanda kwenye miti na miti sasa kule imeshakwisha kwa sababu wanapanda imekwisha kwa kudondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungumzia suala la *SUMATRA*. Ombi langu, suala la *SUMATRA* limekuwepo katika Mikoa mbalimbali. Sisi Mkoa wa Njombe, Wananchi wetu pale wanapotaka kwenda kupata *sticker* ni lazima

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. DEO K. SANGAJ]

waende Mbeya au Iringa wakati Njombe tumeshapata Mkoa. Kwa hiyo, naomba sana watu wanatoka Makete, Ludewa na Njombe yenyewe wanapata tabu. Kilometra za kutoka Njombe kwenda Mbeya ni sawasawa na unapotoka Njombe kwenda Iringa, sasa ni kwa nini tusiweke Mkoani pale Njombe kuwaokoa watu hawa wasipate gharama wanapokwenda kufuata *SUMATRA* kule Mbeya? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata *TIN Number* wanakwenda Mbeya badala ya Njombe pale, hata *Road Licence* wanakwenda Mbeya badala ya Njombe pale. Kwa hiyo, ombi langu kwa Serikali, naomba sana tusogeze huduma hii katika Mkoa wetu wa Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, mtu anapofanya vizuri ni lazima tuseme. Dar es Salaam siku moja na mimi baada ya kuona msongamano nikasema dereva wangu hebu *park* pembeni, nilipanda treni. Kazi ile uliyobuni ni nzuri, endelea kubuni ili treni ile iweze kufika sasa mpaka Kibaha. Kazi ni nzuri sana, imepunguza baadhi ya msongamano kwa kweli, bila ile nadhani msongamano ungekuwa mkubwa sana. Tunakuombea maisha marefu ili uweze kufanya kazi nzuri uliyopangiwa na Serikali ya Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, sikupenda kulisema naomba niliseme, nilisema na mwaka jana, Wabunge wenzangu tujenge upendo na mshikamano na tuombe sana. Nilisema hata wakati ule wamo Wachungaji humu, wamo Masheikh humu, mtuombee tujenge kupendana ili kuongoza nchi hii kwa pamoja, tuache malumbano ya kutukanana na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, baada ya marekebisho haya naunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana sana Mheshimiwa Deo Sanga, *Jah People*, kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Aeshi kwa dakika tano, atafuatia Mheshimiwa Mgimwa kwa dakika tano. Mheshimiwa Aeshi!

**MHE. AESHI K. HILALY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi angalau dakika tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba niwape pole Wananchi wa Jimbo langu hususani Kata yangu ya Kasinze na Jumapili nitakuwa kule tuungane kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka haraka tunitakwenda kwenye masuala ya umeme. Naomba niwashukuru Mawaziri wote, kwa kazi nzuri wanayofanya Waziri na Naibu wake. Sina lingine la kuwashukuru zaidi ya mliyotutendea ndani ya Jimbo langu la Sumbawanga Mjini. Mheshimiwa Waziri, tumepata vijihi vingi lakini viro pembezoni mwa barabara. Ningekuomba Mheshimiwa Waziri kwamba, kutoka barabarani kwenda nje kidogo ya barabara kama kilometra tano kuna vijiji vikubwa zaidi kuliko vile ambavyo vinapewa umeme, nakuomba tuwakumbuke na wale wengine ili tuweze kuleta maendeleo zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye suala la barabara. Naomba niwashukuru sana na kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri hawa kwa kufanya kazi nzito. Natoa ushauri kwamba, barabara ya Sumbawanga kutoka Tunduma kwenda Sumbawanga inayojengwa kwa kiwango cha lami inapita Sumbawanga Mjini. Ninaliona tatizo linaloweza kutukuta sisi ni lile linalowakibili watu wa Mbeya, sasa hivi Mbeya kuna foleni kubwa sana. Namwomba Mheshimiwa Waziri Magufuli na Naibu Waziri wake, kwa sababu tuna wakandarasi pale wanajenga barabara kwa nini wasiongeze fedha tukajenga *two way* moja kwa moja?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. AESHI K. HILALY]

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii napata shida kutoka Sumbawanga kwenda Mbeya, kitendo cha kufika Mbeya kwenye ile foleni unapita saa mbili, tatu, kuingia Mbeya Mjini. Naiomba sasa Wizara hii ya Ujenzi, Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, ongezeni fedha kidogo wakandarasi wale tulionao watujengee moja kwa moja *two way* kuliko baada ya miaka kumi tuivunje barabara ile na tuijenge upya. Katika barabara ni hili lakini Mheshimiwa Waziri nakuomba tena kwamba, barabara zile zinajengwa sasa zinaenda vizuri, waongezeeni fedha zimalizike kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, ninakwenda moja kwa moja kwenye masuala ya miundombini. Tumeongelea sana suala la reli, wamesahau kama kuna Ziwa Tanganyika na Ziwa Rukwa. Nitazungumzia leo Ziwa Tanganyika kwa sababu inagusa Mkoa wa Rukwa, Katavi na Mkoa wa Kigoma. Tumeisahau meli hii, nakumbuka wakati tunakua Meli ya Liamba ilikuwa inatembea kwa wiki mara moja, ndani ya mwezi inatembea mara nne na abiria walikuwa wanajaa mapaka wanakosa nafasi. Mheshimiwa Serukamba amezaliwa Kigoma na ndio Mwenyekiti, meli hii sasa hivi inatembea mara mbili kwa mwezi nini tatizo, watu wamekufa, watu wamepungua au barabara imejengwa kandokando mwa Ziwa Tanganyika kutoka Kasanga kwenda mpaka Kigoma? Tatizo hapa ni wizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiingia ndani ya Meli ya Liemba kila mtu ana watu wake, *77*ana watu wake, kapteni ana watu wake, kwa hiyo, watoa huduma wote ndani ya ile Meli wana watu wao. *77*akianza kazi akienda kudai tiketi anauliza mimi wa fulani, mimi wa fulani, gharama ni kubwa kuliko mapato. Mheshimiwa Waziri, Mwenyekiti wa Bodi, Mheshimiwa Peter Serukamba, nakuomba, wapo watu wanataka kuiendesha Meli ile kwa kugharamia kukusanya nauli tu, wanaweza kukusanya mapato kama mawakala wengine wanaokusanya katika Halmashauri zetu kukusanya fedha zinazotakiwa kupatikana ndani ya Meli ile. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kila Kiongozi ndani ya Meli ile ana kituo cha mafuta ndani ya Mwambao. Wale ndio

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. AESHI K. HILALY]

wezi wanaiba, matokeo yake inaonekena gharama kubwa kuliko mapato. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, tuko radhi kuchangia mafuta ya tripu mbili na tukasimamia sisi wenyewe tuone mapato yanayopatikana, ni makubwa sana lakini wezi ni wengi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, watu wanakufa, watu wanazama kwenye maboti yale ya mba, watu wananyesewa na mvua saa 12, ifike wakati tuiangalie Meli hii. Miaka mitano iliyopita tulikuwa tunatembeza Meli mbili kwa wiki, Liemba na Mwongozo; nini kimetokea leo wizi! Mheshimiwa tuwe makini sana katika hili. Mimi nipo tayari waunde kamati na mimi niongozane nao na wapo tayari wameshakubali kutoa gharama za mafuta tripu mbili za Meli ambayo gharama zake kama millioni 40 hivi wapo tayari kutoa ili tuangalie ukweli uko wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nakwenda kwenye Wizara ya Mawasiliano. Nilitaka nihoji tu Wizara hii imeisahau Kampuni ya *TTCL*; sijawahi kuona tangu miaka mitano iliyopita tangazo hata moja la *TTCL mobile* tatizo nini? Nini kinachowashinda kuifufua Kampuni hii ya *TTCL*?

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kulifuatilia hili hivi tatizo ni nini? Ninafikiri kuna rushwa kubwa sana pale. Haya Makampuni mengine wanawahonga *TTCL* ili wasifanye matangazo, matokeo yake *TTCL* imekufa, *TTCL* ipo kila sehemu kila Wilaya, kila kona, lakini hakuna hata siku moja Wananchi hata Wabunge hapa hawatumii *TTCL* na wana Maofisi mazuri, wana kila kitu, tatizo lipo wapi? Mheshimiwa Waziri wa Sanyansi na Mawasiliano tunawaomba mlifuatilie hili na mtupe majibu tatizo ni nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nawaomba Wabunge wote tuheshimiane, tunadhalilishana hapa, tunavunja heshima yetu, tunavunja utu wetu. Zamani ukimwona Mheshimiwa Kimiti unatetemeka, lakini leo tumejishushia thamani sisi wenyewe tunaonekana watu wa ajabu. Nawaomba sana ifike wakati tujenge kauli nzuri,

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. AESHI K. HILALY]

tuheshimiane wenyewe kwa wenyewe na tupendane.  
(*Makofifi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, dakika tano zimekwisha, naomba nikushukuru sana, ahsante sana. (*Makofifi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Aeshi, kwa uungwana na kwa nasaha ulizotupatia. Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, dakika tano!

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia eneo hili muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijachangia, naomba nichukue fursa hii kuwapa pole Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Iringa, Jesca Msabatavangu pamoja na Wana-CCM wenzangu, kwa kufiwa na Katibu wetu, Emmanuel Mtanu'ngombe jana. Mungu ailaze pema roho ya marehemu; amina.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kuwapongeza sana Wenyeviti wenzangu kwa jinsi walivyowasilisha Ripoti zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu nitajielekeza katika sehemu tatu; eneo la kwanza ni la nishati na madini. Mara nyingi Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini amekuwa anatauhidi kwamba, kutakuwa na umeme. Naomba jambo hili analoliahidi alitekeleze kwa dhati kwa sababu tayari kumeshaanza kutokea mgao wa umeme katika nchi yetu. Unapotokea mgao wa umeme unadhoofisha sana ukuaji wa uchumi wetu na unaviangamiza sana viwanda vyetu. Wazalishaji wengi wanapata harasa sana katika maeneo yao kwa sababu umeme unapokatika ghafla wanapata hasara na kunakuwa hakuna mtu wa kuwafidia harasa hizo kwa sababu *TANESCO* hawana uwezo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWAJ]

Namshauri Mheshimiwa Waziri, aangalie maeneo mengine; kuna Makaa ya Mawe ya Ngaka, kuna Kiwira na Mchuchuma. Eneo hili kama Serikali itaamua kulifanyia kazi, umeme wake utakuwa rahisi kuliko eneo lingine lolote. Cha kusikitisha sana, tunaendelea kujikita kutumia umeme wa mafuta ambao ni ghali sana ambao unasababisha hali ya uchumi wetu kuendelea kuwa mbaya, kwa sababu gharama ya umeme inapokuwa juu ina maana *cost* za *production* katika viwanda inaongezeka, kwa hiyo, *inflation* inazidi kuongezeka katika nchi yetu. Kupatikana kwa umeme katika maeneo haya hakuhitaji fedha nyingi sana, kwa mfano, tulihitaji kujenga *transition line* kutoka Makambako mpaka Songea ambayo ilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 64, tungeweza tukapeleka kwenye Gridi ya Taifa MG 200 ya KW 220. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna sababu ya kutoangalia eneo hili na wenzetu Sweden walishakubali kutupa mkopo na walikubali kutusaidia katika eneo hili na kuna baadhi ya Mashirika ya Serikali, *PSPF, NSSF*, walikuwa tayari kutuunga mkono katika maeneo haya. Kwa hiyo, Serikali tusiendelee ku-*concentrate* na kushughulikia umeme wa mafuta, umeme wa mafuta unauzwa kwa senti 43 na umeme huu unauzwa kwa senti kumi, kwa hiyo, tuijangalie kwenye jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tuna umeme wa Singida wa upepo ambao unaweza ku-*produce* MG 120. Mheshimiwa Waziri, naomba uliangalie eneo hili. Eneo la umeme ni *very sensitive* kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka kuchangia ni suala la meme katika Tarafa yangu ya Kibengu. Kwa namna ya kipekee, naomba nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri, baada ya kilio cha muda mrefu *at least* hata sasa kwenye makaratsi tumeanza kuona mmekusudia kupeleka umeme katika maeneo yale. Wananchi wa maeneo yale walikuwa *very bitter* kwa sababu wao ndiyo wanahifadhi vyanzo vya Mto Kihansi,

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MAHMOUD H. MGIMWA]

kwa hiyo, tunawashukuru sana kwa hilo, naomba nikupongeze kwa hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba pamoja na pongezi ninazozitoa, kuna kijiji kimoja katika zile Tarafa 16 mmeorodhesha vijiji 15 vitapata umeme, lakini mmekisahau Kijiji cha Igomtwa, naomba nacho mkiingize.

Eneo lingine la umeme ni Tarafa ya Ifwagi. Tarafa ya Ifwagi ni kweli tumepata umeme karibu vijiji vyote, lakini kuna vijiji viwili tumevisahau; kuna Kijiji cha Mtikilwa na Kijiji cha Ikongosi. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha atueleze atatusaidiaje umeme katika maeneo haya.

Eneo lingine nililokuwa nataka kumshauri Mheshimiwa Waziri, Watanzania wanataka washiriki katika uchumi wa nchi yao kwa kutumia rasillimali zao wenyewe. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, hata sisi Watanzania, tuna haki ya kushiriki asilimia 100. Kwa hiyo, kauli ambazo zinakwenda zinatumiza, atusaidie kwenye eneo hili. Watanzania tunayo haki ya kumiliki uchumi wetu na tuna uwezo wa kumiliki uchumi wetu, Serikali inatakiwa iwasaidie Watanzania, tusiwavunje moyo tuwasaidie katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ninalotaka kuchangia ni la barabara. Kwa namna ya pekee nataka niipongeze sana Serikali, imefanya kazi nzuri sana katika sehemu ya barabara, hakuna mtu ambaye hajui kuwa tumefanya vizuri katika barabara katika Afrika Mashariki hakuna Nchi ambayo inaweza kutufikia. Katika llani ya Uchaguzi mwaka 2005 na llani ya Uchaguzi ya mwaka 2010, ilionesa kwamba Serikali itatengeneneza barabara Kinyanambolei, kupitia Sadali ... (*Kicheko*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mahmoud, dakika tano ni kidogo sana, nakushukuru kwa mchango wako. Sasa tuelekee kwenye uchangiaji wa Waheshimiwa

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[NAIBU SPIKA]

Mawaziri na atakaetufungulia upande huo ni Naibu Waziri wa Madini, atafuatiwa na Naibu Waziri wa Nishati. Mheshimiwa Masele, dakika kumi!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa ufanuzi kwa baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, pamoja na Kamati ya Nishati ya Madini. Awali ya yote, naomba kuwashukuru na kuwapongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Madini, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa pamoja na Timu yake nzima ya Kamati, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusimamia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pamoja na Waheshimiwa Wabunge wamechangia kuhusu eneo la wafanyakazi kwamba, Mashirikia yetu yana upungufu wa wafanyakazi ambao ingepaswa waajiriwe waweze kusimamia uendelezaji wa shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili tumelifanyia kazi kwa karibu na tunaishukuru sana Kamati kwa kutusaidia kuweza kuharakisha zoezi hili na hivi sasa tumeweza kupata *approval* kutoka kwa *Treasury Registrar* pamoja na Ofisi ya Rais (Utumishi) na Mashirika yetu ikianza na *TPDC*, tayari imepata *approval* ya kuajiri wafanyakazi 187, ambao hawa watafanya kazi pamoja na Wachina wanaojenga bomba la gesi kutoka Mtwara kuja Dar es Salaam. Pia kuna wafanyakazi wengine 39 hao watafanya kazi katika Ofisi ya Makao Makuu ya *TPDC*. Shirika letu lingine la *STAMICO* pia limepata *approval* kutoka Ofisi ya Rais (Utumishi) na jumla ya wafanyakazi 100 wataajiriwa. Zoezi hili linaendelea, baadhi wameshafanyiwa *interview* na wengine tayari wameshapata *offer letter*. Wakala wetu wa *TMAA* pia imepata jumla ya wafanyakazi 48, wanaendelea na zoezi la *interview* na wengine wameitwa kuripoti ofisini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika michango ya Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Dkt. Kafumu, alizungumzia kuhusiana na Kamishna wa Madini kwamba,

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI]*

nafasi ile imekuwa wazi muda mrefu na anayeshikilia anakaimu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Serikali zoezi hilo limeshafanyika tayari majina yameshapendekezwa na kilichobakia tu ni mamlaka ya Rais ambayo inayafanya kazi majina yale ili yaweze kuthibitishwa na hatimaye tutapata Kamishna wa Madini. Zoezi hilo linaendelea vizuri, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kazi hiyo inafanyika kwa kufuata taratibu zikiwemo za *vetting* na hatimaye kupata Kamishna.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Kafumu amezungumzia uwepo wa Mamlaka ya *TMAA* kwamba, mamlaka hii shughuli zake zinaingiliana pamoja na shughuli za *TRA* na mamlaka ya Kamishna wa Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala hii ilianzishwa chini ya Sheria ya *Executive Agencyya* Mwaka 1997 na kufanyiwa marekebisho mwaka 2009 kwa lengo la kuchukua nafasi ya iliyokuwa Kampuni ya *Alex Stewart* ambayo ilikuwa ikifanya kazi ya kukagua Migodi hii, ambayo ilianzishwa miaka ya 1990, mwishoni ili kuhakikisha Serikali inapata mapato na kuchunguza shughuli za uendeshaji wa Migodi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala hii ilipoanzishwa, ilianzishwa kwa kazi maalumu. Inafanya *Special Audit* za Madini, ikiwemo *ku-test samples* na kujua kiwango cha madini kilichopo katika mchanga ambaao unazalishwa katika migodi mbalimbali. Kazi hizi zinapaswa kufanywa na watu ambaao tayari wana ujuzi katika migodi mbalimbali. Kazi hizi zinapaswa kufanywa na watu ambaao wana ujuzi katika Sekta hii ya Madini, ama wenyewe utaalamu wa mambo ya madini kwa maana ya Wanajiolojia na *Engineers waliosomea* masuala ya miamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchakato huu, itakumbukwa kuwa wakati Kampuni ya *Alex Stewart* ipo, Serikali ikuwa inatapa hasara kubwa sana za kuwalipa, zaidi

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI]*

ya Bilioni 1.2 ilikuwa ikilipwa Kampuni hiyo kwa mwaka. Bunge hili hili lilipitisha kwa makusudi kabisa kuanzisha Wakala hii kwa lengo la kuwa jicho la Serikali kuhakikisha kwamba, nchi yetu inaendelea kunufaika na hatupunjwi katika shughuli zote za Migodi na Serikali inapata kodi na malipo mbalimbali inayostahili kulingana na shughuli zinavyendeshwa. Bahati nzuri ndugu yangu Kafumu alikuwepo pale kama Kamishna, kwa hiyo, alishiriki kikamilifu katika mchakato huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la kodi, Mheshimiwa Barwany alichangia jana na Waheshimiwa wengine, imekuwa ni kawaida kwa Waheshimiwa Wabunge kulalamika kwamba tunapoteza, migodi hailipi kodi. Naomba niliweke wazi, Kamati ama Tume ya Bomani ilioundwa na Mheshimiwa Rais mwaka 2007 na baadhi ya Wabunge wakiwa Wajumbe, Tume ile illifanya kazi kubwa ya kubaini upungufu uliokuwepo kwenye Sekta ya Madini. Bunge hili kwa kushirikiana na Tume ile liliweza kutunga Sera ya Madini ya 2009, ambayo ilikuwa ni maboresho ya Sera iliyopita. Pia mkatunga Sheria ya Madini ya 2010 ambayo ilikuwa pia ni maboresho ya Sheria ya Madini iliyopita ili kuondoa upungufu ambaa ulikuwepo kwenye Sheria zilizopita. Sasa kazi hiyo imefanyika na ninawaomba sana Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania kwa ujumla, isiwe ni *perception* tu kwamba tunaibiwa, lakini Sheria imetungwa na Serikali inasimamia kikamilifu kuhakikisha tunapata kile tunachostahili. Kwa mfano, Mheshimiwa Barwany alizungumzia mikataba, ni rahisi sana kusema mikataba mibovu, mikataba mibovu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuhakikishie mikataba ile kwa kiwango kikubwa imerekebishwa, upungufu tunaendelea kuushughulikia kuurekebisha chini ya mazungumzo pamoja na Makampuni yale ili ule ambaa tumeubaini na ambaa Sheria Mpya mliyotunga Waheshimiwa Wabunge imeubaini, tuweze kuurekebisha. Hivi sasa tunajadili na tumekamilisha Mkataba wa *Uranium*. Katika mkataba ule kwa mara ya kwanza Wizara imeweza kusimamia kuhakikisha hakuna misamaha ya kodi. (*Makofi*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI - MHE. STEPHEN J. MASELE]*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mikataba hii hakuna kificho, mikataba iko wazi yejote anayetaka kuona mikataba hii, anaweza kufika Wizara ya Nishati na Madini anaweza kupata na kusoma mikata ile. Maana ya uwazi siyo kuiweka mikataba kwenye magazeti, maana ya uwazi ni namna gani Wabunge au mwananchi anaweza akaifikia na kuiona mikataba hiyo kwa taratibu zilizopo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya uchimbaji imekuwa ni kilio cha Wabunge wengi na niseme ukweli kwamba maeneo mengi yanayotengwa ni yale ambayo unakuta mengine hayana madini yanayotosheleza na wachimbaji wadogo bahati nzuri wanafahamu maeneo ya madini yalipo na sehemu zenyenye mashapu mengi.

Serikali inaendelea kufanya zoezi la kufuta leseni zote ambazo hazifanyi kazi na hili tunalfanya kuisaidia nchi. Tunalfanya kwa mujibu wa sheria na matakwa ya sheria, hatufanyi kwa sababu tunataka kumwonea mtu ama kwa sababu una shida na mtu fulani. Haya ni matakwa ya sheria ambayo imetungwa. Ukichukua Leseni ya Utafiti ni miaka minne, uki-renew miaka mitatu, uki-renew mara ya mwisho miaka miwili. Kama hujafanya chochote kwa mujibu wa sheria, Waziri ama Kamishina wa Madini ana uwezo wa kuifuta ile leseni kwa kufuata taratibu na ndiyo tunachokifanya. Kwa hiyo, tunavyoendelea kufuta hizi leseni asitokee mtu akadhani kwamba watu hawampendi, ama Serikali haipendi wazawa, lakini tunafanya hivi kwa matakwa ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati alizungumzia kuhusiana na kurudishwa kwa mlima wa Kabulo. Zoezi hilo linaendelea, tumeshatoa barua ya kuwataka wajieleze kwanini wameshindwa kuendeleza na kwa mujibu wa sheria eneo lile pia litarudishwa Serikalini kama watashindwa kukidhi mahitaji yote ya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kidogo kuhusiana na suala la Nzega. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Kigwangalla kwa uugwana wake. Kwa kweli hakuna mtu mwingine yejote anayeweza akajivunia mafanikio ambayo

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI - MHE. STEPHEN J. MASELE]*

wameyapata Nzega. Kama leo wanazungumzia Shilingi bilioni tatu ni jitihada ambazo Mheshimiwa Kigwangalla amezifanya kwa kushirikiana na Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wa Nzega wanapata Shilingi bilioni tatu zao. Kwa hiyo, mipango yote ambayo wanaipanga kufanya matumizi ya fedha zile ni mipango halali na fedha zile wamezipata kihalali. Lakini ukisema kwamba Mheshimiwa ameziweka kwenye akaunti yake, siyo kweli. Barua iliyotoka Halmashauri ya Nzega kwenda kwenye mgodi wa *Resolt* na kuja kwetu Wizarani ni barua ilioandikwa na Mkurugenzi na kusainiwa na Mkurugenzi na ikiwa akaunti za Serikali kwa maana ya Halmashauri ya Wilaya ya Nzega. (*Makofii*)

Kwa hiyo, binafsi nachukua nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Nzega kwa kuwa na uwakilishi mzuri na nimwahidi tu Mheshimiwa Kigwangalla kwamba maombi yake aliyoyaomba tutaendelea kuyasimamia kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata haki yao na wananchi wa Nzega ambao walipisha mgodi ule, wanapata haki yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa George Simbachawene.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nami nichukue nafasi hii kuishukuru sana Kamati ya Nishati na Madini inayoongozwa na Mheshimiwa Mambalaswa kama Mwenyekiti na Mheshimiwa Bwanausi wakisaidiana na Wajumbe wengine akiwepo mama yetu mpendwa Mheshimiwa mama Anne Kilango Malecela. Tunawashukuru sana wote kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi nina hoja kama nne, lakini kwa kweli niwashukuru sana Wabunge wote kwa ujumla kwa michango mizuri ambayo imetolewa kwa Wizara yetu.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)]  
utaona michango hiyo ni mingi, kabrasha hili lote ni michango ya Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge kwa michango mingi na mizuri ambayo inaisaidia Wizara yetu. Tutaendelea kusaidiana chini ya ulezi wa Kamati hii makini ambayo siyo tu inatimiza katiba ya nchi inavyotaka ya kutusimamia na kutuelekeza lakini pia inaielea Wizara hii ili tuweze kufanya kazi vizuri ya Watanzania. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata shida kidogo wakati wa michango ikichangiwa hapa na nianze na hili ambalo nadhani pengine inatuweka vibaya sisi Mawaziri; kwamba eti ukiwa Waziri ni lazima ufanye mambo yote na pengine wakati mwingine hapa tumeshuhudia Mawaziri wakipata taabu kwamba wamejipendelea. Lakini leo hii tumeambiwa Mawaziri wengine hawajafanya kitu, na leo wameguswa Mawaziri wangu, Mheshimiwa Lukuvi hapa na Mheshimiwa Mary Nagu. Nataka niseme, katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya wananchi hususan umeme sisi kama Chama kilichoshinda uchaguzi tunatekeleza llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. (Makof)

Katika hili nataka niwaambie Watanzania, hatutapendelea na wala hatutanyima miradi ya maendeleo eti kwa sababu eneo hilo anatoka mpinzani. Hapana, hiyo siyo CCM. CCM ni ya Watanzania wote, na wana haki yao kupata maendeleo. Miradi inayosemwa kwa mfano ya Jimbo la Isimani ni miradi ambayo inafanyika katika Tarafa ya Idodi; kuna REA pale inafanyika *REA phase two* na Tarafa ya Pawaga yote. Zote hizi ni ahadi za Mheshimiwa Rais. Sisi tunatekeleza tu. Yeye ndiye msimamizi mkuu wa llani ya Uchaguzi. Kwa hiyo, Tarafa hii ya Idodi, Pawaga, na ambazo tayari mkandarasi amekwishapatikana, zote hizi zitapata umeme. Ni ahadi ya Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Mbunge anasimamia kwa karibu sana. Mimi hao wengine sijawahi kuwaona wakija hata kwangu na mimi ndio ninayekusanya mambo yote hapa. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarafa ya Pawaga, mkandarasi yupo kazini anaendelea na kazi, Tarafa ya Isimani

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)]*  
*Symbion wameshaweka Megawatt 10 na tunatarajia backbone Tarafa ya Isimani yote itapata umeme. Kwa hiyo, hii ni utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi. (Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mary Nangu ni Mbunge wa Hanang', amekuwa akiniandikia hapa na mara ya mwisho mwezi wa sita ameniletea barua ofisini. Waziri anakuja kwa Naibu Waziri kwamba tuunganishe Singa kwenye Herbada kupeleka umeme. Mheshimiwa Mary Nagu nikuhakikishie wewe ndio mbunge wa Jimbo hilo, ndiyе unayefuatilia na Uwaziri wako isiwe ni adhabu, na vijiji vingine hivi 17 vyote vitapata umeme. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende ajenda yangu ya pili, nizungumzie Shirika letu la *TANESCO* na changamoto za huduma kwa wateja. Nakubali ziko changamoto nyingi lakini tumejitahidi sana kuhakikisha kwamba zinapungua siku hadi siku. Tumekuja kupata shida tu, pale ambapo tulipopunguza bei, wamejitokeza Watanzania wengi wanaotaka kupata huduma hii. Labda nioneshe tu kwa mfano, tulikuwa tukoje. Mwaka 2005 tumeweka umeme kwa wateja 27,685; mwaka 2006, wateja 31,492; mwaka 2007 wateja 30,000, mwaka 2008, wateja 56,000 mwaka 2009, wateja 59,000; mwaka 2010, wateja 65,000; mwaka 2011, wateja 73,000; mwaka 2012, wateja 89,000; na kuanzia mwaka huu Januari hadi Novemba, tumeweka umeme kwa wateja 135,000. Haijawahi kutokea! (Makof)

Kwa hiyo, hata lengo letu la Serikali kwamba tutafikia lengo la 150,000 tatalitimiza na kwa asilimia tunakwenda asilimia 24 na lengo la ilani ya Uchaguzi ni asilimia 30. Nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wale wote ambao wanashirikiana na *TANESCO*. Mtusaidie tu katika kuboresha kutoa taarifa za wale ambao wanaotuchelewesha. Kwa hiyo, utaona kwamba changamoto tulizonazo sasa hivi ni upungufu wa nguzo na vifaa mbalimbali. Sasa tumejipanga, kuanzia sasa mpaka mwezi Machi, nataka niwahakikishie wale wateja wote ambao hawajafungiwa umeme hadi mwezi Machi tutakuwa tumewafungia umeme kwa sababu tunasambaza nguzo kwa kasi kubwa. Sasa hivi katika kanda

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)] zetu zote tano tutapeleka nguzo za awamu ya kwanza 18,000. Kwa hiyo, naamini kabisa hizi zitweza kutoa punguzo kubwa na tatizo liliopo.

Nichukue nafasi hii kuwaagiza *TANESCO* kwamba watusaidie. Hivi mteja ambaye hahitaji nguzo, anawezaje kukaa kwenye kusubiri hadi zaidi ya muda ule uliopo kisheria wa zaidi ya wiki mbili? Nichukue nafasi hii kuwaagiza kwamba mteja ambaye hahitaji nguzo, anahitaji mita na waya tu, haitaji kusubiri zaidi ya muda huo. Naagiza kwamba, mwezi Januari ndiyo mwisho wa kusikia mteja ambaye ahitaji nguzo anasubiri subiri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeamua na tumedhamiria kwamba lazima *TANESCO* ibadilike. Madaraka mengi ya *TANESCO* Waheshimiwa Wabunge yalikuwa yame-concentrate Dar es Salaam. Sasa tumeamua kuweka *reform*, taarifa ya wataalam iko tayari na tumeshirikiana na *TANESCO* wenyewe, tumekubaliana madaraka yashushwe Mikoani, Mikoa iagize vifaa vyao, Mikoa ionicze, Mikoa isimamie Idara zote za ufundi na nydinge zote na siyo kuweka Dar es Salaam watu wachache waamue, hii ndiyo inayotuletea shida na mimi hili naamini kabisa litatusaidia kupunguza usumbufu uliopo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, usambazaji wa umeme *REA phase II*, imesemwa hapa baadhi ya Mikoa ambayo ilikuwa hajapata wakandarasi, nichukue nafasi hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kwamba leo hii Dar es Salaam wanamalizia na kesho tunaweza tutatangaza Wakandarasi wote wa Mikoa yote. Tumewaaagiza na kwamba lazima tuhakikishe tunawapatia Wabunge mwende mkale *Christmas* mkiwa na orodha ya wakandarasi wenu. (*Makof!*)

Mheshimiwai Naibu Spika, imesemwa hapa juu ya maeneo ya huduma za jamii ambazo haziwekewi huduma ya umeme. Nichukue nafasi hii kusema na nimeshasema mara nyangi na hili ni agizo la Mheshimiwa Waziri wetu kwamba sehemu zote za huduma za jamii ni lazima

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)]* zipelekewe umeme. Katika *REA phase II* maeneo haya yote ndiyo kipaumbele ya kupelekewe umeme. Kwa hiyo, *REA* wahakikishe kwamba wanasogeza umeme pale.

Nichukue nafasi hii kuwaomba Halmashauri zote nchini na Taasisi zote, jamani kazi yetu sisi ni kupeleka umeme mpaka karibu na kwako. *Service line*, inatakiwa tujipange kwenye Halmashauri zetu tuone kama ni sehemu ya miradi ya maendeleo, ijadiliwe kwenye *Ward Cili* watusaidie, maana tukiwaingizia mpaka ndani, mwisho watasema tulipie. Sasa hiyo haitakuwa biashara. Niwaombe sana Halmashauri zote nchini zijue umeme ni maendeleo na wananchi wanataka sana maendeleo haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii tena kueleza namna ambavyo tatizo la nguzo litabakia sasa ni historia, kwa sababu kuanzia sasa tunapeleka nguzo Kanda ya Ziwa kwa kuwa kuna upungufu wa nguzo 5,000 tumeamua kupeleka 6,500; Kilimanjaro na Arusha, kunatakiwa nguzo 9,500 tumeanza na 1,200 lakini hatutasmama, tutaendelea kupeleka; Dar es Salaam, *Coast*, Lindi, Mtwara kwa maana na Pwani, kuna *demand* zinahitajika nguzo 4,500 tumeanza kupeleka 6,000; Mbeya, Ruvuma, Rukwa, kunahitajika nguzo 6,000 tutaanza kupeleka 3,000 na nyingine zitakuja; Kanda ya Kati, Morogoro, Dodoma, Singida, kuna upungufu wa nguzo 7,400 lakini tunaanza kupeleka nguzo 4,000. Upungufu huu hautajirudia maana maeneo yaliyokuwa yanatuchelewesha yalikuwa ni pamoja na Sheria ya Manunuvi, tumeyafanyia marekebisho, sasa *flowiko* vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kigoma iko kwenye kanda ya Ziwa, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, tushirikiane. Wako watu wa chini katika Shirika la *TANESCO* wanaoharibu huduma hii tunayoitoa. Nichukue nafasi hii kuwaomba TAKUKURU watusaidie, kama wanatafuta wala rushwa wanaochelewesha, kila hatua ambayo mteja anaomba huduma ya *TANESCO* lazima itolewe rushwa; sisi tunasema hiyo siyo sera yetu, hiyo ni sera ya watu wahujumu wa uchumi, sera ya watu ambao wanatuibia. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuwaomba sana kwamba maeneo hayo

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)] tunapambana nayo, lakini yanafanywa na watu wa chini. Kwa hiyo, huko wanakokwenda sisi hatuwezi kufika, lakini tutajitahidi na tumekubaliana tutarekebisha hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa muda ulionipa. Naunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Naibu Waziri wa Nishati na Madini - Mheshimiwa George Simbachawene, sasa naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa Prof. Muhongo.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba kutoa ufanuzi kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, nishukuru Kamati chini ya Mwenyekiti wake Mwambalaswa anafanya kazi nzuri sana, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wengine. Vilevile nishukuru Kamati ya Bajeti ambayo imetusaidia sana kuweza kuleta fedha *REA* na kwa ujumla Waheshimiwa Wabunge niwashukuru sana michango yenu ilikuwa mizuri, tumeifuatilia na napenda kuwahakikishia kwamba Wizara yetu haiumii au haichukii kukosolewa, ili mradi kukosolewa kuwe ni kwa maana. (*Makof*)

Nianze na *REA*. Kwanza, kabisa niombe samahani kwa Naibu Waziri, nilikuwa sijamweleza, tulipishana dakika chache, Bodi ilikuwa inakaa baada ya kuona kwamba miradi waliyoisema ianze Oktoba haijaanza. Nimewaambia Bodi jana na leo walikuwa na kikao wamemaliza kama nusu saa iliyopita na wameniletea kwa *FAX*. Haya ndiyo maamuzi yao na lazima yatekelezwe. Yasipotekelezwa inamaanisha kwamba hiyo *Management* inabidi iondoke na ikishindwa kuwaondoa mimi nitawaondoa. (*Makof*)

Tumekubaliana hivi, ujumbe walioniletea kwamba ikifika tarehe 31 Januari, 2014 watakuwa wameshawachagua Wakandarasi. Hii ni kutoka na Sheria ya Manunuzi. Sheria ya Manunuzi imewachelewesha. Itakapofika tarehe 15 Februari, 2014 yule Mkandarasi atakayekuwa amechaguliwa kama

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[WAZIRI WA NISHATI NA MADINI ]*

hatakuwa tayari kufanya kazi, itabidi aachwe achukuliwe mwagine. Kwa kuwa ndugu zangu na marafiki zangu Waheshimiwa Wabunge kete ya kurudi Bungeni hapa wenye Majimbo wengine ni umeme, miradi yote ya umeme itaanza tarehe I Machi, 2013 na itakwisha Juni, 2015. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mtakuwa mna hali nzuri. (*Makofii*)

Vile vile tumeleka kwamba hao Wakandarasi wakipatikana tutawapeleka kwenye Serikali ya Mkoa, Serikali ya Wilaya na tutawapatia majina na *contract* zao na Halmashauri mtusaidie kufuatilia. (*Makofii*)

Kuhusiana na mambo ya fedha, wengine walikuwa wanasema kuhusu bajeti ya *REA*; bajeti ya *REA* ya miaka miaka miwili ni Shilingi billioni 881. Nadhani wengine wamekuwa hawalioni, bado sisi wenyewe tunatafuta fedha za nje kwa bidii sana. Tumepata fedha kutoka *Norway, African Development Bank, World Bank*, kutoka Sweden, na hivi sasa tuna majadiliano na fedha kutoka *European Union, Australia* na *United Kingdom*. Kwa hiyo, hii ni Wizara inayotafuta fedha yenye. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu umeme vijijini; tumedhamiria kupeleka umeme vijijini na nataka kuwashakikishia kwamba ilani ya uchaguzi ya CCM inayosema kwamba ifikapo mwaka 2015 ni lazima Watanzania wasiopungua asilimia 30 wawe wamepata umeme ninawahakikishia hiyo asilimia itafikiwa na ni muda siyo mrefu.

Kwa hiyo, nawaomba msikilize kwa makini sana salamu za Mheshimiwa Rais za mwisho wa mwaka, nimemwachia, hili njukumu lake, naye ndiye mkubwa wetu, atawaeleza wananchi jinsi tunavyokwenda. Wale wanaobeza nadhani watashangaa kuona tunafanya miujiza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya mashirika yetu (*reform*), Manaibu Waziri wameongea kwamba tunaijenga *TPDC* mpya, na *TPDC* mpya Kampuni zilizoanzishwa ambazo hajaanza kazi zitaanza kazi hivi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NISHATI NA MADINI ]*

karibuni. Kuna *COPEC* ya kununua mafuta, kuna *GASCO* ya uuzaaji wa gesi, halafu tunatengeneza kampuni itakayosimamia shughuli za bomba. Vilevile tunatengeneza kampuni mbili ambazo kila Kampuni moja itapewa kitalu kimoja kimoja kile cha chini kabisa ambacho tunapakana na Msumbiji, tunajua kuna gesi nydingi katika hivyo vitalu kwa hiyo tutakuwa na kampuni mbili. Inamaanisha tutampatia mtu mmoja au nchi moja kuingia ubia na *TPDC*. Kwa hiyo, hayo ni mageuzi. Mageuzi siyo mpaka usimame kwenye gazeti uitishe *press conference*. Mageuzi ni vitendo na watu wanaona vitu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa fedha zitatoka wapi? Watu wengi wamesema fedha, fedha, na wengine wanasema tunaibiwa. Kwa mara ya kwanza kwa historia ya hii nchi tunapata *capital gain*.

Kampuni ya *OFIM* imeuziana *share* na kampuni *Pavilionya Singapore* na sisi tunaanza kupata *gain tax*. Yaani sasa Watanzania ile ya kusema tunaibiwa, tunaibiwa ni *history*. Ndiyo maana nasema Wizara yetu tunataka kwenda mbele zaidi kuliko kuonekana watu wamechoka, wanaongelea vitu vya miaka 1960, 1970. Ni kwamba yale mauziano yao tutapata Dola za Marekani zisizopungua milioni 258 (*two hundred and fifty eighty million USD*). Hayo ni mauziano tu na bado *TPDC* ina *share* huko.

Kwa hiyo, huo ndiyo mtaji wetu wa kwanza wa kufanya *TPDC* iingie kwenye shughuli za kibiasara na tumeshaandikia Hazina, nadhani Hazina itakubali zile fedha isipelekwe kwa watu. Nasikia wengine huku mnapewa fedha, hamsafiri na nini, sasa zisiende huko. Sasa hii Kampuni ya *TPDC* ikishakaa vizuri, haziwezi kwenda kuliwa, zitakwenda kwenye mafuta huko huko. (*Makof!*)

Hisa, ndugu zangu wanaosema Watanzania washiriki, tuachane na mambo ya ubin afsi, na ulafi, mtu anatumwa kuja kuongea vitu asivyo vielewa. Hili Kampuni la *TPDC* ikishasukwa ikasimama sawasawa tume sema wananchi watauziwa hisa kwa uwazi kabisa. (*Makof!*)

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[WAZIRI WA NISHATI NA MADINI ]

TANESCO, mmeishaelezwa mabadiliko yake. Nyaraka zote mbili tunazo. Tumeshaanza kurekebisha hili Shirika, ndio maana Naibu Waziri amesema tuna-decentralize, inabidi vifaa vingine vianze kununuliwa kwenye Kanda huko. Mimi ninazo *documents* mbili. Ni kwamba kuanzia mwezi Januari, 2014 zoezi hili linaanza. Lakini tumeishaanza. Kuanza ni kuona vitendo. Kuibadili TANESCO ni lazima ulifanye kitaalam, kwa sababu rasilimali za TANESCO ni Shilingi trillioni nne (*Four trillion Tanzanian Shillings*).

Kwa hiyo, siyo Shirika la kuamka tu asubuhi unasema navuja Shirika, ninaanzisha Mashirika 100, haiwezekani. Utakuwa hujafanya kazi kitaalam. Kwa hiyo, tunalibadili. Lakini wakati tunalibadili, vile vile tunanzisha Kampuni nydingine. Kwa mfano, mambo ya umeme wa Joto Ardhi (*Geothermal*). Tumeanzisha Kampuni chini ya TANESCO, ambayo inaanza kazi mwakani, kazi yake ni kushughulikia *Geothermal Energy*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuibadilisha TANESCO, tumetafuta fedha za ndani na za nje. Tumepata Dola za Kimarekani milioni 300, kutoka *World Bank*. Juzi tumepata milioni 50, kutoka *African Development Bank*. Tena juzi hiyo hiyo tumepata kutoka *African Development Bank* milioni saba kwa ajili ya *reform* ya TANESCO. Hizi fedha kwanza kutolea, wanaozitoa wana imani kwamba kweli kazi itafanyika, na wana imani na watekeleza wale wanaotekeleza. Kwa hiyo, mtu asiyeamini ni shauri lake. Kama wewe hapa unakaa huamini, dunia nzima inaamini, hatuwezi kubishana na wewe, tutakuacha ukae hivyo hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa wamesema suala la nishati kuchanganyika. Hili nililiongea kwenye Bajeti, naomba nilirudie tena. *Energy Mix* huwa inakaa kati ya miaka 20 mpaka miaka 30 duniani kote. Sasa *Energy Mix* yetu mchanganyiko wa kupata umeme tutazalisha umeme kutoka kwenye gesi asilia ambayo tuna 46 *trillion cubic feet*, tutapata umeme kutoka kwenye Makaa ya Mawe, ambayo tuna

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NISHATI NA MADINI]*

*deposit ya 1.5.5 billion tons.* Mwingine anauliza Makaa ya Mawe hatujui yapo!

Waheshimiwa Wabunge, niwaeleze. Ramani ambayo ni ya kisasa kabisa inayoonesha madini yote ya Tanzania ni mimi niliitengeneza. Sasa haiwezekani mimi nisijue Makaa yako wapi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Makaa ya Mawe tuayatumia. Kuna hili la Maji (*Hydro*). Mchangiaji mwingine amesema twende tuendeleze *Stiglers*.

Mheshimiwa Mbunge aliyeongelea suala la *Stiglers* hajui Sayansi hairuhusu *Stiglers*. Watu wa *Stiglers* walikuja nikawaambia waje na *Water Budget*. Ukitengeneza *Hydro Dam*, lazima uje na *Water Budget*. Una maji kiasi unapokea, kiasi gani unatumia na kiasi gani yanayobaki. Hayo ndiyo mambo ya kitaamam. Kwa hiyo, unaposema *Stiglers*, njoo ofisini kwagu na *Water Budget*. Kama huna hiyo, achana na hiyo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Ndugu zangu tuseme mitambo yetu yote ya kufua umeme kwa kutumia maji, *capacity* yake ni 562 *Megawatts*.

Sasa hivi tuna matatizol! Sasa tutakuwa kama watu kusema kweli siyo Wanasayansi; kuna Mabwawa hapa yamekauka, halafu mtu anakwambia jenga *Stiglers*. Ni kitu cha ajabu sana hicho. Hairuhusiwi duniani, na hatuwezi kufanya kosa kama hilo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu tutazalisha umeme kutoka kwenye nishati jadidifu, yaani *renewable energies*, iwe ya *Solar, ya Wind, Geothermal...*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa, nusu dakika; hivi yule aliyekuwa anasema Waziri mzigo yuko wapi tena? Mheshimiwa Profesa endelea na mchango wako. (*Kicheko/Makofi*)

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Waziri Kivuli, inabidi achukue *notes* huko labda. (*Kicheko/Makofi*)

Sasa ndugu zangu tuendelee na maelezo yetu. Kwa hiyo, hivyo vyanzo vingine tunavyo. Wengi wamesema kuhusu *STAMICO*. Ndugu zangu niwaeleze, tunataka *sector* ya watu binafsi, lakini duniani kote kama unaujua uchumi wa dunia, huwezi ukaacha *a private sector* kwa nchi kama za kwetu hata kubwa bila kuingiza mkono wa Serikali (*public*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii kama wewe ni *scholar* mzuri, Wamarekani na Waingereza, wakifanya *analysis* kwa nini China imekuja kwa nguvu, wanagundua kwamba kumbe Uchumi wa China uliotumia mkono wa Serikali ni uchumi mzuri sana. Kwa hiyo, hii *STAMICO* tunajijenga na inaanizisha Makampuni yafutayo:-

Tulawaka wana Kampuni; wameongelea Kiwira, Kiwira kila kitu tumemaliza wanayo Kampuni ya pili; Kampuni ya tatu, wataanzisha ya Kyerwa kwenda kununua ile batu ambayo inaenda kuuzwa kule Rwanda na Burundi. (*Makofi*)

Wengine wameongelea *TMMA* na Naibu Waziri ameongea, lakini niwaeleze toka *TMMA*, ianze kazi, imeokoa zaidi ya Shilingi bilioni 2.2. Imeweka Ma-*Desk* yake kwenye uwanja wa ndege, imeishashika matukio 32 na kujaribu kuokoa madini ya dhamani Shilingi bilioni 15.8. Sasa kama mtu anahoji *TMMA*, ni mtu kama hafahamu, afadhali kwanza aje ofisini apate takwimu ndipo aanze kuhoji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye Sekta ya Madini. Mchango wetu mwaka 2013 ulikuwa asilimia 3.5 wa *GDP* Pato la Taifa. Lakini ndugu zangu mnaoimba, Mbunge mwagine amesema Profesa lugha zako usikatishe watu tamaa; kwanza sayansi hakuna kukata tamaa *you must survive!* Sasa nakukatishaje tamaa?

Hii dunia haitaki watu dhaifu. Kama ukielezwa unashindwa, *then you a weak person.* Siwezi kukuweka moyo

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NISHATI NA MADINI ]*

kwa kudanganya. Well, mimi nitakuweka moyo kwa kukupatia vitu vya haki kabisa vya ukweli. (Kicheko/Makofi)

Sasa ndugu zangu, nilirudia, naomba niongelee hili la rasilimali. Msidanganyike, adui wa maendeleo wa nchi yetu ni Mtanzania mwenyewe. Naomba nitoe takwimu za kuthibitisha huo usemi wangu. Ukichukua maeneo yote yaliyotolewa leseni ya migodi Tanzania nzima, Watanzania ndio wenye asilimia 70.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa.

**WAHESHIMIWA WABUNGE:** Aaah!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Bado!

**WABUNGE FULANI:** Mwongeze dakika kumi.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Bado dakika moja tu.  
Ni kengele ya kwanza hiyo!

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Ya kwanza!

**NAIBU SPIKA:** Tayari, muda wake umekwisha?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Kengele ya kwanza!

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, muda wako umekwisha  
Mheshimiwa Profesa.

**WAHESHIMIWA WABUNGE:** Mwongeze dakika 10.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MBJNGE FULANI:** Mwongeze dakika kumi.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**NAIBU SPIKA:** Hata mimi ningelipenda Mheshimiwa Profesa aendelee, lakini muda hauko upande wetu.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** No. Lakini nataka kuonesha watu ambao hawalipi kodi,...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa. Sasa ni wakati wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi. Anazo dakika kumi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nikushukuru kwa kupata nafasi hii na mimi nichangie katika hoja iliyopo mbele yetu. Kabla sijachangia naomba nitoe pole sana kwa wananchi wangu wa Wilaya ya Wanging'ombe. Nyumba 36 za wananchi wangu zimeezuliwa na mvua juzi katika Vijiji vya Dulamo, Mambegu, Luduga, Iponda, Kanani, Chalowe, Igwachanya. Nyumba 36. Niseme tu kwmaba Mbunge wenu yuko pamoja na nyinyi, nitakuja kushughulika tuone ni namna gani nitakavyowasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania yetu ni kubwa kama mnavyofahamu. Tuna kilometra zaidi ya 86,000. Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Jakaya Kikwete, wakati anaingia madarakani alikabidhiwa kilomita 6,000 tu barabara zenye lami. Naye akasema ili niweze kuongeza kasi ya uchumi wa nchi hii, naweka kipaumbele katika kujenga barabara za lami, na akaanza na ujenzi wa kilomita 11,550 kiwango cha lami, toka alivyoingia Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete. Ni kazi kubwa. (*Makofii*)

Hata ukiangalia kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010, orodha ni kubwa sana, ni ndefu, Waheshimiwa Wabunge kila moja ana barabara yake hapa ambayo anataka ijengwe kwa kiwango cha lami. Sasa uwezo wa Serikali peke yake inawezekana tukahitaji pengine nje ya Bajeti, kama walivyosema Kamati ya Miundombinu. Serikali ndivyo inavyofanya. Kwa sababu ukichukua barabara hizi zote katika miaka kumi unazungumza zaidi ya Shilingi trilioni 115 zijengwe ndani ya miaka 10. Wizara yetu ya Ujenzi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA UJENZI ]*

imekuwa inapata fedha chini ya Shilingi trillioni moja kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumeweza kutumia mbinu, ni lazima mtu uwe mbunifu katika kutekeleza Miradi mikubwa ya namba hiyo. Kwamba unaweka Makandarasi, Makandarasi wana viwango tofauti vyta utekelezaji. Lakini tumefanya vizuri, zaidi ya asilimia 70 ya Miradi ya barabara, kwa mfano ulioingiwa kuanzia mwaka 2008, iko mbioni kukamilika. Kwa hiyo, sehemu kubwa ya barabara hizi ziko mbioni kukamilika. Tunategemea kwamba tukifika mwaka 2015 tuwe na kilomita hizo 17,000 zilizojengwa kwa kiwango cha lami.

Sasa nikija kwenye hoja za Waheshimiwa Wabunge, tuseme tukianza na Kamati ya Miundombinu, kwanza nimpongeze Mwenyekiti pamoja na Kamati yake, wametupa mapendekezo mazuri ya kutujenga, hawajatubomoa; wametupa moyo; Mheshimiwa Dkt. Magufuli huko aliko, pamoja na kwamba ana mziba, anasikia vizuri kwa sababu wengi wamemsifia. Nami naendelea kumpongeza pia, kwamba aendelee na kasi hiyo. Waheshimiwa Wabunge tumuunge mkono ili tuweze kuifanya nchi hii ifunguke, wananchi waweze kuuza mazao yao, wapate thamani bora zaidi ya mazao yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imezungumza kwa uchungu sana kuhusu msongamano wa magari barabarani katika Jiji la Dar es Salaam. Serikali iliishaanza kutekeleza kwa nguvu sana kuanzia mwaka 2009 kupunguza msongamano. Kama nilivyosema hapo awali, hatuwezi kuondoa msongamano kwa sababu katika Jiji la Dar es Salaam, jinsi nilivyokuwa limepangwa, shughuli zote ziko mahali pamoja katika Wilaya ya Ilala. Maofisi yote yako Wilaya ya Ilala.

Kwa hiyo, asubuhi magari yote zaidi ya 10,000 yanakwenda Ilala, na jioni magari yote yanarudi. Kwa vyovyyote vile lazima msongamano uwepo. Lakini lazima tutafute mbinu nyngine, tupate sehemu nyngine, kwa mfano katika Wilaya ya Kinondoni yajengwe maofisi kule, zijengwe

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA UJENZI ]

Super Markets katika Wilaya ya Temeke, ili kusudi kusiwe na ulazima kwamba kila mtu asubuhi anakwenda katikati ya Jiji la Dar es Salaam. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tunayo miradi ambayo inaendelea likiwepo Daraja la Kigamboni. Kwa vyovyote vile daraja hili ni mfano ambao tunajenga kwa kutumia sekta shirikishi, Sekta ya NSSF, na sasa hivi tunaingia kwenye ubia tuanze kuingiza kwenye sekta binafsi katika ujenzi wa barabara. Lakini wananchi waambiwe kwamba barabara zile ambazo zitajengwa kwa utaratibu ule, lazima tutalipia kidogo ili tuweze kumaliza barabara nyingi. Huu ndiyo mfano ambao nchi nyingi hata Malaysia barabara nyingi ukipita kule ukitaka kufika haraka, basi utapita kwenye barabara ambazo utatoa kidogo pesa. Sasa hiyo ni *approach* ambayo tutakwenda nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo miradi kwa mfano kupanua barabara ya Mwenge – Tegeta, nayo tunategemea kabisa ikiisha, msongamano utapungua kwa kiasi fulani. Tuna barabara hii ya mabasi yaendayo kwa kasi, kutoka Kimara mpaka Kivukoni. Kwa vyovyote vile miradi hii ikimalizika foleni itapungua, ingawa haiwezi kumaliza tatizo hili. Tunaanza ujenzi wa *flyovers* pale TAZARA, Serikali ya Japan inatusaidia, tutajenga *flyover* pale Ubungo na maeneo mengine, kwa lengo la kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda niendele na mambo mengine. Waheshimiwa Wabunge wengi mmezungumza suala la kudhibiti uzito. Kwa sasa hivi tunayo mizani ya kupia uzito wa magari. Tunazo mizani 28. Lakini tunacosema ni kwamba kwenye mizani kuna msongamano. *Approach* tunayoitaka sasa hivi ni kujenga mizani ya kisasa. Ni kwamba gari litakuwa linapima huku linatembea. Lakini tutaanza na kujenga mizani wa kisasa pale Kurasini, kwamba gari likishapimwa uzito wake pale Kurasini, tuna uhakika kwamba tutafanya *tracking system* kuangalia hiyo gari. Kwa mfano, ile mizigo inayokwenda *transit*, nchi za Burundi, kutakuwa na *tracking system* ambayo tunajua

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA UJENZI ]

hatakwenda route tofauti na ile iliyopangwa. Kwa hiyo, atakuwa na sehemu tatu za kukaguliwa. Atakaguliwa Vigwaza. Manyoni na Nyakanazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mpango ambao tumekubaliana kwenye Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, tuwe na vituo vitatu vya kukagua magari yale ya *transit*. Lakini kwa magari yetu haya na Watanzania kwa kweli nawaomba sana wenye malori, tunajua ni watu muhimu sana katika uchumi wa nchi hii, lakini tumekuwa tunapambana zaidi ya asilimia 25 ya magari sasa hivi haya malori yanazidisha uzito. Ndiyo maana Waziri wetu amekuwa mkali kweli kweli. Lazima tuwe wakali, kwa sababu vinginevyo barabara hizi zinazojengwa kwa fedha nyingi za Watanzania, haziwezi kudumu. Tunaomba wote tushirikiane katika suala hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la barabara kuharibika mapema. Wabunge wengi wamezungumza kwamba barabara zinaharibika mapema. Lakini kutohana na takwimu tulizonazo zaidi ya asilimia 80 ya barabara ambazo tunazijenga haziharibiki mapema. Barabara hizi zinasanifiwa kwa miaka 20. Lakini ukiweka lami nyepesi kitaalam, mimi ni Mhandisi; inatakiwa baada ya miaka saba lazima uweke *layer* nyingine ya lami.

Kuna Mheshimiwa mwingine amezungumza kwamba tunaweka lami unene kidogo. Lakini ule unene wa lami siyo unaobeba mzigo. Mzigo unabebwa na lile tuta. Unachanganya na *cement*, ukiweka nene zaidi maana yake itabeba mzigo mkubwa zaidi. Kwa Tanzania *standard* zetu barabara hizi tumezisanifu kubeba mzigo usiozidi tani 56.

Sasa kinachokuwa kinapimwa pale ni ile *excel*. Yaani gari likiwa na *excel* kumi, basi huo mzigo u-*spread* kwenye *excel* kumi. Sasa tunachosema nini kimezidisha, ni kile kinachozidi kwenye ile *excel limit* ambayo imewekwa. Hiyo sasa imewekwa kwenye Sheria. Waziri wetu amepewa mamlaka ya kutenegeneza kanuni. Sasa kesho akiona uharibu wa barabara unakwenda kwa kasi, anaweza akapunguza hiyo *excel limit*, amepewa madaraka yale. Kwa

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA UJENZI ]

hiyo, nawaomba sana Watanzania tusilalamike kama atapunguza *excel/limit* kwa maana ya kulinda barabara zetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie suala la Ndundu – Somanga. Mheshimiwa Murtaza Mangungu, pamoja na Mheshimiwa Said Mtanda, wamezungumza kwa uchungu. Mtu mwingine akisikiliza atasema Seikali ya CCM, haijafanya chochote kwa wananchi wa Kusini. Sasa niwaambie ukweli kwamba Serikali ya CCM imeshajenga kilometra 450 kutoka Dar es Salaam mpaka Lindi. Sasa hivi hicho kipande kinacholalamikiwa zimebakia kilometra 14 tu kuwekwa lami. Sasa kwa nini tusiishukuru Serikali ya CCM kwa kazi nzuri iliyofanya? Lakini mtu atalalamika kwa nguvu kweli! (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi pale kuna Mkandarasi, ni kweli hana kasi inayotakiwa, lakini naamini kabisa kazi ile itakamilika kwa muda tuliokulaliana. Akichelewa, tuna nafasi ya tozo iko kwenye mkataba, huo ndiyo utaratibu wetu.

Kwa hiyo, kama atachelewesha tutamkata kwenye tozo. Lakini tukisema tumfukuze leo, barabara hiyo mpaka mwaka 2015 itakuwa haijaisha. Maana tukianza mchakato wa kumpata Mkandarasi mwingine tutachukua mwaka mzima, aje, naye huyo pengine atalegalega zaidi; naomba tumvumilia huyu Mkandarasi amalize. Lakini sisi tuna mahali pa kumtoza ili amalize kazi ile. Kimkataba alitakiwa amalize mwezi Desemba, 2013. Kama atachelewesha atamaliza zaidi ya hapo tutamkata.

Kwa hiyo, Serikai haitapoteza. Hivyo ndivyo vitu ambavyo tunaweka kwenye Mikataba.

Nzungumze suala lingine ambalo Waheshimwa Wabunge mmelizungumza, suala la *maintenance*. Mheshimiwa James Mbatia, umezungumza kwamba ni lazima tuwe na *sustainable maintenance system*. Tuwe na mpango

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA UJENZI ]

endelevu wa matengenezo wa barabara zetu. Serikali ilianzisha Mfuko wa Barabara.

Kazi ya Mfuko ule ni kufanya matengenezo. Asilimia 90 ya fedha zile ni kutengeneza Barabara. Kama mnavyofahamu na wananchi Tanzania nzima, Mikoa yetu Ma-Managerwa *TANROAD* kila mmoja anakotoka barabara zinakuwa nzuri, kwa sababu zinatengenezwa. Barabara haiwezi kutengenezwa kama fedha hazipo. Kwa hiyo, lazima uwe na mfuko ambao una uhakika fedha zake zipo ili uweze kutengeneza barabaa zile. Sababu mojawapo ambayo husababisha barabara kunaharibika mapema ni pale ambapo barabara hazitengenezwi kwa wakati unaotakiwa. Kwa hiyo, lazima uwe na *intervention* inayotakiwa ili kusudi barabara yako iweze kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nafasi inaruhusu, nijibu baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezungumza. Mheshimiwa Maryam Msabaha amezungumza kwa kirefu na kuonekana kabisa kama vile barabara zote tunazozijenga zinaharibika mapema.

Nataka niseme kwamba hii siyo kweli na kwa bahati nzuri yeye yuko kwenye Kamati ya Miundombinu, na kwa sehemu kubwa tukikutana naye wamekuwa wanatupongeza. Kwa hiyo, naomba tuwaambie wananchi ule ukweli, kwamba Wizara ya Ujenzi ndiyo inayotupeleka mbele katika matengenezo na ujenzi wa barabara katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wamezungumza habari ya malori mazito haya, labda watozwe zaidi. Lakini mimi nasema suala la malori tutasimamia sana utekelezaji wa sheria katika kudhibiti uzito wa magari.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha  
kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Simwoni Mheshimiwa Profesa Mbarawa, natumaini Naibu Waziri wa Sayansi na Teknolojia ataongea; dakika kumi tafadhal!

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuzungumza. Dakika kumi ni chache lakini nitajitahidi kujibu na yale ambayo sitayajibu, basi tutawajibu kwa maandishi Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia.

Nianze na suala la minara na mawasiliano vijijini. Kwa Wabunge waliochangia na hata wale ambao hawakupata fursa ya kuchangia, nafahamu kwamba hili ni jambo ambalo liko ndani ya nyoyo zao na ndani ya mahitaji ya wapiga kura wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba tulivoamua kuifanya sekta hii iwe sekta binafsi tulitoa fursa kwa makampuni binafsi kupeleka mawasiliano kule wanakotaka. Kwa maana hiyo, makampuni mengi binafsi yaliama kupeleka mawasiliano maeneo ya mijini kuliko vijijini. Baada ya kubaini kasoro hiyo, Serikali ikaanzisha mfuko wa mawasiliano kwa wote kwa maana ya kutoa ruzuku kwa makampuni binafsi yapeleke mawasiliano vijijini ambapo hakuna mvuto wa kibiashara. Sasa licha ya ruzuku, bado makampuni hayo yamekuwa na kiburi au uamuzi wa kupeleka au kutopeleka mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya kubaini kwamba tunalo tatizo, tumeamua kubadilisha utaratibu. Mawasiliano ni miundombinu muhimu sana ya uchumi kama ilivyo umeme, barabara na reli. Sote tunafahamu kwamba Serikali imekuwa inawekeza fedha nyingi sana kwenye kujenga barabara, reli na kupeleka umeme vijijini. Sasa Waheshimiwa Wabunge wengi hapa wamekuwa wakiidai Wizara minara, lakini wanatudai minara wakati hatujatengewa hata senti tano ya kujenga mnara hata

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA ]  
mmoja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge unapokuja kunidai mnara na mimi nakwenda kuomba kwenye kampuni binafsi ambayo inaweza ikakubali au isikubali kujenga ule mnara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kitu ambacho tumeamua na ambacho napenda kuwaomba Waheshimiwa Wabunge mtuunge mkono ni kwamba kuanzia mwaka ujao wa fedha na sisi kama Wizara tutaomba fedha za Serikali tutengewe na sisi ili tujenge minara vijijini, ili pale Mheshimiwa Mbunge anapokuja kunidai mnara, basi angalau niwe na fedha ambayo Serikali imetenga kama inavyotenga kwenye umeme na kwenye barabara. Tunaamini kwamba hii itakuwa na tija kubwa. Ni kweli umeme ni muhimu sana, lakini unapopeleka umeme kijijini, mwananchi bado analazimika kufanya *wiring* ndani ya nyumba na kadhalika. Lakini ukijenga mnara, anachohitajika ni kununua simu tu.

Kwa hiyo, imani yetu ni kwamba tumeomba wenzetu Wizara ya Fedha watuunge mkono tutakapoomba fedha hizo takribani Shilingi bilioni 300 kwa mara moja kwa ajili ya kujenga minara kote nchini ambapo hakuna minara. Ndiyo! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia suala la *TTCL*, ni kweli Shirika hili kwa muda mrefu limekuwa taabani, lakini kama Serikali tumechukua hatua ya kulirejesha. Kwanza, kama mnavyofahamu huko nyuma tulibadilisha, na Shirika hili lilikuwa linatumia teknolojia inaitwa *CDMA*, kwamba ukitaka kutumia mtandao wa *TTCL*, basi uwe na simu ya *TTCL* peke yake, huwezi kubadilisha *chip*. Matokeo yake ni kwamba kampuni hii imepoteza wateja wengi kutoka na teknolojia hiyo. Kwa hiyo, kitu ambacho Wizara tumefanya, mwezi uliopita tumefanikisha shirika kupewa masafa mapya mengine ambayo sasa yatawezesha shirika hili kuingia kwenye ushindani sawa na makampuni mengine.

Vilevile tupo kwenye mazungumzo na wenzetu wa *Airtel*/na mazungumzo hayo yapo kwenye hatua ya mwisho

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA ]*

ili tumalize ile ndoa, shirika hili liweze kumilikiwa 100% na Serikali ili tuweze kulidhamini kimtaji na liweze kukopa vilevile. (*Makof*)

Pia kumekuwa na matatizo ya *Management*. Kwa muda mrefu kumekuwa na ubadhilifu, tumewasimisha viongozi wakuu wanee na mimi binafsi nilipeleka masilitaka TAKUKURU kwa baadhi ya viongozi waliokuwa wanafanya ubadhirifu pale na *CAG* yupo anakagua. Ni imani yetu kwamba mapema mwaka ujao tutafika mahali ambapo tutapata ufumbuzi wa matatizo ya *Management*. Lakini pia tumempata *CEO* mpya na mchakato umeanza wa kujaza zile nafasi ambazo watu wanakaimu. Imani yetu ni kwamba mwakani sasa baada ya kumaliza ndoa na *Airtel*/na baada ya kukamilisha kupata masafa mapya, Shirika hili mtaliona sasa likirudi kwa nguvu na kushindana na mashirika mengine na kuirudishia heshima Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nimalize tu kwa kusema kwa ufupi kwamba katika utendaji wetu sisi kwenye nafasi za Serikali pamoja na Wabunge, sifa na heshima ya utendaji wakati mwingine inatokana na maumbile. Ukimshindanisha Kobe na Kiboko kucheza, siku zote Kiboko atashinda. Hapa wapo Waheshimiwa Wabunge na Mawaziri ambao wana maumbile ya Kobe, hata wacheze kwa bidii gani, wanaonekana kama hawachezi.

Kwa hiyo, kazi tunayoifanya kwa pamoja ni ya kuijenga nchi yetu, hakuna watu wazalendo kuliko wengine kwani wote tunaipenda nchi yetu kwa usawa. Kwa hiyo, tuheshimiane na tusaidiane katika kazi hizi tulizopewa kama Wabunge na kama Mawaziri. Kukejeliana na kukashifiana wakati wote wakati tunajenga nyumba moja, siyo jambo jema. (*Makof*)

Kwa hiyo, napenda kuwasihii wenzangu kwamba Tanzania hii ni yetu wote. Wale mliokaa upande ule na sisi tuliookaa upande huu, sisi tulipo Serikalini na ambao hawapo Serikalini tunajenga nyumba moja. Tukiwa humu ndani kukashifiana, kukatishana tama na kushutumiana hakuna sababu yoyote wala tija yoyote. (*Makof*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA ]

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nimalize kwa kusema kwamba kwa Wabunge ambaao hoja zao zijazigusa, tutawaandikia kila mmoja kutoa majibu ya maandishi. Wale ambaao wana maswali kuhusu minara, siku zote wasisite kuuliza, lakini dhamira yetu ni ile ile kwamba itakapofika mwaka 2015 kila eneo la nchi yetu ambalo halina mawasiliano litakuwa na mawasiliano. Hii ni ahadi ya Chama cha Mapinduzi na sisi tutaisimamia na tutaitekeleza. Mwakani tutakapoomba fedha kwa ajili hiyo, tunaomba mtuunge mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na sasa naomba nimsimamishe Naibu Waziri wa Uchukuzi – Mheshimiwa Dkt. Charles J. Tizeba.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba niwapongeze sana Wenyeviti wa Kamati kwa taarifa walizowasilisha pamoja na Wabunge waliopo katika Kamati hizo. Lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe kwa kazi nzuri sana anayoifanya ya kusimamia shughuli za uchukuzi hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utakuwa katika mambo kama matatu hivi na nilitaka nianze na suala la viwanja vya ndege. Wabunge wengi wamezungumzia viwanja vya ndege katika Mikoa na maeneo wanayotoka, lakini wengi wamezungumzia uwanja wa ndege wa Dar es Salaam, ujenzi wa jengo la abiliria sehemu ya tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa ujenzi wa *terminal three* katika uwanja wa ndege wa Julius Nyerere, Dar es Salaam, sasa upo katika hatua nzuri sana. Usanifu wa kwanza ulitaka tujenge jengo dogo, lakini baada ya kuona mahitaji yalivyo makubwa sana katika uwanja huo, Wizara iliishauri Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ipitie upya mchoro

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*/NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA J  
ule ili ijengwe jengo ambalo angalau litatufikisha mahali tunapopataka kwa mahitaji ya sasa.*

Kwa hiyo, upitiaji wa hiyo michoro umekamilika na utaratibu wa upatikanaji wa vibali mbalimbali kutoka Hazina na kwingine umekwisha na tunaratajia sasa *effective* tarehe 6 Januari, 2014 Mkandarasi ataanza shughuli za ujenzi moja kwa moja. Ujenzi huu tumeiomba kampuni ya *BAM* wahakikishe kwamba wanatukabidhi jengo letu ifikapo mwezi Juni, 2015. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uwanja wa ndege wa Mwanza na wenyewe unaendelea vizuri. Kwanza ulikumbwa na tatizo hilo hilo kwamba mchoro uliokuwa umetayarishwa mwanzo ulikuwa ni mdogo ambao usingekidhi mahitaji ya Mwanza. Kwa hiyo, nao walishauriwa pia wapitie upya ule mchoro. Mwezi uliopita tumewashirikisha wadau, wamekubaliana na ile *concept* na sasa hivi wanamalizia tu kufanya mapitio ya *BOQs*.

Kwa hiyo, jengo la uwanja wa ndege wa Mwanza litaanza kujengwa. Sasa hivi Mkandarasi yupo *site* wanarefusha barabara ya kutua na kurukia ndege kwa mita 500 zaidi. Wamekwishaanza hiyo shughuli, watajenga jengo la kupokelea mizigo, wamekwishaanza, misingi imekamilika, wanajenga jengo la kuongozea ndege, misingi imekwishamalizika. Kwa hiyo, tunategemea kwamba shughuli ile haitakuwa ndefu sana kama moja iliyowahi kutokea huko Mbeya. (*Makofi*)

Viwanja vingine vya ndege vya Bukoba, Kigoma na Tabora vimekamilika katika awamu hizo na Songwe pia jengo la abiria linaendelea kujengwa uwanja wenyewe, *runway* imeshakamilika na tutarajie sasa viwanja vya Shinyanga, Sumbawanga na Kigoma awamu ya pili. Vimekwishapata idhini ya kutumia pesa na kwa hiyo na vyenyewe vitaanza kujengwa baada ya muda si mrefu. Kigoma *runway* itaongezwa kuititia fedha ya *World Bank*, lakini jengo la abiria litajengwa kwa fedha ya *European Investment Bank*. (*Makofi*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA ]

Mheshimiwa Naibu Spika, wazungumzaji wa Kanda ya Kusini wamezungumzia *particular* uwanja wa Lindi. Lakini naomba niseme tu kwamba uwanja ule ulikuwa unatumika Shirika letu la Ndege la Tanzania (*Air Tanzania*) lilikuwa linakwenda Lindi. Lakini baada ya barabara ya Dar es Salaam - Lindi kutengemaa kwa kiwango kikubwa, abiria wamepungua katika uwanja ule na imekuwa ni hasara kwa mashirika yaliyokuwa yanakwenda pale. Ni kama ilivyo Dodoma. Dodoma siyo kwamba Makampuni hayataki kuja, lakini abiria hawatoshi kwa sababu ya barabara ya Dar es Salaam Dodoma ni nzuri. Lakini mahitaji yakikua, wale wafanyabiashara hawasubiri kuitwa, wanaona wenyewe; watakwenda na wataendelea kusafirisha abiria kutoka maeneo hayo.

Mwanzo Mbeya ilikuwa hawaendi Mbeya mjini, lakini kwa sababu mahitaji ni makubwa, sasa hivi Songwe abiria ni wengi na mashirika mengi yanazidi kuomba nafasi ya kwenda kuchukua abiria kule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie Bandari ya Lindi ambayo pia nimekwishaitolea ufanuzi mara kadhaa hapa Bungeni. Bandari ya Lindi siyo kwamba imetekelizwa na Serikali, tatizo liliopo pale ni ule mchanga ambao umeaja sana kwenye bandari ile iliyopo sasa kiasi cha kutowezesha meli kutia nanga. Mamlaka ya Bandari ilitenga fedha katika bajeti ya mwaka 2012 wakatangaza kumpata Mkandarasi wa kuongeza urefu wa bandari kuingia baharini, lakini hakupatikana mtu. Kwa hiyo, wametangaza tena. Tunatarajia safari tutawapata Wakandarasi wenyewe nia ya kufanya hiyo kazi na kwa hiyo, bandari ya Lindi itajengwa ili meli ziweze kuanza kusimama pale Lindi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari za Ziwa Tanganyika kwa ndugu yangu Mheshimiwa Keissy, Bandari ya Kipiri, nadhani ndani ya mwezi mmoja tutakuwa tumeikabidhi. Magati mengine yale manne kwa sababu ya Mkandarasi aliyejewa amepewa kwanza alishindwa kutekeleza kazi yake vizuri, tumetangaza upya watapatikana Wakandarasi na *this*

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA J  
time around tutakuwa makini sana ili tusipate Kandarasi  
legelege kazi zile ziweze kufanyika vizuri. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo suala la *MV. Liemba*, nimemsikia kwa makini sana Mheshimiwa Mbunge wa Sumbawanga ambaye ametoa pendekezo hapa kwamba wapo watu ambao wako tayari kutoa fedha ya mafuta ili wafanye safari nne kwa mwezi. Sisi hilo pendekezo tunalikaribisha. Nawaagiza basi *Marine Services* wafanye mazungumzo na Mbunge tuone hiyo *exercise* kama *ita-proof* kweli kwamba kwenye *MV. Liemba* upo wizi au haupo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kwa haraka haraka reli za Mtwara-Mbambabay na Tanga - Moshi - Arusha - Musoma. Tulipofika siyo pabaya katika reli hizi mbili. Tullitoa tangazo kwa reli zote, watu binafsi wenye nia ya kushiriki katika ujenzi wa hizo reli wajitokeze lakini yalijitokeza makampuni kwa reli zote mbili, tukafanya kuyatathmini, tukateua machache na sasa hivi Makampuni hayo yamepewa sasa nafasi ya kuleta *request for proposals*, yaani mchanganuo mrefu zaidi wa kitu gani wanataka kufanya, kwa muda gani na kadhalika ili tathmini ikifanyika, basi tuwapate Wakandarasi wawili Kusini na Kaskazini ambao wataingia mkataba na Serikali kwa ajili ya ujenzi wa hizo reli. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sio hatua ndogo. Katika hili niseme tu kwamba tutashirikisha sekta binafsi katika ujenzi wa hizi reli. Umuhimu wa hizi reli sidhani kama iko haja ya kuzungumzia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongezee tu kidogo kwa maelezo mazuri sana yaliyotolewa na Naibu Waziri wa Ujenzi kuhusu msongamano wa Dar es Salaam. Pamoja na hatua hizo ambazo zinachukuliwa na Wizara ya Ujenzi za kujenga barabara zinazopishana angani na kadhalika, *DART* inaendelea sasa hivi, watu wanaona Dar es Salaam lakini Wizara ya Uchukuzi ilianzisha usafiri wa treni pale Dar es Salaam na inaendelea kutoa huduma kwa reli za *TAZARA*,

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA ]  
reli ya Kati, Ubungo Maziwa mpaka Mjini na Pugu mpaka TAZARA. Tunadhamiria sana kwamba tutaongeza huduma hiyo nadhani katika bajeti mwaka 2014 ili tuwe na treni zinazokwenda mpaka Pugu kuititia uwanja wa ndege kurahisisha shughuli ya kwenda *Airport* kwa sababu kuna shida sana.

Pia tumetangaza kwamba wenyе nia ya kuwekeza katika usafiri huo wa Mjini Dar es Salaam kwa njia ya reli wafanye hivyo. Wizara ya Ujenzi pia inajenga meli itakayoanzia Bagamoyo mpaka mjini kuititia vituo tisa, Mheshimiwa Magufuli alikwishalitolea maelezo mazuri sana hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumeunda Kamati ya Serikali ya pamoja ya kuangalia tatizo zima la msongamano kwa Dar es Salaam na Wilaya za jirani na tunaendelea kufanya mazungumzo na kupeana mikakati namna gani tuboreshe usafiri wa Dar es Salaam na Wilaya za jirani kwa maana ya Bagamoyo, Kisarawe, Kibaha na Mkuranga ili usafiri wa Dar es Salaam usijikite katika eneo la kiutawala la Mkoa wa Dar es Salaam peke yake, bali upanuke huko kote ambako Mji kwa sasa umefika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja!  
(*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Naibu Waziri wa Uchukuzi  
- Mheshimiwa Dkt. Tizeba na sasa nimwite Waziri wa Uchukuzi  
- Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe kwa dakika kumi.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu nitumie maji haya kwani nakohoaa, nashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nizishukuru Kamati zote mbili pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao, lakini vile vile niwashukuru kipekee Wabunge wote wanaotambua kazi

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI]*

ngumu tuliyonayo ya kufufua miundombinu ya uchukuzi nchini na kutupa moyo kusonga mbele. Tutasonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikiliza kwa makini michango yote ya Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli nitaongelea michache tu, mengine kama alivyosema Mheshimiwa Dkt. Tizeba tutaiwasilisha kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeongelea mambo mengi, nianze na suala la *TAZARA*. Kwanza tunashauriwa kwamba tuhakikishe Mkurugenzi Mkuu wa *TAZARA* anatoka hotelini. Nilitaka tu niseme tu kwamba ushauri huu umechelewa kidogo, tulishachukua hatua muda mrefu, huyo bwana mkubwa hayuko Hotelini.

Pili Kamati ilishauri turekebishe Sheria ya *TAZARA* inayotoa kipaumbele kikubwa kwa *MD* wa *TAZARA* na kwamba *MD* lazima awe Mzambia. Ushauri vile vile umechelewa, tulishaanza mchakato mwezi Januari na sasa hivi Kamati ya Wataalamu wa Tanzania wakiongozwa na *CPDwako* Lusaka, Zambia kubadilishana mawazo na wenzao wa Zambia kabla hayo mawazo hayajafikia Baraza la Mawaziri.

Kamati inashauri madeni ya *TAZARA* yafuatiliwe. Hilo vile vile tumelifanyia kazi, kufikia mwezi uliopita tumekusanya Dola milioni 1.2. Yapo madeni sugu ambayo Baraza la Mawaziri itabidi tuwasaidie wenzetu kuweza kukusanya. Kuna deni la Shirika la Reli la Kongo, kuna deni la Shirika la Reli la Zambia na deni vile vile la *NFRA* la Tanzania tayari nimekwishampelekea *notice* mwenzangu ndugu yangu Mheshimiwa Chiza na Mheshimiwa Malima kwamba kuna wajibu wa kulipa hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa angalizo, hata kama tutakusanya madeni yote, *TAZARA* inahitaji kuwezeshwa upya, inahitaji mtaji mpya iweze kusonga mbele. Nasema hivyo kwa sababu sasa hivi *TAZARA* inahudumia mizigo kidogo sana ikilinganishwa na mwaka 2004/2005 ambapo ilikuwa inaweza kuhudumia tani 54,000, ilikuwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI ]

inawaingizia zaidi ya Dola milioni 4.35; leo hii wanahudumia tani 23,000 tu na wanapata Dola milioni 1.5 wakati mahitaji ni Dola milioni 2.5.

Waheshimiwa Wabunge wametoa ushauri mwingi kuhusu *TAZARA*, nami naomba niseme kama Wizara sasa, kwamba Wizara inaona sasa wakati umefika kuteua Wajumbe watano wa Kamati ya Miundombinu na Wajumbe watano wa Kamati ya Bajeti kwenda Lusaka Zambia kukabiliana na Wabunge wenzetu wa Zambia, tulijadili suala hili kuhusu hatma ya *TAZARA*. Nina uhakika Kamati hii tutakayoituma kwenda Zambia itakuja pengine na mawazo mazuri kuisaidia Serikali tufanye nini. Namshukuru sana Mheshimiwa Rebecca Mgondo kwa mchango wake kuhusu suala hili.

Kamati vile vile imeongelea suala la *ATCL* na kudai kwamba Wizara ya Uchukuzi haitoi ushirikiano wa kutosha kwa wawekezaji, hapana. Kwa sababu imeandikwa kimaandishi, lazima nijibu. Siyo sahihi hata kidogo na bahati mbaya Kamati haikutoa jina hata la huyo mmoja tuliyemkatalia kumsikiliza inasema tu ukurasa wa 17, yule Mchina aliyetaka kuleta ndege tisa. Hizo ni porojo tu. Unajua hamna mtu dunia hii ya leo atakayekuletea ndege bure.

Mimi naomba niseme Waheshimiwa Wabunge kwamba, kuna *tendency* ya kuona mtu akishachaguliwa kuwa Waziri ni kama amepoteza akili hivi! Yaani kweli anakuja mtu na ndege bure, mimi nikatae kuchukua? Lakini akija na masharti ya kipuuzi kwamba nakupa ndege hizi bure, nipe mlima Kilimanjaro, nitakataa. Kwa hiyo, ndiyo hicho! (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa tuliyofanya *ATCL* ni kuondoa Bodi iliyopita, kuondoa *Management* iliyopita, haikuwa nzuri hata kidogo, lakini vile vile kubaini uozo uliopo na uozo huo tumepeleka *TAKUKURU*.

Pili, kazi yetu imekuwa ni kusafisha *balance sheet* ya *ATCL*. Kazi hiyo tumefika mbali sana na tatu ni kuleta *proper financial management* ndani ya *ATCL*. *ATCL* wana ndege

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI]*

moja, lakini leo hii ndiyo unaona ufanisi wa ATCL. Ile ndege inakwenda *Comoro*, Bujumbura, Mtwara, tena *punctual* na wameanza ku-*make profit*. Sasa tumesema *this is good*, hapo ndiyo tunataka ku-*invest*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya muda siyo mrefu tunaleta *CRJ* ambayo ni *Jet* na tumeshaanza mchakato wa kupata *embraermbili*. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tutaleta bajeti hapa angalau pesa ndogo ya kuwasaidia vijana muipitishe basi badala ya kusema maneno mengi kuhusu *ATCL*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilisikitishwa sana na maneno yaliyokuwa yanatolewa hapa Bungeni. Watu tunasahau, hili ni Bunge jamani, tunasikilizwa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara ya ndege na ubora wa ndege unasimamiwa na vyombo vilivyothibitishwa Kimataifa. Kwa upande wa Tanzania tuna *TCAA* ambayo inasimamiwa na *IKL*.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana, Mbunge wa Tanzania anasimama Bungeni tena bila kujali, tena Kimipasho mipasho tu, "ndege ile inavuja." (*Kicheko/Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *it is so surprising!* Yaani unasema *statement* hiyo bila kujua *implications* za tamko kama hilo kwa dunia ya Kimataifa, ni aibu kubwa kwa Bunge hili. Angesema mtu kama pengine Mheshimiwa Nundu ningelewa, kwa sababu ndiye pekee ndani ya Bunge hili ni *Aero Space Engineer!* Ndiye anayejua mambo ya *Aero dynamics*. Lakini naelewa *entry qualifications* zetu hapa Bungeni ni kujua kusoma na kuandika. Jamani, haya mambo mengine tuwaachie watu wengine. (*Kicheko/Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ndege ile tunayotumia Q400 inaruka futi 21,000 mpaka 23,000 juu angani. Kama kweli inaweza kuvuja, italipuka, kwa sababu ni *pressurized*. Ni sayansi ndogo tu! (*Kicheko/Makof!*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI ]

Mheshimiwa Naibu Spika, aah, niliache hilo! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vilevile nielezee tu kuhusu miradi ya reli. Mimi nimekuja kuamini kwamba engine Waheshimiwa Wabunge hawana taarifa sahihi za miradi ya reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna miradi miwili ya reli hapa. Mradi wa kwanza wa reli ni mradi amba Serikali yetu ilikubaliana na Serikali ya Rwanda mwaka 2005, mwezi Mei kujenga *standard gauge railway* kutoka Isaka kwenda Kigali. Mwezi Septemba, 2005 Burundi ikatu-join na kutaka nayo kujenga *standard gauge railway* kutoka Keza kwenda mpaka Msongati. Huo ni mradi wa kwanza. Lakini kutokana na busara ya Kiongozi wetu wa Kitaifa hapa akasema, sasa mzigo ufike kutoka Kigali kuja Isaka, halafu itokee *trans shipment* kuingiza kwenye *gauge* yetu ya mita, hapana. Tujenge pia kutoka Isaka kuja Dar es Salaam *standard gauge railway*. *This is the distinct project, inatofautiana hii reli yetu ya kati.*

Sasa tunachanganya *feasibility* nyingi, inalaumiwa Serikali, tunaionea bure Serikali. *Feasibility* zote hizi zinazofanyika, tatu zilizotokea zote zimefanyika kwa mamlaka ya nchi zote tatu. Tanzania inalaumiwa kwa kitu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, *studyya* kwanza iliyofanywa na *DBI International*, hawa *Dorchebard International* walifanya *feasibility* toka Isaka kwenda Kigali na Msongati. *Feasibility* ya pili imekuja kufanya na hawa *Burlington Northern Santa Fe (BNSF)* wa Marekani. Nao wakafanya kutoka Dar es Salaam kuja Isaka. *Study* ya tatu ni ya *Cana Rail analing* hiyo ni *dittle design*.

Waheshimiwa Wabunge huwezi ukajenga reli kwa kuweka kamba. *Studies* lazima zifanyike! Hizo *studies, study* ya mwisho ya *Cana Rail* haijatoka. Mawaziri ndio tunakutana mwezi ujao Kigali na *Headquarters* wa Sekretarieti ya Ujenzi ile iko Kigali. Sasa Tanzania imechelewesha wapi huu mradi? Ni maneno tu!

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI]

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mradi wa pili wa reli ni *central line* yetu wenyewe, kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma, Mwanza, Mpanda, Singida, Tanga mpaka Arusha. Hiyo ni *central line railway* tumedhamiria nayo kuiboresha. Tukishakamilisha *standard gauge* tutakuja kurudi huku. Tunachofanya sasa hivi ni kuhakikisha tu kwamba reli zote kuu kuu, nyepesi, tunazibadilisha. Tumeshafikisha kilometra 525 *under difficult financial conditions*. Lakini badala ya kupongezwa, ni maneno mengi tu kutulalamikia. Mmetupa hiyo hela ya kuweza kwa mfano kukarabati reli kilometra 1270 tunazohitaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini tumefanya hivyo, tunajenga madaraja, tunakamilisha madaraja matatu sasa hivi kati ya Kintinku, Bahi; *three huge bridges*. Mwaka huu wa fedha Bunge hili limetupitishia pesa kuweza kukarabati madaraja mengine 25, tunaendelea vizuri sana. Tunanuna vichwa vya treni na mabehewa ambayo ni *adjustable*, yanaweza yakatumika kwa *meter gauge* na kwa *standard gauge*, yote ni kwamba tuna-envisable baadaye na tutakwenda kwenye *standard gauge*.

Gati namba 13 na 14 nilisemee kwa kifupi sana, naomba hili suala lisiongelewe tena hapa Bungeni, nitawaelewa vibaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, *bath* namba 13 na 14 was *ill conserved from the beginning* kwa sababu *liligubikwa* na maslahi finyu ya kifisadi. Naeleza kwa nini. Leo hii tumemaliza kufanya *hydrographic and topographical surveys*, ukichimba chini ili meli kubwa ziweze kupita pale, inabidi uondoe miundombinu yote ya mafuta pale chini. *Expenses* zinapanda kutoka Dola zilizokuwa nyingi za 523 kwenda mpaka Dola milion 700. Itakuwa *most expensive baths* katika dunia hii. Lakini siyo hivyo tu, ukiingiza meli kubwa pale, kipenyo cha kugeuka kinahitaji mita 600 siyo mita 440 zilizopo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ni kengele ya pili hiyo.

**WAZIRI WA UJENZI:** Ah, basi Mheshimiwa. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe. Dakika kumi hizi ni kidogo sana. Sasa wakati Wenye viti wetu wakijiandaa kuja kuhitimisha hoja zao, kufuatana na kanuni ile bora ya uendeshaji wa shughuli za Bunge, nilipomkatiza Mheshimiwa Profesa Muhongo, Waheshimiwa Wengi mlisema aah! Nime-*take note* ya jambo hilo. Kwa hiyo, kwa dakika zile ambazo meza huwa inayo, naomba nimpe dakika zisizozidi dakika tano ili aweze kumalizia alichokuwa anakiongea. Sote tuziangalie hizo dakika tano. Mheshimiwa Profesa Muhongo!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, hili suala la kwamba Watanzania hawashiriki kwenye faida za rasilimali zao, kuna Mbunge pale kasema, kuna wengine nao walikuja kwenye midahalo, nashukuru Mheshimiwa Lissu alipata jibu lake pale pale kwa *data*. (*Kicheko/Makof*)

Sasa nataka niende kwenye *point* kuonyesha Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wanaonisikiliza kwamba watu walioshika maeneo mengi ambaao wameshindwa kuyaendeleza wanaofanya hatupati fedha ni Watanzania. Kwa hiyo, mtu asiwasilishe mambo ya kibaguzi na kusema kwamba ni wageni na huku mtu huyo huyo anafanya biashara na wageni lakini anasema ni wageni.

Sasa nimekuja hapa nimefyatua watatu tu kwa sababu muda hautoshi. Mtu wa kwanza mwenye eneo kubwa kabisa nchini hapa, anaitwa Al-Hussein Juma Danani, ana Kampuni 19, ana eneo kilometra za mraba 25,589.02 yaani kilometra za mraba elfu ishirini na tano mia tano themanini na tisa nukta sifuri mbili. Kama hujui *square kilometers*, nchi ya Israel ina Kilometra za mraba 20,770. Huyu mtu ana Israel nzima.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI]*

Kwa wale ambaio wamekwenda Kuwait; Kuwait yote ile ina kilometra za mraba 17,818. Huyu mtu amezidi Kuwait nzima. Nchi ndogo ya Swaziland ina Kilometra za mraba 17,364, huyu mtu ana ishirini na tano. Ukichukua *Serengeti National Park*, huyu mtu ana Serengeti 1.7. Kwa hiyo, watu msipotoshwe na mambo ya uzawa, sijui Watanzania hawashiriki, wewe mimi nakupatia, hapa takwimu zinaonyesha Watanzania ndio wanazo.

Wa pili ni Hassan Ahmed Abdulbar Kampuni 19.

**MBUNGE FULANI:** Ni Wahindi!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Usiwe mbaguzi, ni Watanzania! (*Kicheko/Makofii*)

**MBUNGE FULANI:** Wamezaliwa hapa hapa!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mbona mlimsikiliza Mandela kwamba hamna ubaguzi? Usiwe mnafiki! Haya, kama ni Wahindi, naendelea, sikilizeni. Haya huyu ana 14,238 anaizidi nchi ya Gambia, anaizidi Jamaica, Mkoa wa Kilimanjaro anao 1.1. Haya, nilisema watatu tu. Wa tatu ni Regnald Mengi, ana Kampuni tano, eneo lake ni kilometra za mraba ni 3,883.18, yaani anaizidi Mauritius...

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**NAIBU SPIKA:** Naomba utulivu jamani, tuko Bungeni! Naomba utulivu.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Anazidi Commoro. Kwa sababu yeye anatoka Moshi; Mji wa Moshi una Kilometra za mraba 43. Huyu ana Miji kama hiyo 89. Kwa hiyo, ndugu zangu hii inathibitisha kwamba rasilimali ni sisi wenyewe. (*Kicheko*)

Sasa nimalizie kwa kusema kwamba sisi Wizara ya Nishati na Madini ndio tumepewa majukumu ya kutoa umeme utakaozalisha uchumi wa nchi. Nilitaka kumalizia kwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO ]

kusema kwamba mambo tunayoyafanya Serikalini, siyo ya kubahatisha. Sasa hivi uchumi wetu unakua kwa 6.7% mpaka 7%. Ukipika 8% ambapo labda ni mwakani, tutapunguza umasikini. Lakini tukitaka kufuta umasikini, lazima uchumi wetu ukue kwa zaidi ya asilimia 10 na ndiko tunakotaka kwenda huko. Vile vile ili uchumi ukue, ni lazima tuwe na umeme wa uhakika.

Waheshimiwa Wabunge na Watanzania mnaonisikiliza, ni kwamba tunaongeza umeme mara mbili. Sasa hivi uwezo wetu wa kuzalisha umeme ni *Megawatt 1,501.24*, lakini tutafika 3,000 mwaka 2015. Juzi kontena imetoka Marekani yenye *turbines* za kuja kufunga kinyerezi. (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Muhongo. Ahsante sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Tundu Lissu nimekuona. Kama una neno nitakupa nafasi mwishoni kabisa. Kwa sababu ya muda tulionao, naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu Mheshimiwa Peter Serukamba. Mheshimiwa Peter Serukamba - Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, muda unaufahamu, lakini ukiwa *brief* tutakushukuru.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA (MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuhitimisha hoja yetu tulioitoa jana. Kwa sababu ya muda nawaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba sitaweza kutaja watu wote waliochangia, lakini itoshe kusema Kamati yetu ya miundombinu imepata michango kwa maandishi na kwa kuongea humu Bungeni watu 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwanza nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi niweze kumalizia hoja yetu. Lakini pia jambo moja ambalo

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. PETER J. SERUKAMBA (MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU ] ningependa niliseme, nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mwakyembe. Ukiangalia kwenye *gallery* yako toka tumeanza kusikiliza hoja hapa Bungeni za Wenyeviti wa Kamati na ningependa Wenyeviti wa Kamati wa-note ni Wizara peke yake imeleta watu kusikiliza maoni ya Kamati. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo kwangu mimi ni kubwa kwamba wanachukulia kwamba shughuli ya Kamati ni shughuli muhimu sana na ndiyo maana wameleta watu wote wa Wizara kusikiliza. Ningetamani ingefanyika hivyo katika Wizara ya Ujenzi lakini haikufanyika, ningetamani ingefanyika hivyo katika Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia lakini haikufanyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nitaanza kujibu machache kulingana na muda ulivyo. Ngoja nianze na suala la Bandari. Naomba nianze kwa historia kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya *Kemondo Bay* ilijengwa mwaka 1971, Bandari ya *Bukoba* ilijengwa mwaka 1945, Bandari ya *Musoma* ilijengwa mwaka 1966. Bandari ya *North Mwanza* ilijengwa mwaka 1950, Bandari ya *South Mwanza* ilijengwa mwaka 1939, Bandari ya *Nansio* ilijengwa mwaka 1954; Bandari ya *Dar es Salaam* mara ya *mwanza* ilijengwa mwaka 1905, ikajengwa tena mwaka 1950; *KGO* ya *kwanza* ilijengwa mwaka 1965; *Bath* ya 8 mpaka ya 11 ilijengwa mwaka 1972 mpaka 1976 wakati tunajenga *Reli* ya *TAZARA*. Bandari ya *Itungi* ilijengwa mwaka 1975, Bandari ya *Mtwara* ilijengwa mwaka 1954, Bandari ya *Kigoma* ilijengwa mwaka 1910 na Bandari ya *Tanga* ilijengwa mwaka 1889.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeamua kusema haya kwa sababu Kamati inaposema kwamba *speed* yetu siyo nzuri, hakuna tunayemwonea wivu hata kidogo. Ukiangalia wakati Bandari hizi zinajengwa, *population* ya Tanzania ilikuwa ni ndogo, uchumi wa Tanzania ulikuwa ni mdogo, lakini leo *trade* imekua, *population* yetu imekua na uchumi wetu umekua. Kwa namna yoyote ile, hatuna maelezo kwa nini

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. PETER J. SERUKAMBA (MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU] hatuanzi kujenga bandari nyingine. Tunaweza kusema lolote, lakini maelezo hayatoshelezi. (*Makofii*)

Bandari ya Dar es Salaam ni kitovu cha uchumi wetu. Kama leo Wabunge tukiambiwa Bandari ya Dar es Salaam siyo muhimu, mimi nitakubali. Lakini mimi bado ninaamini, bado Bandari ya Dar es Salaam tunayo nafasi ya kuipanua. Tunaweza tukajenga gati ya kwanza mpaka ya saba na tunaweza tukajenga gati ya 13 mpaka ya 14. Inaonekana ni gharama kubwa, lakini maendeleo yana gharama kubwa. (*Makofii*)

Tunataka kwenda kujenga pale Bagamoyo. Naishukuru Serikali imeingia mkataba na *PPP* kujenga kwa Dola bilioni kumi. Dola bilioni kumi siyo nyingi sana, lakini Dola milioni 700 ni nyingi sana. Mimi hapa napata mashaka kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, miltupa safari juzi kwenda Malaysia. Jambo kubwa tulilojifunza na ambalo ningependa Waheshimiwa Wabunge tujifunze, unapotaka kuongoza biashara, anayekuja kufanya biashara lazima tuijandae, atapata faida. Lakini wewe ambaye unataka kufanya naye biashara, lazima ujue unataka kupata nini? Kama unadhani anayekuja kuwekeza atapata fedha nyingi, wewe ukaona vibaya, basi fanya mwenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekwenda Bagamoyo. Bagamoyo pale wanatuambia kina kikubwa cha maji Bagamoyo ni mita tano, kina kidogo ni mita tatu. Pale kuna Chuo cha Mbegani na maeneo mengi sana. Kwa hiyo, ukitaka kujenga Bandari leo pale Bagamoyo, kwanza unaanza kuchimba kina kikubwa. Ukianza kuchimba kina kikubwa, maana yake kufika hizo mita 16, siyo chini ya Dola milion 400. Hii ni *choice* kama nchi, lazima haya wayafanye. Naomba watu wa Serikali tuyafanye, Watanzania wanataka tufanye kazi; wametuamini, tuna uwezo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Tanga imejengwa mwaka 1889. Mimi naipongesa *TPA* na Wizara,

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. PETER J. SERUKAMBA (MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU ]  
ime-compensate pale Mwambani, imelipa pesa nyingi sana.  
Lakini mpaka leo sioni mradi gani unaanza lini? Sisi tunajua  
yako mengi yanafanyika. Shida yetu, nami niwaombe watu  
wa Serikali kwamba tunataka jiwe la Msingi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua nikitoa mfano huu  
watu wanakasirika. Juzi ameingia Rais Uhuru, hata mwaka  
haujawkisha ameshaweka jiwe la Msingi. Leo anajenga Reli  
ya *standard gauge* kutoka Mombasa kwenda Nairobi na  
baadaye anakwenda huko, ameingia juzi. Tulikwenda wote  
kutafuta pesa za kujenga Bandari, lakini wao wameshamaliza  
Bandari ya Mombasa hizo gati mbili. Kwa hiyo, nasema  
ningetamani Serikali, ile miradi ambayo ni mizuri ambayo siyo  
ya kifisadi, tunaitaka iwe mizuri. Maana haiwezekani wakati  
tunasema mradi huu ni mbaya kwa sababu ni wa kifisadi,  
mzuri uko wapi? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Kigoma  
imejengwa mwaka 1910. Hata ukienda kwenye *depreciation*  
kwa wale ambao wamesoma *Accounting*, lazima uirudia hii  
bandari leo. Hizi Bandari, kwa mfano ya Tanga, Bandari ya  
Mtwara, Bandari ya Musoma, bandari zote ukiangalia miaka  
yake unaona kwa *depreciation* tu, wakati umefika wa  
kuzijenga. Sisi kwenye mapendekezo yetu tumeiomba Serikali,  
kama Serikali haina pesa tuwashirikishe watu binafsi/Sekta  
binafsi. Siyo lazima iwe ya ndani, hata ya iwe ya nje. Wenzetu  
wanafanya, kwani sisi hatuwezi kufanya! (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala Reli Mheshimiwa  
Waziri amelisema vizuri sana. Ni kweli *study* ziko tatu. Ni kweli  
wanafanya kazi kubwa, wanatengenezesha sasa  
*locomotives* zaidi ya 20, nampongeza Mheshimiwa Waziri Dkt.  
Mwakyembe. Wanatengeneza mabehewa, na kwa kweli  
wamekuta hali ya reli ni mbaya sana. Sisi tunachosema kwa  
Serikali, kwa hali ya Reli ilivyo, tusipowekeza sana, tutakwenda  
taratibu. Reli hii imekaa miaka 100. Tukiitegemea Reli hii  
iliyokaa miaka 100 mpaka imeharibika, tunapeleka fedha  
kidogo kidogo, tutalaumiana tu. Lakini wote humu ndani  
tunaamini reli ni kitu muhimu sana kwa ajili ya maendeleo  
yetu. Nchi zote zilizoendelea wanatumia reli. (*Makof*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. PETER J. SERUKAMBA (MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU ]

Hapa sisi kama Kamati, hatum-target Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwakyembe wala nani, tunachosema Serikali tulipe kipaumbele Shirika la Reli, tuwape fedha za kutosha ili tujenge reli yetu. *Study zipo; feasibility study* zimeafanywa, *design* zimefanywa; narudia tena, ningeomba kwa kazi kubwa mnayofanya, kabla hatujaondoka mwaka 2015, na sisi tuwekejiwe la msingi la kuanza *standard gauge*. Hili ndiyo ninalowaomba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala la barabara za Dar es Salaam. Mheshimiwa Waziri hapa amesema kazi ni kubwa. Inafanyika kazi kubwa sana ya barabara, hata mimi naunga mkono kwamba kazi kubwa inafanyika. Lakini bado hali ya Dar es Salaam ni ngumu. Kama tukikaa kwenye Bunge hili tukasema hali ya Dar es Salaam ni nzuri, jamani watu wanakaa barabarani masaa manne mpaka matano. Ukiangalia hizo *measure* tunazoambiwa za sasa, ukijenga *flyover TAZARA*, maana yake watapita vizuri *TAZARA*; ukifika Buguruni kwenye *junction* hupiti. Ukiengena *flyovers TAZARA*, maana yake pale Chang'ombe huendi. Ukiiona nchi zote ambazo wamejenga *flyovers*, zimeungana. Lazima ujue unapoyanyanya magari haya unakwenda kuyaweka wapi. (*Makofii*)

Kwa hiyo, ningeomba suala la Dar es Salaam, suala la *feeder roads*, Dar es Salaam leo ukijenga *outer ring roads*, yaani barabara pete zote tukiamua kuzijenga na za mitaani, hali ya barabara Dar es Salaam itapungua. Kama Kamati, tumetoa mapendekezo kwamba kwa Dar es Salaam twende nje ya bajeti, tutafute fedha, tukope ili tuweze kuokoa hali ya Dar es Salaam. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni madeni ya barabara. Madeni ya barabara ni makubwa sana. Ningeomba Serikali watafute fedha kwa ajili ya haya madeni. Lakini hili la madeni, mimi nataka niliongelee, na hili ni la kwetu Waheshimiwa Wabunge. Ukienda kwenye Kitabu cha Bajeti, Mwandiga – Manyovu, Shilingi bilioni moja kilometa 60. Kasulu - Kigoma Shilingi bilioni mbili.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. PETER J. SERUKAMBA (MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU ]

Kwa hiyo, kila sehemu tumewekewa Shilingi bilioni moja moja, bilioni mbili, bilioni tatu. Kwa ambaye amesomea *Engineering*, ukitangaza kilometra 50, una Shilingi bilioni moja, huwezi kulipa hata asilimia 15 ya *advance*. Huwezi! Maana yake tunapitisha barabara, na hii ni kazi yetu Wabunge, lakini kesho tunaanza kupitisha madeni. Kwa hiyo, ningesema kupanga ni kuchagua. Waheshimiwa Wabunge, tuamue sasa, tuanze na barabara ipi, tuishie na barabara ipi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wenzetu barabara nydingine wameweka *Road Toll*. Ukimtafuta mtu binafsi ajenge leo kutoka Dodoma mpaka kwenda Dar es Salaam, utampata. Kwa hiyo, fedha ambazo ungezitumia kwa ajili ya kujenga Dar es Salaam, ukazitumie kwenye barabara zetu za Tabora, barabara za *feeder roads*, ukazitumie kwenye afya, ukazitumie kwenye maji. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya *Hansard* kuchukua vizuri, jielekeze kwenye *mic*.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA (MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kusema barabara wote tunazitaka, lakini maisha mengine lazima yaende. Kama tukiamua tunajenga barabara zote, na baada ya miaka mitatu barabara unairudia tena, hatukuwekezi kwenye reli, bado hatuitendei haki nchi yetu. Barabara ya Dodoma - Morogoro imejengwa mimi niko Mbunge hapa. Leo barabara hii imekwisha. Barabara ya Dar es Salaam - Chalinze, wamekuja *NSSF* pamoa na Wamalaysia wanaomba wajenge *City Highway*, leo ni mwaka wa tatu hatufanyi maamuzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee juu ya ugawaji wa fedha za Serikali. Wizara ya Ujenzi pale ukipeleka leo Shilingi bilioni 200, wanachofanya, wanagawa fedha kwa *pro-rata*. Ukipawa kwa *pro-rata* maana yake ni kwamba wa Shilingi tano unampa Shilingi moja; wa Shilingi saba unampa Shilingi moja, matokeo yake hamna anayerudi kazini. Lakini nilidhani na tumeshauri kama Kamati kwamba fedha ikija Shilingi bilioni 100, walipe hata Wakandas kumi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. PETER J. SERUKAMBA (MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU] waende wakafanye kazi. Zikija unawalipa wengine. Ukimpa mtu a *lump sum* money, una hakika harudi mpaka miezi mitatu au miezi minne. Lakini tunawalipa kidogo, matokeo yake madeni hayaishi kila siku. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *Terminal III* nashukuru Waziri amesema wanakwenda vizuri. Ilikuwa nia yetu, maana tulikutana na Waziri wakatuambia kinachoendelea kule *Terminal III*. Kwa hiyo, sisi tumefurahi kwamba sasa *Terminal III* tumefika pazuri, tunawapongeza sana watu wa Wizara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, iko Barabara ya Nyakahura - Rulenge - Mwarugalama, ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Lakini barabara hii Mbunge wake amefanya kazi moja kubwa sana. Nimeamua niichukue hii kuisema kwa sababu Mbunge amefanya kazi ambayo wengi hatuifanyi.

Mheshimiwa Mbunge kwa kupitapita kwake amekwenda *ADB*. *ADB* wamesema kwamba barabara hii kwa sababu inaunganisha Tanzania na Burundi, tutaijenga. Tunachoomba ni Wizara ya Ujenzi ipeleke barua ya kuiomba *ADB* waijenge barabara hii. Hatupeleki barua, leo mwaka wa tatu. Tatizo ni nini? Kama hatutaki *ADB* wachangie, tuijenge kwa hela za Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mizani; ukisoma kwenye *BRN*, wamesema watajenga *Weight Motion Initiative* wapime. Mimi ningeomba na Mheshimiwa Waziri amesema vizuri sana, na ni muhimu sana na tumesema kwenye Kamati. Tunaomba jamani tuhakikishe magari yetu hayatoki Bandarini kabla hayajapimwa. Maana kama ni mzigo wa *transit*, ukishaweka mzani bandarini ukaupima, huna sababu ya kupima mwingine kwa sababu hakuna sehemu ambako watashusha au wataongeza mzigo. Kwanza mzigo wenyewe una *seal*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la masafa (*TTCL*), namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, amelisema. *TTCL* pamoja na kuwapa masafa, lingine kubwa ambalo

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. PETER J. SERUKAMBA (MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU] tumewaomba Serikali litekelezwe, Serikali inadaiwa sana na *TTCL*. Shirika la kwetu, tunaotumia huduma ni sisi. Ukichukua ile orodha ya wanaodaiwa na *TTCL* ni Idara za Serikali na Wizara. Nami namwomba Waziri sasa awaambie watu wa *TTCL* kwamba umefika wakati hata Wizara na Idara zikatiwe huduma. Wakikatiwa huduma watalipa. Ukienda kwenye vitabu vya Bajeti, pesa kwa ajili ya kulipia simu zipo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la Minara; Waheshimiwa Wabunge wote wamesema humu ndani, na kweli wanataka minara. Niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge tuamue sasa, tunapokuja kwenye Bajeti mwaka kesho tutafute fedha, tujinyime ili tuweze kupata minara. Lakini tukitaka kutegemea Makampuni haya, hatutakwenda ksa spidi tunayoitarajia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Meli ya Liemba, ameisemea vizuri sana rafiki yangu Mheshimiwa Aeshi. Jamani umefika wakati, ukiona ile meli imekaa zaidi ya miaka 100, nawaombeni Wizara tutafute namna tutakavyoweza kufanya ili tuihudumie vizuri. Lakini pia lazima tusikubali kupoteza mapato. Kwenye Ziwa Tanganyika kama alivyosema Mheshimiwa Keissy, tunachokitegemea sisi ni Liemba. Kwa hiyo, ningeomba sana tuweze kuishughulikia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wamesema ni suala la watu wengi sana kukaimu. Ukienda *SUMATRA* wanakaimu, *TIA* wanakaimu na Bandari wanakaimu. Mimi ninaamini mtu anayekaimu hawezi kuwa effective ambavyo tulitarajia. Kama wanafanya kazi nzuri, naomba muwape mikataba. Kama hawafanyi kazi nzuri, tuwaondoe. Maana haiwezekani mtu anakaimu miaka miwili mpaka mitatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati naongelea suala la barabara, niliamua kutoa mfano wa barabara nyiningine ambayo wakati wa Uhuru ndiyo ilikuwa inatumika sana. Ni barabara wanayoita ya Musoma - Busekela - Musoma, ilikuwa ina-cover Wilaya zote zile za Serengeti, Musoma Mjini kuja mpaka Bunda. Ina kilometra 80. Barabara hii toka wakati

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. PETER J. SERUKAMBA (MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU] wa Mwalimu Nyerere! Sasa umefika wakati, kama tumeingia siku ya pili tukajenga Chato, tunashindwaje barabara hii ya Baba wa Taifa aliyetafuta Uhuru? (Makof)

Mheshimiwa Amina Makilagi amelisemea vizuri sana. Mama yule aliliongea mpaka akataka kulia hapa ndani, kwamba angalau kwa barabara hii, na kwa kweli jamani tukubaliane; yule mzee wetu Baba wa Taifa angeamua ajipendelee kwanza Musoma, maana yake angeondoka Musoma amemaliza kila kitu. (Makof)

Mhehimiwa Naibu Spika, barabara ya Ndundu - Somanga. Waziri amesema Ndundu -Somanga bado kilometra 14. Lakini hatuna majawabu kwenye barabara ya Ndundu - Somanga. Haiwezekani kilometra 60 tuzijenge kiwa miaka nane. Wakati anaongea Mheshimiwa Pindi Chana kwamba kuingla Dar es Salaam njia ni moja, nikajua dada yangu Mheshimiwa Pindi Chana amesahau kwamba kuna Watanzania wengine wanatoka Lindi na Mtwara nao wanaingia Dar es Salaam, hawapitii Ruvu. Kwa hiyo, njia za kuja Dar es Salaam siyo Ruvu peke yake. Kuna watu wa Lindi na Mtwara, nao wakuja kwa kupitia njia yao. Ambapo kwa kweli ningeomba, Ndundu - Somanga tuimailize ile barabara. (Makof)

Barabara hii imejengwa toka wakati wa Mwinyi; Mwinyi akafanya kipande chake akamaliza, haikwisha; akaja Mzee Mkapa akafanya, haikwisha. Haiwezekani na Mheshimiwa Rais Kikwete aondoke hajamaliza Ndundu - Somanga. Ningeomba tujitahidi tuwe tumemaliza Ndundu - Somanga. Kamati yetu tulikwenda juzi, Mheshimiwa Waziri Mwakyembe alitupeleka kuangalia Bandari ya Lindi, ukipita Ndundu - Somanga pale unakaa zaidi ya masaa mawili, ambayo ni sehemu ndogo tu haizidi kilometra 50. Kwa hiyo, niwaombe watu wa Wizara ya Ujenzi kwamba suala la Ndundu - Somanga walishughulikie kwa haraka sana. (Makof)

Lingine ambalo Mheshimiwa Waziri alisema barabara zetu, anasema hazivimbi. Mimi ningeomba watu wa Wizara

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. PETER J. SERUKAMBA (MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU] ya Ujenzi, watu wakileta mawazo, tuyafanyie kazi. Haiwezekani!

Kwa wale ambao ni Mainjinia wanajua, *Abstract-concret* zote duniani wanafanya, ndiyo zimeanza kufeli Tanzania. Tumeona hii hapa ime-fail, ile ya *Kilwa Road* ime-fail. Huku kwenda Iringa kuna sehemu ime-fail. Lazima tuijulize, kama tumeamua kwenda barabara za *standardza Abstract Concret*, maana yake lazima tuijulize kwanini zinafeli? Aidha *design* ina matatizo ama usimamizi siyo mzuri. Kwa hiyo, ningeomba haya nayo tuyaa ngalie kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningesema tuangalie na Ma-engineer watuambie, kuna nini? Aidha, kama kuna *design failure* watuambie, wafanye uchunguzi. Hatuwezi kusema tu zinazoharibika hata ikiwa ni 5%, bado tumetumia fedha nyngi kama nchi.

Kwa hiyo, ningeomba sana watu wa Wizara ya Ujenzi na Kamati inaomba, tunajua wanafanya kazi nzuri, lakini haya matatizo yanayotokea wayafanyie uchunguzi wa kutosha kwanini yanatokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu juzi alikwenda Kigoma. Iko barabara kutoka Mwandiga kwenda Kagunga. Ni matumaini yangu watu Wizara ya Ujenzi walimsikiliza Waziri Mkuu, na Mheshimiwa Rais alikuja akasema hayo hayo, lakini barabara ile mpaka leo hatujawekewa fedha. Kwa kweli tukijenga barabara ile siyo tu kwamba tunapeleka watu kule Gombe na Mahale kwa maana ya Gombe, lakini tutakuwa tumepeleka ukombozi. Kuna watu wanaokaa Mwamgongo na Kagunga toka Uhuru hawajawahi kuona gari. Tukifanikiwa leo tukawapeleke gari, tuna hakika hali yetu itakwenda vizuri sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kwenye barabara, barabara zote za Ukanda wa Tabora, zinasusua. Tatizo ni nini? Ukitoka Nzega kwenda Tabora, muda waliosema wangkuwa wamemaliza kazi muda umepita. Unatoka

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. PETER J. SERUKAMBA (MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU]  
Tabora unakwenda Urambo, Urambo unakwenda Kaliua kasi  
ya barabara ile ni ndogo sana.

Ukiangalia barabara ya kutoka Mbeya kwenda Chunya mpaka Rwanjiro barabara ile ingeshakwisha, lakini mpaka leo haijakwisha. Haiwezekani barabara tumesaini miaka mitatu inakwenda miaka mitano mpaka sita. Lazima tujiulize tatizo ni nini? Barabara za namna hiyo ziko nydingi, zimechelewa sana. Zimechelewa kwa sababu ya malipo. Kwa hiyo, ningeomba watu wa Wizara ya Fedha kama ni kukopa tukope ili tumalize barabara hizi tuweze kuanza na barabara nydingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nawashukuru Mawaziri kwa majibu yao, lakini tunaomba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupitia maombi yetu sasa ambayo tumetoa kuanzia pale namba 7.0, Maoni na Mapendekezo Mahsusini ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu, ukisoma yote haya mpaka namba 12 naomba Bunge lako sasa wakati wanapitia waweze kuyaona. Lakini kabla sijamalizia nilitaka niseme la mwisho la ATC, nilikuwa nimelisahau.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge hatulalamiki, Wabunge tunatamani ATCifanye kazi, hatuna shida nydingine. Mimi kesho nikiamka asubuhi nikakuta ATC wana ndege 100 wanaruka duniani nitakuwa wa kwanza kushangilia. Ndilyo nia yetu. Tuwaombe wafanye kazi zao hakuna ambaye analalamika, tunachotaka sisi wafanye. Nimalizie kwa kusema tunachotaka ni mambo yaende haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja sasa Bunge lako likubali maoni na mapendekezo mahsusini ya Kamati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
(*Makof*)

**MHE. JUMA S. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,  
naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu Mheshimiwa Peter Serukamba.

Waheshimiwa Wabunge, kwa ajili ya uendeshaji wa Bunge, ili tuelewane kwa madaraka niliyonayo nitaongeza muda wa nusu saa kwa sababu baadaye kidogo kutakuwa na maelezo ya Mheshimiwa Mbunge Paresso. Uongezaji huo wa muda hauna haja ya kuomba kibali cha Bunge kufuatana na Kanuni ya 28(8). Kwa jinsi hiyo, tutakwenda kwa nusu saa zaidi. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tumemsikiliza Mwenyekiti wa Kamati akihitimisha hoja yake. Kwa kweli kama siyo suala la muda, kwa uhitimisho huu ilistahili baadhi ya Wizara watupe maelezo tena kwenye baadhi ya maeneo. Kwa maana ya Bunge yaani kuna baadhi ya mambo kidogo yametuweka kwenye njia panda. Lakini kabla sijawahoji, kwa uongozi bora wa Bunge hapa na kwa kuwatendea haki Watanzania, yako mambo huwezi kuyaacha kiporo.

Kabla ya kuwahoji, kuna jambo limezungumzwa hapa likatuletea mkanganyiko mkubwa, hasa lile la kuacha mradi wa Dola millioni 700 ukaenda mradi wa Shilingi billioni 10. Hili ni jambo kubwa na zito. Kwa dakika zisizozidi tano, kwa mamlaka niliyonayo hapa Mezani nimwombe Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, aelezee hili jambo kwanini liko hivyo?

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwanza nilitaka tu kusema kwamba kwa kweli utaratibu wa kuwapa Mawaziri dakika 10 kuweza kucomment kwenye hoja ambazo zimeongeleta na Wabunge 50 kwa siku mbili *it is grossly unfair*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba nijibu sasa swalii lako kwamba kwanza Serikali haijasaini mkataba wowote wa Dola bilioni 10. Naomba tuweke hiyo *records straight* kuhusu *project* ya Bagamoyo ambayo ina miradi minne tofauti. Kuna ujenzi wa Bandari, kuna *project* ya EPZ,

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA UCHUKUZI ]

kuna ujenzi wa Reli na ujenzi wa Barabara. Tuko kwenye negotiations, hilo halijafanyika.

Pili, mimi naomba tu pengine Mawaziri tutaamua kutoa kauli za Serikali ili kufafanua masuala yaliyojitokeza hapa ambayo hatujapewa muda kujieleza, unakatishwa katikati na yanaelezwa mambo ambayo mmeshayafanya. Kwa hiyo, ni kiini macho cha ajabu ajabu tu, lakini *anyway*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema tu kwamba nitatoa kauli ya Serikali kwa mfano, kufafanua kuhusu miradi miwili ya reli ambayo inachanganywa na imeendelea kuchanganywa tu hapa; *studies* za mradi huu zinapelekwa huku, huku kumewekwa huku kwa hiyo, hatuelewi tunakwenda wapi.

Kwa hiyo, kauli ya Serikali itasaldia. Lakini vilevile ujenzi wa *bath number 13 and 14* ambao sisi tumeamua kuanza na tumeshaanza, sio kwa gharama za Dola milioni 523 lakini kwa nusu ya hiyo gharama kwa sababu hatuwezi kuendelea na ule mradi wa awali ambao utatutaka tuhamishe miundombinu ya mafuta, lakini vilevile kukata mita 160 za eneo la Kigamboni ili meli ziweze kugeuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana nilikuwa nasema, mradi huu uliasisiwa sio kwa kuweka mbele maslahi sana ya Taifa, uliasisiwa na maslahi binafsi yaliyokithiri kipimo kwa sababu *CCCC* ambao walikuwa na huo mradi toka mwanzoni pale na wakaondolewa na Mamlaka na *PPRA* kwa kujihusisha na rushwa huko *Philippines* nashukuru Mungu kwamba waliondolewa kwa sababu nimekuta Wizarani hawa jamaa wametuvuruga kweli!

Sasa hivi baada ya kufanyika *topographical* na *hydrographical survey* pale kuonyesha kwamba *it is impossible* *ku-implement* *hiyo project*, tumetakiwa kusaini kitu kinaitwa *Deed of Novation* kuhamisha huo mradi kutoka *CCCC* kwenda *CHEC* ambayo ni kampuni ambayo tumeiamini kufanya hiyo kazi. Imeshindikana kwa sababu *CCC* ni *holding company* ya *CHEC* kwa hiyo, tunakuja

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[WAZIRI WA UCHUKUZI]*

kukutana wataalamu wawakilishi wa CHEC tunakuta wote ni watu wa CCCC. Nimemwandikia Balozi wa China kwamba mzaha huo sitaki, na nimetoa muda kwamba kesho tarehe 20 ni mwisho wa hiyo *project* kuendeshwa na Wachina. Kwanza, hiyo siyo zawadi *it is a loan*, ni mkopo. Mkopo tunaweza kupata kokote kule. Kwa hiyo, ndio maana nilikuwa nasema huu mradi Mheshimiwa tutautekeleza, lakini siyo kwa misingi ile ya awali na nitaleta kauli ya Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Angalau hilo linatufanya tuwe mahali kidogo pa kuweza kuelewana. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mwakyembe. Hoja iliyotolewa na Mwenyekiti hapa Waheshimiwa Wabunge ni kwamba sasa mpokee na kukubali taarifa ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu pamoja na Mapendekezo na Maoni yaliyomo katika taarifa hiyo.

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu pamoja na Maoni na Mapendekezo yake yaliridhiwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Wote wameafiki taarifa hiyo. Nawashukuruni sana Kamati kwa kazi nzuri ambayo mmekuwa mkiifanya, mwendelee kufanya kazi hiyo kwa niaba ya Bunge zima na Watanzania na Wizara zote ambazo ziko chini ya Kamati hii ya Miundombinu, naomba mwendelee kushirikiana na Kamati yetu ili baadhi ya mambo haya ambayo bado yanahitaji kupigwa pasi vizuri zaidi na kuwekwa vizuri zaidi, yaweze kukaa vizuri.

Ni matumaini yangu kwamba ripoti ya mwakani itakuwa bora zaidi kuliko hii ya mwaka huu.

Kwa muda wetu ulivyo, naomba sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini - Mheshimiwa Victor Mwambalaswa. Anakuja Mwenyekiti Mwenyewe. Mheshimiwa tafadhalii, ukiweza kutumia kama dakika 20 nitakushukuru. Endelea Mheshimiwa Mwenyekiti. Ukizidisha kidogo siyo mbaya sana.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA (MWENYEKITI KAMATI YA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuja hapa kuhitimisha hoja ya Kamati yangu ambayo tulitoa jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru sana Wabunge wote ambao wameichangia hoja hii. Wabunge waliochangia kwa kuongea ni 45, waliochangia kwa maandishi ni Wabunge 11.

Nawashukuru sana wote, ahsanteni sana. Michango yenu ni mizuri sana, inaboresha sana kazi ya Kamati yangu. Ninawaahidi kwamba michango hii ambayo mmeitoa itasaidia sana kuimarisha na kuboresha kazi ya Kamati kwa kipindi kinachokuja. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Nailbu Spika, hoja ya kwanza ambayo Wabunge wengi wamechangia na siwezi kuwatamka kwa sababu ya muda, ni hoja ya (*REA*), Wakala wa kupeleka umeme vijijini kwamba ipewe fedha zote ambazo zimepangwa kwenye bajeti. Serikali yenye we imepanga mpango wa kuweka umeme vijijini kwa asilimia 30 by 2015.

Basi Serikali ihakikishe fedha zote ambazo zimepangwa kwa miaka miwili hii, hizo Shilingi bilioni 881 zipelekwe *REA* ili umeme uende vijijini. Serikali itii kwa sababu mwaka wa fedha uliopita Serikali haikupeleka hela zote ambazo zilikuwa zimepangwa kwenda *REA*. Sasa miaka miwili hii ambayo tumeamua kwamba lazima umeme uende vijijini *ku-stimulate* maendeleo ya wananchi wetu vijijini, basi Serikali itii katika bajeti hii na kuhakikisha kwamba fedha zote hizo Shilingi bilioni 881 zinaenda *REA* na kupeleka umeme vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, naomba hili liwe ni agizo la Bunge lako kwamba fedha zote zilizopangiwa *REA* ziende *REA* na Serikali itii bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili, Wabunge wengi wamechangia wanasema miradi ya kufua umeme mikubwa iliyopo kwenye *BRN (Big Results Now)* na mingineyo ambayo

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA (*MWENYEKITI WA NISHATI NA MADINI*)] iko nje ya *BRN* ipewe kipaumbele kikubwa katika bajeti ili *TANESCO* na nchi nzima iondokane na mitambo ya kukodisha ambayo inakula hela za nchi hii. Ifike mahali mitambo yote ya kukodisha iondoke. Kwa hiyo, miradi yote, yaani Mradi wa Kinyerezi I wa Megawatt 150, Kinyerezi II Megawatt 240, Kinyerezi III Megawatt 300, Kinyerezi IV Megawatt 600 na mingine ambayo iko nje ya hiyo Kinyerezi, kama Mradi wa Kilwa wa Megawatt 200; miradi hii yote Serikali ihakikishe inaipa kipaumbele ili by 2015 miradi hii yote iwe imekamilika, nchi iachane na aibu ya kukodisha mitambo ambayo inakula hela ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hii nayo ya pili nakuomba iwe ni Azimio la Bunge kwamba miradi yote ambayo iko kwenye *BRN*, iwe ya kufua umeme au ya kusambaza umeme, ya Dar es Salaam kwenda Chalinze, kwenda Tanga mpaka Arusha; ya kutoka Iringa kupita Dodoma kwenda Shinyanga mpaka Singida mpaka Shinyanga; kutoka Kahama, Nyakanazi, Kigoma, Mpanda mpaka Mbeya, mpaka Iringa; Makambako kwenda Songea; Somanga kuja Dar es Salaam ya usambazaji hiyo pamoja na hii ya ufuaji, basi yote ipewe kipaumbele kikubwa kwenye bajeti za miaka hii ili nchi iondokane na *Rain pause*. Naomba nayo hii iwe ni Azimio la Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyngine imeibuliwa hapa ni kwamba Serikali iendeleze kutoka vyanzo vingine kama mkaa wa mawe, joto ardhi, upepo na kadhalika. Iendeleze miradi hii katika kufua umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kiwira, Bunge limefurahi kwamba umepelekwa *STAMICO*. Pamoja na kupelekwa *STAMICO*, niliongea wakati natoa hoja hii juzi kwamba mradi wa Kiwira wakati Serikali inafanya juhudzi za kuurudisha Serikalini ili apewe *STAMICO*, Wizara ilifanya kuuza Mlima wa Kabulo. Mlima wa Kabulo ndiyo una makaa ya mawe mengi zaidi. Sasa huwezi kuipa *STAMICO* kwamba iendeshe, ifue umeme pale Kiwira wakati Mlima wenye makaa ya mawe mengi umemuuzia Mwekezaji mwingine. Kwa hiyo, tunasema Serikali irudishe mlima wa Kabulo

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA (MWENYEKITI WA NISHATI NA MADINI)] Serikalini na apelekewe TANESCO. Kama ni kuwachukulia hatua waliofanya mauzo haya kinyemela, itajua Serikali yenye. Kwa hiyo, nalo hili ni Agizo la Kamati yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri pia alisema hapa kwamba Serikali kuititia Wizara hii ya Nishati na Madini wameamua waunde Kampuni ya *Geothermal* ya kufua umeme kwa joto ardhi. Tunashukuru sana, hilo liendele. Lakini vitalu vyenye joto ardhi; unajua Kenya sasa hivi wanafua umeme wa joto ardhi karibu watakaribia Megawatt 1000 kwa sababu wao hawana vyanzo vingine kama sisi. Lakini vitalu vyatoto ardhi Kenya ni vichache kuliko Tanzania kwa sababu ya hili Bonde la Ufa kwetu sisi ni kubwa zaidi.

Kwahiyo, sisi tuna vitalu vingi zaidi vyatoto ardhi. Sasa kuna wajanja ambao wamejimilishwa vitalu hivyo vyatoto ardhi. Tunaiagiza Serikali, tunaiomba Serikali, tunaishauri Serikali vitalu vyote vyatoto ardhi virudi Wizarani vipewe Kampuni hii ambayo itakuwa inafua umeme. Kwa hiyo nalo hili ni Azimio la Bunge kwamba vitalu vyote kwa kampuni hii ambayo imeundwa ya kufua umeme kwa joto ardhi, vitalu vyote vyenye *potential* kubwa ya joto ardhi virudishwe Serikalini kwenye Kampuni hii ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kwamba uvunaji wa rasilimali gesi uwe wa wazi na uwanufaishe Watanzania wote. Hii iwe kwenye sheria, iende pamoja na bomba la gesi. Bomba la gesi litakamilika mwakani.

Wakati natoa hoja yangu nilisema kwamba Serikali kwa sababu ya ugumu tu wa kupata vibali vyatoto ardhi, hawakuajiri vijana Ma-engineer na Ma-technician wa kuangalia mabomba yanavyotengenezwa na yanavyojengwa. Hatujachelewa sana, Mradi vibali vimepatikana sasa hivi, wanaajiri. Hawa vijana ambao wameajiriwa waende China wakajifunze mitambo ya kuchakata gesi inayojengwa, wajifunze inayojengwa na pia wajifunze ujanja wa kuangalia bomba hili ili Kampuni hii ambayo sasa Serikali imesema inaianzisha Kampuni ya

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA (MWENYEKITI WA NISHATI NA MADINI)]  
GASCO ambayo itasimamia gesi iwe na wataalamu wa kutosha wa gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji wengi wameonesha kwamba wananchi wa Lindi na Mtwara hawana tatizo kabisa na gesi kutoka Mtwara. Tatizo lao ni ahadi za Serikali. Hiyo ya kwanza. Kama walisema watawapatia umeme wananchi wa Lindi wamewapatia? Kama walisema watawapatia barabara wananchi wa Lindi, wamewapatia? Kwa hiyo, nawaomba sana Serikali, ahadi ambazo inaagiza itemize. Wananchi wa Lindi na Mtwara wanachotaka ni vitu viwili. Cha kwanza, Serikali itimize ahadi; cha pili, elimu iendelee kuwaelimisha. Serikali iendelee kuwaelimisha kwamba, kwa mfano kuna hoja inapitapita huku kwamba mtambo wa kuchakata gesi utajengwa Dar es Salaam, wakati mtambo huu unajengwa Mtwara.

Kwa hiyo, Serikali iendelee kuwaelimisha wananchi wa Lindi na Mtwara kwamba rasilimali ya gesi ambayo tumeipata itawasaidia Watanzania kwa njia nyngi. Kutakuwa na viwanda vyatya *cement*, viwanda vyatya *mbolea*, kutakuwa na biashara za wananchi nyngi nyngi. Kwa hiyo, elimu kama hii iendelee kuwekwa kwa wananchi wa Lindi na Mtwara kwa sababu wao hawana tatizo. Tatizo ni uelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme hapa. Nimesema kwamba Kamati inaishauri Serikali kwamba uvunaji wa gesi hii uwe wa wazi na uwafaidishe Watanzania wote. Narudia, uwe wa wazi na uwafaidishe Watanzania wote kwa njia *mbalimbali*. Serikali ilisema hapa, Waziri amesema kwamba Kampuni ya *TPDC* na Kampuni itakayokuwa inashughulikia gesi Watanzania watanunua *share*, Watanzania wote watanunua hisa humu, sawa.

Pia tunaishauri Serikali, hata kama kuna Watanzania ambao wanatakiwa wapate vitalu vyatya gesi, wana uwezo au kwa pamoja au mmoja mmoja wenyewe uwezo kwa kufuata sheria wakaribishwe. Lakini ambacho Kamati inaishauri Serikali kwamba hapana, ni pale ambapo Mtanzania anatumia ujanja wake apate kitalu halafu akinadi ambayo ni rasilimali

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA (MWENYEKITI WA NISHATI NA MADINI)]  
ya Tanzania, hapo hapana. Hapo hatuishauri Serikali ifanyi  
hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kugawa na kuuza rasilimali za nchi ni kazi ngumu kweli. Hapa Serikali iliamaa kuuza nyumba za Serikali. Serikali ikaona ikuza nyumba kwa *tender* watanunua matajiri. Hawa Waswahili wenzangu watakosa hizo nyumba. Serikali kwa makusudi ikasema hapana, tuwauzie Waswahili ambao wanakaa kwenye nyumba hizo. Ni jambo zuri kabisa. Lakini tukasema tunapowauzia nyumba hizi kwa sababu ni rasilimali ya Watanzania wote, msiziuze na msizifanyie biashara. Alah lah lah! Wapi! Nadhani *forty percent* wameuza. Ndiyo maana kuna maghorofa *Oysterbay*, zilikuwa ni nyumba za chini, sasa kuna maghorofa. (Makofi)

Kwa hiyo, kuuza rasilimali za Serikali ni kazi ngumu sana. Kwa hiyo, ndiyo maana tunasema hata kwenye hii rasilimali yetu ya mafuta na gesi, kumpa mmoja mmoja hivi hivi ni ngumu sana. Yatafanyika yale yale ambayo yalifanyika kwenye nyumba. Tunaomba kama kuna Watanzania ambao wana uwezo kweli kweli kwa makundi au kupitia kampuni zetu, nao wapewe haki kushiriki kwenye uvunaji wa rasilimali zetu hizi. Naomba hii hapa nayo iwe ni agizo ni ushauri kwa Serikali kwamba iwe na uwazi zaidi. Nashukuru sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine, nasema *TPDC* na *TIPPER* zijenge uwezo mkubwa zaidi wa kuhifadhi mafuta kwa faida ya nchi. Mafuta yote yanayoingia nchini yapokelewe kwenye maghala hayo. Hapo sasa ndiyo *flow meters* ziwekwe kwenda kwenye makampuni ambayo yanauza mafuta. Pia *TIPPER* na *TPDC* waongeze uwezo wa bomba la kupokelea mafuta *SBM* ili liwe na njia nne badala ya njia moja ya sasa. Wenzetu wa Kenya wanafanya hivyo, na hii inasaidia sana kuzuia upotevu wa mafuta, inasaidia sana kuongeza mapato kwenye kodi. Kwa hiyo, naomba hilo nalo lichukuliwe na Bunge lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine, inasema wawekezaji wanaohodhi maeneo ya madini kwa muda

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA (MWENYEKITI WA NISHATI NA MADINI)]  
mrefu sana bila kuyaendeleza, maeneo hayo yarudishwe Serikalini wapewe wazawa kuyaendeleza. Wachimbaji wadogo wadogo ndio wawe wa kipaumbele. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, alitaja hapa Mheshimiwa Waziri, lakini mimi kwa uzoefu wa Kamati yangu na alisema Mheshimiwa Arfi kwamba Wilaya ya Mpanda asilimia 75 ya Wilaya ya Mpanda kampuni moja imeshika leseni za utafutaji wa madini. Kampuni moja! Asilimia 75 ya Mpanda! Wilaya ya Chunya ninapotoka mimi, ukubwa wa Wilaya ni kilomita za mraba 29,000. Kampuni tatu zinamiliki leseni za utafutaji madini kwa ukubwa wa kilomita za mraba 10,000 karibu nusu ya Chunya. Kampuni tatu! Mkoa wa Geita kampuni moja ya mzawa ambaye sasa hivi ametoroka, amekimbia nchini, inamiliki asilimia 75 ya Mkoa wa Geita. Mtu mmoja! Tunasema, Serikali mlifanya makosa kuwamilikisha watu namna hii. (Makof)

Sheria inatamka wazi wazi kwamba unammilikisha mtu eneo la kutafuta madini, unampa miaka minne. Akikosa madini, baada ya miaka minne anarudi Serikalini kwamba mimi nimekosa. Kwa hiyo, baadhi ya eneo anamrudishia Kamishna wa Madini, hawapi watu wengine. Lakini Serikali iliruhusu huyo mtu anarudisha eneo halafu anaandikisha kwa jina lingine. Anarudisha eneo anaandikisha kwa jina lingine. Kwa hiyo, miaka 10, miaka 20 anaendelea kumiliki eneo hilo hilo wakati Watanzania wanataka fedha sasa za maendeleo. Wewe unayetaka kumiliki maeneo kwa kufanya *speculation*, Watanzania wanataka fedha sasa. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Bunge linatoa Azimio kwamba Serikali kwa kufuata Sheria, Makampuni yote ambayo yanamiliki maeneo makubwa sana na hawajayafanya kazi, basi maeneo hayo yarudishwe kwa Kamishna wa Madini, wapewe wachimbaji wadogo wadogo na wazawa wengine ambao watayaendeleza sasa. (Makof)

Tunaishauri Wizara kwamba ianze mchakato huo kwa kufuata sheria na katika Kikao cha Kamati hii ya Bunge cha Bajeti, basi ripoti ya mchakato huu kwamba umefikia wapi,

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA (MWENYEKITI WA NISHATI NA MADINI)]  
iletwe kwenye Kamati. Kwa hiyo, hili nalo ni Azimio la Bunge.  
(Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine inasema Shirika la Maendeleo la Petroli (*TPDC*) na Makampuni ya Bima nchini hapa washirikiane kuandaa utaratibu wa Bima katika Sekta hii ya Gesi na Mafuta. Makampuni ya Bima hapa nchini yapo zaidi ya 20, hasa hasa makampuni ya Taifa *National Corporation* na Zanzibar *Insurance Corporation*, haya yapewe kipaumbele. Makampuni haya ya Tanzania yenye we ndiyo yatafute makampuni ya nje yaingia nayo ubia ili Sekta hii ya mafuta na gesi iwanufaishe watanzania katika Bima. Maana watu wanaweka Bima nje wakati kazi wanafanya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hilo nalo ni Azimio. Naomba kwa ridhia yako iwe ni Azimio lako la Bunge kwamba Serikali kuititia *TPDC* na Makampuni ya Bima washirikiane kuandaa utaratibu wa Bima zote za kwenye Sekta hii ya Gesi na Mafuta zifanyike hapa Tanzania. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati natoa hoja yangu jana nilisema Kamati ilitembelea Makao Makuu ya Shirika la Mafuta ya Petroli (*TPDC*). Pale kwa sababu lile jumba siyo lao ambapo wapo, chumba kinachohifadhi nyaraka muhimu za mitetemo, sijui za vitu gani, zote za gesi na mafuta, cha ajabu chumba ni kibovu sana, kinavunja na hizi nyaraka tunahitaji sana kwa vizazi vyetu vijavyo. Kwa hiyo, naomba nalo hili liwe Azimio la Bunge kwamba Maktaba ya Nyaraka za Taarifa zote za Gesi na Matufa ikarabatiwe na kuwekwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya na kwa ridhaa yako, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo katika Taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
(Makof)

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini - Mheshimiwa Victor Mwambalaswa kwa kuhitimisha hoja yako vizuri kabisa. Tunashukuru sana. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, kama alivyosema Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba sasa mpokee na mkubali Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini pamoja na Mapendekezo na Maoni yaliyomo katika ripoti hiyo. (*Makofî*)

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini Pamoja na Mapendekezo na Maoni yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Wote kabisa wameafiki. Nawashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge wote katika Kamati hii ya Nishati na Madini.

Tunajua kazi mliyonayo ni kubwa sana kwa niaba ya Bunge mmefanya kazi nzuri. Tunajivuna kwa kazi ambayo mmekuwa mkifanya, tunaomba mwendelee kufanya kazi yenu. Lakini pia tunashukuru sana kazi nzuri sana inayofanywa na Wizara ya Nishati na Madini katika kufuatilia masuala yote yanayohusiana na Wizara hii, na kwa kweli tunawatakia kila kheri katika malengo ambayo mmekuwa mkitueleza hapa ndani.

Tunatumaini kabisa kwamba mwakani wakati wa taarifa ijayo hali itakuwa bora zaidi kuliko hata ilivyo sasa.

Sasa moja kwa moja nimwite Mheshimiwa Cecilia Paresso kwa maelezo binafsi. Mheshimiwa Cecilia Paresso.

## HOJA BINAFSI YA MBUNGE

**Maelezo Binafsi ya Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso  
Kuhusu Hatua za Kuchukua ili Kudhibiti Ajali za  
Barabarani Hasa Nyakati za Sikukuu za  
Mwisho wa Mwaka na Mwaka Mpya**

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuwasilisha maelezo haya kwa Mujibu wa Kanuni ya 50 (1) (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na ajali mbaya sana za vyombo vyaa usafiri na usafirishaji hasa katika kipindi cha mwisho wa mwaka na mwanzo wa mwaka. Hili limekuwa likijirudia kwa kipindi kama hiki cha Mwezi Desemba karibu miaka yote na kupelekea wananchi kuona kama ni mazoea, wakati watu wanaendelea kupoteza maisha. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Gazeti la Habari leo la tarehe 19 Novemba, 2013 ni kwamba, Baraza la Taifa la Usalama Barabarani lilitikiria kuwepo kwa ongezeko la takwimu za ajali katika vipindi vyaa sikukuu za mwisho wa mwaka na mwanzo ya mwaka. Ajali, vifo na majeruhi vinatajwa kuongezeka katika kipindi hicho kutokana na makosa mbalimbali. Zipo sababu nydingi mtambuka zinazosababisha ajali ambazo zinazohusisha Idara na Taasisi mbalimbali. Nyingi ya sababu hizo ni kutokana na makosa ya kibinadamu kama vile ulevi, uzembe, mwendo kasi, uchakavu wa magari, ubovu na ufinyu wa barabara na ongezeko la vyombo vyaa usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Januari hadi Novemba, 2012, takwimu zinaonyesha kuwa matukio makubwa ya usalama barabarani yaliyoripotiwa ni 21,531 ikilinganishwa na matukio 22,208 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2011. Huu ni upungufu wa matukio 677 ambayo ni sawa na 3%. Sambamba na kupungua wa matukio makubwa ya usalama barabarani, matukio madogo

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[MHE. CECILIA D. PARESSO]*

ya usalama barabarani yamekuwa yakiongezeka ambapo jumla ya matukio madogo 548,600 yameripotiwa katika kipindi cha Januari hadi Novemba 2012, ikilinganishwa na matukio 397,292 yaliyopotiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2011. Hivyo kuna ongezeko la matukio 151,308 sawa na asilimia 27.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa idadi ya matukio makubwa imepungua, idadi ya ajali zilizosababisha vifo imeongezeka kutoka matukio 3,012 mwaka 2011 hadi matukio 3,144 mwaka 2012. Hili ni ongezeko la matukio 132 sawa na 4.3%. Idadi ya watu waliokufa mwaka 2012 ni 3,655 na waliojeruhiwa ni 18,348, ukilinganisha na kipindi kama hicho cha mwaka 2011 ambapo waliokufa walikuwa 3,682 na waliojeruhiwa 19,238.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 16.3 ya ajali nchini husababishwa na uendeshaji wa magari mabovu yasiyokidhi viwango vya ubora na asilimia 7.3 zinatokana na ubovu wa miundombinu, pamoja na mazingira ya barabarani kama vile magari kuharibika barabarani na kutokuwekwa kwa alama yoyote ya kuashiria kuwa gari lina matatizo. Aidha, kumekuwa na tabia ya madereva wazembe kuwapa utingo au makondakta wa magari hayo kuendesha huku wakielewa vyema kuwa wasaidizi hao hawana sifa za kuendesha magari hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi huu wa Desemba, 2013 ambao hata haujamalizika, takribani watu 31 tayari wamepoteza maisha kutokana na ajali za barabarani na zaidi ya watu 200 wamejeruhiwa katika ajali za barabarani. Hizi ni takwimu zilizopatikana katika vyombo vya habaari kuanzia tarehe 1 hadi tarehe 15 Desemba, 2013. Yamkini takwimu za vifo na majeruhi kutokana na ajali za barabarani zikawa zinaendelea kuongezeka ninapotoa maelezo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya Jeshi la Polisi kupitia Kitengo cha Usalama Barabarani ambao muda wote hufanya ukaguzi wa magari haya ya abiria katika vituo rasmi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. CECILIA D. PARESSOJ]

na maeneo mengine kwa kushtukiza, bado matukio ya ajali za barabarani yanaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kujiuliza, inakuwaje gari la abiria linapata ajali linaua watu wakati gari hilo limepita katika vituo kadhaa vyta ukaguzi? Inakuwaje wahusika wanashindwa kuona kama gari hilo lina matatizo? Hapa kuna tatizo la msingi la kufanya uchunguzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo lengo la msingi la maelezo haya kutaja sababu za ajali barabarani ingawa zimetajwa kwa uchache, nia yangu na msingi hasa wa maelezo haya ni kuitaka Serikali kupitia Mamlaka za usafiri kama vile *SUMATRA* na za usalama barabarani kama vile Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi madhubuti kuona kama kuna visababishi vingine vyta ajali na kuvidhibiti ili kuondokana na misiba ambayo ingeweza kuepukwa hasa nyakati hizi za sikukuu za mwisho wa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhamira hiyo, naitaka Serikali kupitia maelezo haya kufanya mambo yafuatayo ili kutokomeza vifo vinavyotokana na ajali barabarani:-

(i) Kufanya ukaguzi maalumu wa mabasi yote ya abiria kama yanakidhi vigezo vyta ubora wa kusafirisha abiria;

(ii) Kuweka katazo kwa mabasi ya abiria hasa ya Mikoani kubadili njia kwa tamaa ya kujipatia fedha nyingi hasa nyakati hizi za siku kuu za mwisho wa mwaka na mwaka mpya;

(iii) Kupiga marufuku upandishaji wa nauli kiholela unaofanywa na wamiliki wa magari ya abiria kwa kuwa nauli kubwa ndio kichocheo cha madereva kwenda mwendo kasi ili kufanya *route* nyingi ili kujipatia faida kubwa;

(iv) Kufanya uchunguzi maalumu wa matukio ya rushwa katika vituo vyta ukaguzi wa magari ya abiria, kwa kuwa magari mengine yanaonekana wazi kuwa ni mabovu, lakini bado yanaendelea kusafirisha abira; (*Makof*)

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[MHE. CECILIA D. PARESSO]*

(v) Kuhakikisha kuwa kila basi linalofanya safari ndefu kwenda Mkoani linapatiwa Askari mmoja wa Usalama Barabarani msindikizaji ili kuhakiki kwamba Sheria za Barabarani zinazingatiwa ili kuepuka ajali zinazoweza kuepukwa;

(vi) Kukarabati maeneo yote korofi ya barabara ambayo yamekuwa mojawapo ya visababishi vyta ajali;

(vii) Kutunga kanuni ambazo zitambana mmiliki wa gari la abira pamoja na dereva kulipa fidia kwa familia za wafiwa na majeruhi kutokana na ajali iliyo sababishwa kwa uzembe;

(viii) Kuweka vigezo maalumu katika kutoa leseni kwa madereva wa mabasi ya abiria kama vile kupima akili za madereva, mwenendo wao kitabla na afya zao kwa ujumla. Hii ni kwa sababu, kuna uwezekano dereva akawa ameathirika kiafya na hivyo kuwa na msongo wa mawazo jambo linaloweza kupelekeea ajali; na

(ix) Kuweka muda maalumu wa ukaguzi wa leseni ili kuona kama madereva bado wana sifa za kuendesha vyombo vyta usafirishaji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kutambua kwamba maelezo binafsi ya Mbunge hayajadiliwi Bungeni na wala Waziri anayehusika halazimiki kujibu hoja zilizomo katika maelezo haya, lakini itakuwa ni uungwana na busara ya hali ya juu kama Mawaziri wanachusika na uchukuzi na usalama wa raia wataona kuwa ni jambo ambalo halikubaliki kuendelea kupoteza maisha ya wananchi wasio na hatia kutokana na ajali barabarani na hivyo angalau kueleza japo kwa ufupi kuititia fursa ya kauli za Mawaziri juu ya mikakati au mipango waliyonayo ya kuondokana na kadhia hii. (*Makof*)

Aidha, nina imani kwamba kama Serikali itazingatia mapendekizo niliyotoa katika maelezo yangu, basi tunaweza kupunguza ajali za barabarani hasa nyakati hizi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. CECILIA D. PARESSO]

za sikukuu za mwisho wa mwaka na mwaka mpya kwa kiasi kikubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda kuchukua fursa hii kuwatakitia Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote heri ya Sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya wa 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Cecilia Paresso kwa maelezo hayo.

Waheshimiwa Wabunge, kutohana na muda wetu kama mnavyouona nyote na ratiba yetu ya siku ya leo ilikuwa *packed* sana, lakini tunamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa ushirikiano wenu tumemaliza siku ya leo salama.

Naomba basi niahirishe Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

(*Saa. 1.55 Usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,  
Tarehe 20 Desemba, 2013 Saa Tatu Asubuhi*)